

4 MEI, 2013

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Nane - Tarehe 4 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge Mkutano wa 11 unaendelea, kikao hiki ni cha 18.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:-**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

4 MEI, 2013

**MHE. OMAR R. NUNDU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA (K.n.y. MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014  
Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu ya Bajeti kwa mwaka 2013/2014 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Pili, nawashukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Namshukuru pia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa maelekezo anayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Nawathibitishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa ufanisi, uadilifu na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah (Mb.) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib (Mb.) kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati hiyo. Hali kadhalika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo. Ninawaomba Wajumbe hao wapokee shukurani zangu kwa maoni waliyotupatia wakati wa kuchambua mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014. Maoni na mapendekezo yao yametusaia sana katika kuiandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 28 Machi, 2013 Mbunge mwenzetu Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Jimbo la Chambani alifariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako Mheshimiwa Naibu Spika, familia, ndugu na marafiki kwa msiba huo. Namuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira na dhima ya Wizara ya Ulinzi na JKT. Dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwa Taasisi iliyotukuka ya kudumisha amani na usalama nchini. Kwa kuzingatia kwamba ulinzi wa Taifa ndilo jukumu la kwanza kwa Serikali, dhima ya Wizara hii ni kuilinda mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya

maadui kutoka nje au ndani ya nchi na kuhakikisha kuwa uhuru na maslahi ya Taifa letu (national interests) yanakuwa salama wakati wote. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu inaendelea kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966 Sura 192 na Sheria ya JKT ya mwaka 1963 Sura 193, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekabidhiwa jukumu la kusimamia Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa katika kutekeleza majukumu yake. Vile vile Wizara yangu ina wajibu wa kuvipatia vyombo hivi mahitaji yake ya kimsingi ili kuviwezesha kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ina majukumu saba.

Kwanza, Wizara ina jukumu la kulinda mipaka ya nchi yetu.

Pili, Wizara ya Ulinzi inasaidiana na Mamlaka za kiraia katika kukabiliiana na majanga ili kuwapatia wananchi waliofikwa na majanga misaada ya kibinadamu.

Tatu, Wizara inashiriki katika shughuli za Ulinzi wa Amani katika nchi zenye migogoro duniani.

Nne, Wizara hii inaandaa umma wa Watanzania kushiriki katika shughuli za Ulinzi wa Taifa.

Tano, Wizara inawajengea vijana wa Kitanzania moyo wa uzalendo na mshikamano wa kitaifa ili kuwaandaa kikamilifu katika kutekeleza shughuli za kujitegemea.

Sita, Wizara ya Ulinzi inafanya utafiti ili kuendeleza teknolojia kuhusu matumizi ya kijeshi na kiraia.

Saba, Wizara hii inaimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika masuala ya Kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu niliyoyataja hapo awali, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imejiwekea malengo makuu manane kwa mwaka 2013/2014. Kwanza, kuandikisha Wanajeshi wapya kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa. Pili, kuwaendeleza kielimu maafisa na askari wa JWTZ na JKT. Tatu, kununua na kulipatia Jeshi zana bora kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa.

Nne, kutunza na kuhifadhi vizuri zana za kijeshi na kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi na makazi kwa Wanajeshi. Tano, kuimarisha mahusiano mema na nchi nyingine duniani katika masuala ya kijeshi. Sita, kutoa mafunzo ya ulinzi wa mgambo kwa Watanzania ili kuimarisha Jeshi la Akiba. Saba, kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya kuwajengea nidhamu, ukakamavu na moyo wa uzalendo. Nane, kuyajengea mashirika ya Mzinga, Nyumbu na SUMAJKT mazingira bora ya kukuza teknolojia ili yaweze kujitegemea na kupunguza utegemezi kwa ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2012/2013, tulipokea maoni, ushauri na maelekezo kutoka kwa iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na majibu yake yameainishwa. Hali kadhalika, hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huo pia zimezingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka 2013/2014 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jukumu kubwa la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kulinda uhuru na usalama wa nchi yetu naomba nieleze hali ya usalama wa mipaka yetu na nchi nyingine ilivyokuwa katika mwaka 2012/2013. Hali ya usalama wa mipaka yetu na nchi jirani, nchi kavu na baharini ni shwari kwa ujumla. Hata hivyo katika baadhi ya mipaka yetu na nchi za Uganda, Kenya na Zambia kuna tatizo la muda mrefu la kung'olewa kwa alama za mipakani yaani "*beacons*". Wizara yangu kwa kushirikiana

na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa zinaendelea kulifanyia kazi suala hili ili kuzirudisha alama hizo kwenye eneo la mpaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpaka katika Bahari ya Hindi. Hali ya Usalama katika eneo la mpaka wa Bahari ya Hindi lenye urefu wa kilomita 1,424 ambako nchi yetu inapakana na Kenya, Visiwa vya Ushelisheli, Komoro na Msumbiji inaendelea kuwa shwari. Hivi sasa matukio ya uharamia yaliyokuwa yakitokea miaka mitatu iliyopita yamepungua kwa kiasi kikubwa. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2012 hadi sasa hakujatokea tukio lolote la uharamia katika eneo hili. Mafanikio haya yanatokana na doria zinazofanywa na Jeshi la Wananchi kupitia Kamandi yake ya Wanamaji pamoja na ulinzi unaofanywa na majeshi ya Ulaya, Asia na Marekani katika eneo la Ghuba ya Aden.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Usalama katika mpaka huu wenye urefu wa kilometa 1,190 ambako Tanzania inapakana na Kenya na Uganda inaendelea kuwa shwari. Hata hivyo kumejitokeza tatizo la wahamiaji haramu kutoka Ethiopia na Somalia wanaoingia nchini kwa kupitia kwenye mpaka wetu na nchi jirani. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi zimekuwa zikiwasaka wahamiaji haramu pamoja na kuwatafuta Mawakala wa biashara hiyo ili kuwachukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpaka wa Kaskazini. Hali ya Usalama katika mpaka huu wenye urefu wa kilomita 1,220 ambako Tanzania inapakana na Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni shwari. Jeshi la Wananchi wa Tanzania linaendelea kudumisha ulinzi katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Ili kuimarisha ulinzi wa eneo hilo Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatarajia kupata boti 2 za kisasa mwishoni mwa mwaka huu ambazo zitatumika kufanyia doria katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpaka wa Kusini Tanzania inapakana na Msumbiji, Malawi na Zambia. Hali ya usalama katika mpaka wetu wa kusini wenye urefu wa kilomita 759 zikiwemo kilomita 36 za maji kwenye Ziwa Nyasa ni shwari. Kuhusu mgogoro wa mpaka katika Ziwa Nyasa kati ya Malawi na Tanzania mazungumzo bado yanaendelea. Mazungumzo haya yanaratibiwa na Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto mbalimbali nilizoieleza hapo awali, napenda kuwahakikishia wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla kwamba ulinzi wa mipaka yetu ni imara. Jeshi letu liko makini na linaendelea kuchukua tahadhari kwa kuimarisha vikosi vyake ili kudumisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2012/2013. Naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/2013. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiriya kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 57,650,000.00 kutoka katika Mafungu yake matatu (yaani Fungu 38 – NGOME, Fungu 39 – JKT na Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi). Hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Mafungu hayo matatu yalikusanya mapato ya jumla ya Shilingi 27,584,536.00 sawa na asilimia 47.8 ya makadirio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya shilingi 1,086,550,058,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika Mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, shilingi 678,363,492,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 408,186,566,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 718,855,852,627.00 sawa na asilimia 66 ya Bajeti yake. Kati ya fedha hizo shilingi 583,155,852,627.00 zilikuwa ni kwa Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, fedha zilizopokelewa ni Shilingi 135,700,000,000.00 sawa na asilimia 33 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya fedha zilizopokelewa inaonesha kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida hadi mwezi Machi 2013 kwa ujumla ulikuwa ni wa kuridhisha. Fedha kwa ajili ya mishahara na marupurupu zilipokelewa kulingana na makisio ya bajeti. Hata hivyo, fedha zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za Maendeleo zilikuwa kidogo ukilinganisha na mahitaji. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Wizara ilipata wastani wa asilimia 33 tu ya fedha zilizoidhinishwa kwa Matumizi ya Maendeleo. Hali hii imeathiri utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo yake, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali. Kwa upande wa Matumizi ya Kawaida, shughuli zilizokusudiwa kutekelezwa ni pamoja na kulipa stahili mbalimbali za Wanajeshi, vijana walioko katika mafunzo ya JKT na watumishi wa umma, kusafirisha wastaafu, kutoa huduma muhimu za chakula, tiba, sare na usafiri kwa Wanajeshi na vijana walioko katika mafunzo ya JKT. Wizara pia ilipanga kulipia huduma za umeme, maji, simu na mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu ya ulinzi, kuimarisha mafunzo ya kijeshi, kuendesha mafunzo ya ulinzi wa mgambo na kutengeneza magari na zana za kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Bajeti ya Maendeleo, Wizara ya Ulinzi iliweza kulipia mikataba ya ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi, kujenga maghala ya kuhifadhia silaha na ujenzi wa mahanga ya kuhifadhia zana mbalimbali. Shughuli nyingine ni pamoja na kumalizia ujenzi wa majengo mbalimbali, kukarabati miundombinu katika makambi, kurejesha mikopo ya mikataba ukiwemo wa *NSSF*, kulipia sehemu ya malipo ya awali ya mkopo kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za wanajeshi, kuboresha kiwanda cha Shirika la Mzinga, kukarabati mitambo na miundombinu kwa ajili ya kuboresha shughuli za utafiti katika Shirika la Nyumbu, kupima na kulipa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya shughuli za Jeshi. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi. Suala la kuwajengea weledi maafisa na askari wetu limeendelea kupewa uzito mkubwa unaostahiki. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2012/2013 maafisa na askari wetu walishiriki katika mazoezi mbalimbali ya medani katika ngazi ya brigedi likiwemo zoezi kubwa la Ongeza Nguvu lililofanyika katika brigedi ya kusini mwezi Novemba, 2012. Wanajeshi wetu pia wameshiriki katika mazoezi ya pamoja chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Malengo ya mafunzo hayo ni kuwajengea Wanajeshi uwezo wa kukabiliana na matishio mapya yakiwemo ugaidi, uharamia baharini, uhamiaji haramu na maafa. Vilevile maafisa na askari wamehudhuria kozi mbalimbali katika shule na vyuo ndani na nje ya nchi kikiwemo Chuo cha Taifa cha Ulinzi (*National Defence College*) ambacho kimeanza kozi yake ya kwanza inayowahusisha Maafisa Wakuu kutoka Majeshi ya Ulinzi na Usalama na Maafisa Waandamizi Serikalini. Kozi hiyo inayowashirikisha wanafunzi 20 ilianza rasmi tarehe 3 Septemba, 2012 na inatarajiwa kumalizika tarehe 20 Julai, 2013. Hali kadhalika, wanajeshi wetu wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya zana mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kutoa mafunzo ya ulinzi wa mgambo kama sehemu muhimu ya Jeshi la akiba. Katika mwaka 2012 wanamgambo 11,482 walihitimu mafunzo hayo katika sehemu mbalimbali nchini. Aidha, mafunzo ya Uongozi mdogo wa mgambo yaliendeshwa huko "*Kunduchi Training Camp*" (KTC), Dar es Salaam na wanafunzi 39 walihitimu mafunzo hayo. Jeshi la Ulinzi pia limeendelea kutoa mafunzo ya ulinzi shirikishi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola ili kukabiliana na uhalifu nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za tiba na upatikanaji wa dawa kwa maafisa, askari, watumishi wa umma na wanajeshi wastaafu zimeendelea kutolewa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati za Jeshi 70 zilizoko katika vikosi mbalimbali nchini. Huduma hizo ambazo pia hutolewa

kwa wananchi hususan wanaoishi katika maeneo jirani na vituo hivyo vya afya zimetolewa kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi imekuwa ikilipia gharama za shughuli mbalimbali zikiwemo doria za mipakani, operesheni za kijeshi na kufungua *'detachment'*. Vile vile Wizara yangu imelipia huduma muhimu zikiwemo mafuta, umeme, maji na simu. Wizara pia imepata zana na vifaa vipya vya kijeshi yakiwemo magari ya huduma kwa wanajeshi. Hata hivyo, ununuzi wa zana na magari mapya umeongeza kiwango cha mahitaji ya mafuta ikilinganishwa na bajeti iliyotolewa. Kutokana na hali hiyo Wizara yangu imelazimika kulimbikiza madeni yenye thamani ya shilingi 35,496,809,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jukumu la Jeshi la Wananchi wakati wa amani ni kushirikiana na Mamlaka za Kiraia kukabiliana na majanga au maafa pale yanapotokea. Katika kutekeleza jukumu hilo, Jeshi la Wananchi lilishiriki katika kutoa misaada katika maafa makubwa matatu: Ajali ya kuzama kwa meli ya MV Skargate tarehe 18 Julai, 2012; ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16 iliyotokea katika Jiji la Dar es Salaam tarehe 29 Machi, 2013.

Vile vile tarehe 1 Aprili, 2013 Jeshi lilishiriki katika kutoa msaada katika eneo la Moshono huko Arusha kufuatia maporomoko ya udongo katika machimbo ya moramu yaliyosababisha watu 13 kupoteza maisha yao. Katika kutekeleza jukumu hilo Jeshi letu lilishirikiana na mamlaka za kiraia katika shughuli za uokoaji wa majeruhi na uopoaji wa miili ya marehemu. Mbali na kushiriki katika kukabiliana na maafa, Jeshi pia limeshiriki katika zoezi la kusomba mahindi kutoka Laela kwenda Vwawa (Mbozi) tani 4,772, kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda tani 20,000 na kutoka Makambako kwenda Shinyanga tani 3,600. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza maafisa, askari na watumishi wa umma wote walioshiriki katika kutoa msaada wakati wa maafa na kwenye operesheni ya kusomba mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013 Jeshi la Wananchi, Jeshi la Kujenga Taifa na Mashirika yake yameshiriki katika shughuli mbalimbali za Kitaifa. Shughuli hizo ni pamoja na Maonesho ya Sabasaba, Nane nane, na Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 51 ya Uhuru wa Tanzania Bara na Miaka 49 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, majeshi hayo yalitoa timu ambazo zilishiriki mashindano katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu Jeshi la Wananchi limekuwa likikabiliwa na uhaba mkubwa wa nyumba kwa ajili ya maafisa na askari. Hivi karibuni Serikali imepata mkopo wa ujenzi wa nyumba kutoka benki ya Exim ya China. Hivi sasa taratibu za kutekeleza mradi wa ujenzi zimekamilika.

Katika mradi huo tutaanza na ujenzi wa nyumba 6,064 katika awamu ya kwanza kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 300, ambapo Dola za Kimarekani milioni 285 ni mkopo kutoka *Exim Bank* ya China na Dola za Kimarekani milioni 15 zimetolewa na Serikali ya Tanzania. Wizara ya Ulinzi tayari imelipa Dola za Kimarekani milioni 5 za malipo ya awali zinazotakiwa kulipwa kwa mujibu wa mkataba. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2013. Mkandarasi wa mradi huo ni Kampuni ya *Shanghai Construction (Group) General Company* kutoka China. Nyumba hizo zitajengwa katika vikosi 37 vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kigoma, Morogoro, Pemba, Pwani na Tanga.

Ujenzi huu unatarajiwa kuchukua muda wa miezi 50 hadi kumalizika kwake. Mazungumzo ya kupata fedha za ujenzi wa nyumba takribani 4,000 katika awamu ya pili yanaendelea. Vile vile awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhi silaha umeanza kutekelezwa. Awamu ya pili ya ujenzi wa maghala hayo itaanza katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha

Jeshi la Wananchi kwa kulinunulia zana na vifaa vya kisasa. Nafurahi kuarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jeshi limeanza kupokea baadhi ya zana na vifaa hivyo. Tayari vifaa hivyo vimeshaanza kutumika katika shughuli za ulinzi na mafunzo. Hapana shaka hatua hii pia inatarajiwa kuongeza gharama za uendeshaji, utunzaji na matengenezo ya zana. Jeshi la Wananchi litajitahidi kuvitunza na kuvifanyia matengenezo vifaa na zana kwa wakati ili kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inaendelea kuimarisha ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi na nchi mbalimbali duniani zikiwemo China, Ujerumani, India, Marekani, Umoja wa Falme za Kiarabu na Canada. Kwa ujumla ushirikiano huo umekuwa wa manufaa makubwa kwa nchi yetu. Kupitia ushirikiano huo, nchi hizi zimeendelea kutoa misaada mbalimbali kwa nchi yetu kama vile zana, mafunzo, wataalamu na vifaa vya hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi baina ya nchi na nchi umekuwepo pia ushirikiano wa kikanda katika nyanja hizo. Tanzania imeshirikiana na nchi nyingine katika Jumuiya za *EAC* na *SADC*. Majeshi ya nchi hizi yamefanya mazoezi ya pamoja ambapo mwaka 2012 lilifanyika zoezi la Medani (*Field Training Exercise – FTX 2012*) lililoitwa “*ZOEZI USHIRIKIANO IMARA 2012*” huko Nyakinama, Rwanda. Vile vile majeshi hayo yanatarajia kushiriki katika zoezi la *Command Post Exercise – CPX* litakalofanyika nchini Burundi mwaka huu 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa ikiimarisha ushirikiano wake na nchi za *SADC*. Kwa kipindi kirefu nchi yetu inatoa nafasi za mafunzo katika chuo cha Ukamanda na Unadhimu, Arusha kwa nchi za Afrika Kusini, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia, Zambia na Zimbabwe. Aidha, katika kukabiliana na tishio la uharamia kwenye Bahari ya Hindi, Tanzania imesaini makubaliano ya kupambana na uharamia na nchi za Afrika Kusini na Msumbiji. Tanzania pia ilikuwa ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Majeshi ya Wanamaji wa *SADC* (*Standing Maritime Committee*)

ambapo kikao cha mwaka cha Kamati hiyo kilifanyika Tanzania kati ya tarehe 18 hadi 22 Februari, 2013. Katika kipindi hiki kumefanyika mikutano na vikao mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika Jumuiya za *SADC*. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeshiriki katika mikutano na vikao hivyo ili kujadili masuala ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi kimataifa, Jeshi la Wananchi limeshiriki katika operesheni mbalimbali za kulinda amani zinazoongozwa na Umoja wa Mataifa katika nchi zenye migogoro. Hadi sasa kuna jumla ya maafisa na askari 1,081 wa Jeshi la Wananchi wanaoshiriki operesheni hizo katika nchi za Lebanon na Darfur.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lina uzoefu mkubwa katika kuwalea vijana. Mafunzo ya JKT yana manufaa makubwa kwa Taifa letu kwa sababu yanawaandaa vijana kuwa wazalendo, wenye maadili mema na moyo wa ujasiri. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa Jeshi la Kujenga Taifa litafikisha miaka 50 ifikapo Julai mwa huu tangu lianzishwe. Tuna Viongozi wengi waliopata mafunzo haya ya JKT. Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano ni mmoja wa Viongozi hao. Hapana shaka mafunzo ya JKT yanamfanya kijana ajiamini, awe mvumilivu, mzalendo na jasiri katika kukabiliana na matatizo ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu huu wa JKT, uamuzi wa kusitisha mafunzo haya uliwanyima vijana fursa ya kupata malezi mema ya kuwajengea uzalendo na umoja. Ndio maana hivi sasa tunashuhudia mmong'onyoko wa maadili miongoni mwa vijana. Kwa kutambua ukweli huu Serikali yenu imeamua kurudisha mafunzo haya. Naupongeza uamuzi wa Serikali wa kurudisha mafunzo ya vijana wa JKT kwa Mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013 Jeshi la Kujenga Taifa lilichukua idadi ya vijana wa kujitolea 12,620 katika makundi mawili. Kundi la kwanza la

Operesheni Sensa lenye idadi ya vijana 5,898 (wavulana 4,576 na wasichana 1,322) liliandikishwa mwezi Agosti 2012. Vijana hao wamehitimu mafunzo yao ya awali na kwa sasa wapo katika makambi ya Burombola na Kanembwa (Kigoma), Chita (Morogoro), Mafinga (Iringa), Makutupora (Dodoma), Maramba na Mgambo (Tanga), Mgulani (Dar es Salaam), Mlale (Ruvuma), Msange (Tabora), Nachingwea (Lindi), Oljoro (Arusha) na Rwamkoma (Mara) wakiendelea na mafunzo ya stadi za kazi. Kundi la pili la Operesheni Miaka 50 ya JKT lenye idadi ya vijana 6,722 (kati yao wavulana 5,227 na wasichana 1,495) limeanza mafunzo yake tarehe 4 Machi, 2013.

Mafunzo hayo yanaendeshwa katika makambi ya Bulombora, Kanembwa, Maramba, Mgambo, Mlale, Msange, Ruvu na Rwamkoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2012/2013 niliahidi kwamba Wizara yangu itarejesha mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kuanzia mwaka 2013. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ahadi hiyo imetekelezwa ambapo awamu ya kwanza ya mafunzo hayo ya miezi mitatu ilianza tarehe 04 Machi, 2013 kwa kuchukua vijana 4,710. Mafunzo hayo yalizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 26 Machi, 2013 katika Kambi ya Ruvu. Vijana waliochukuliwa ni miongoni mwa vijana 41,348 waliohitimu mafunzo ya Kidato cha Sita katika mwaka 2013.

Aidha, vijana 36,638 waliobaki watachukuliwa katika mwaka 2013/2014 kwa awamu tatu. Mafunzo hayo yatafanyika kwa muda wa miezi mitatu katika makambi ya Bulombora, Kanembwa, Maramba, Mgambo, Mlale, Msange, Ruvu na Rwamkoma. Utaratibu huu wa kuchukua vijana kwa Mujibu wa Sheria hautaathiri mafunzo ya vijana wanaotaka kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa utaratibu wa kujitolea. Jeshi la Kujenga Taifa litaendelea kuwachukua vijana wa kujitolea kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imepokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wanaoeleza kwamba muda wa miezi mitatu uliopangwa kwa Vijana wa Mujibu wa Sheria ni mfupi sana na kwa hiyo wanapendekeza muda huo uwe angalau miezi sita. Napenda kuliarifu bunge lako Tukufu kwamba Serikali haina kipingamizi katika kutekeleza jambo hili ila tatizo kubwa linalotukabili katika kutekeleza dhamira hiyo ni ufinyu wa bajeti inayotolewa ukilinganisha na idadi ya wahitimu wa kidato cha sita. Iwapo bajeti ya mafunzo haya itaongezeka basi taratibu za kuongeza muda zitafanywa ikizingatiwa kuwa JKT imeandaa Makambi yenye uwezo wa kuchukua vijana 20,000 kwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara yangu mwaka jana tulipokea ombi la Waheshimiwa Wabunge kuandaliwa mafunzo maalum ya Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imelifanyia kazi ombi hilo na kuandaa utaratibu wa mafunzo maalum ya wiki tatu kwa Waheshimiwa Wabunge. Mafunzo hayo yalianza rasmi tarehe 4 Machi, 2013 na kufungwa tarehe 26 Machi, 2013 na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Ufungaji huo wa mafunzo ya Waheshimiwa Wabunge ulikwenda sambamba na kuzinduliwa kwa mafunzo ya vijana kwa Mujibu wa Sheria. Wabunge 24 kati ya 47 waliojiandikisha kwa hiari yao walihudhuria mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya Waheshimiwa Wabunge 24 walioanza mafunzo yao ni Waheshimiwa Wabunge 22 ndiyo waliomaliza mafunzo yao. Naomba Bunge lako Tukufu liwatambue Waheshimiwa Wabunge hao ni:- Mhe. Abdallah Haji Ally (Mb.), Mhe. Halima Mdee (Mb.), Mhe. Anthony G. Mbassa (Mb.), Mhe. David Ernest Silinde (Mb.), Mhe. Esther Amos Bulaya (Mb.), Mhe. Zitto Zuberi Kabwe (Mb.), Mhe. Iddi Azan (Mb.), Mhe. Livingstone John Lusinde (Mb.), Mhe. Menrad Lutengano Kigola (Mb.), Mhe. Meshack J. Opolukwa (Mb.), Mhe. Multazar Mangungu (Mb.), Mhe. Mwigulu L. Nchemba (Mb.), Mhe. Said Mohamed Mtanda (Mb.), Mhe. Suleiman Said Jafo (Mb.), Mhe. Yahya Kassim Issa (Mb.), Mhe.

Yusuph Haji Khamis (Mb.), Mhe. Mariam Kasembe (Mb.), Mhe. Mariam Salum Msabaha (Mb), Mhe. Neema Mgaya Hamid (Mb.), Mhe. Raya I. Khamis (Mb.), Mhe. Ritta Enespher Kabati (Mb.) na Mhe. Sabreena Sungura (Mb.). Waheshimiwa Wabunge wawili walipatwa na maradhi na hivyo kutomaliza mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1982 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa amri ya kuundwa kwa Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT) chini ya Sheria ya *The Corporation Sole Establishment Act No. 23 of 1974*. Amri hiyo ilitolewa katika Tangazo la Serikali Namba 116 la mwaka 1982. Lengo la kuanzishwa kwa SUMAJKT ni kuwa na Shirika linalojiendesha kibiashara ili kupunguza utegemezi kwa Serikali katika kuendesha shughuli za JKT na hatimaye liweze kuchangia katika maendeleo ya nchi kwa ujumla. Katika kutekeleza majukumu yake SUMAJKT linaendesha miradi mbali mbali ya shughuli za kilimo na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa shirika la SUMAJKT lina kampuni tanzu ya ujenzi ya *National Service Construction Department* inayofanya kazi kupitia kanda zake tano za ujenzi (Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza). Kanda hizi zinatekeleza majukumu yake baada ya kusajiliwa na Bodi ya Usajili ya Makandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza shughuli za kilimo SUMAJKT imepewa maagizo makuu mawili ambayo ni uzalishaji wa mbegu bora na mpango wa kujitosheleza kwa chakula katika Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa SUMAJKT inazalisha mbegu bora kwa kushirikiana na Makampuni ya *Agricultural Seeds Agency, Tanseeds, Southern Highland Seed Growers na Sub Agro Ltd*. Ili Jeshi la Kujenga Taifa liweze kuzalisha mbegu bora katika kiwango kinachotakiwa na kuweza kutekeleza agizo la Serikali kikamilifu linahitaji mtaji mkubwa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa pembejeo, zana za kilimo (*combine harvesters na tractors*) na mtambo wa kusindika mbegu bora.



Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa kujitosheleza kwa chakula. Jeshi la Kujenga Taifa linategemea kuchukua vijana 41,000 kwa mujibu wa sheria na 10,000 wa kujitolea. Ili Jeshi la Kujenga Taifa liweze kuwalisha vijana hawa kwa mwaka linahitaji unga wa mahindi tani 4480, mchele tani 5,039.82, maharage tani 1,119.96, ngano tani 5,000, mafuta ya kula tani 3,957.192, nyama tani 389,225, mboga mboga na viungo tani 320.13 na matunda tani 2,799.9. Jeshi la Kujenga Taifa limekusudia kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kukidhi mahitaji ya chakula kwa vijana na biashara. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Vikosi vya 842 KJ (Mlale), 835 (Mgambo) na 844 KJ (Itende) vimepewa jukumu la kuzalisha mahindi.

(b) Kikosi cha 837 KJ (Chita) kimepewa jukumua la kuzalisha mpunga.

(c) Vikosi vya 824 KJ (Kanembwa), 833 KJ (Oljoro) na Kambi ya Mtabila vimepewa jukumu la kuzalisha maharage.

(d) Vikosi vya 823 KJ (Msange), 821 KJ (Bulombora), na 834 KJ (Makutupora) vimepewa jukumu la kuzalisha mawese, karanga na alizeti za kutosha ili kusindika mafuta.

(e) JKT lina mpango wa kuboresha ufugaji ng'ombe wa nyama 833 KJ (Oljoro) na 841 KJ (Mafinga) na ufugaji kuku wa nyama na mayai huko 832 KJ (Ruvu) ili kuzalisha nyama na mayai ya kutosha.

(f) 832 KJ (Ruvu) na 834 KJ (Makutupora) vimepewa jukumu la kuzalisha aina mbalimbali za mboga na viungo.

(g) 835 KJ (Mgambo), Mtabila na 824 KJ (Kanembwa) vimepewa jukumu la kuzalisha matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapana shaka utekelezaji wa miradi hii ya kilimo na ufugaji inahitaji mtaji mkubwa. Jeshi la Kujenga Taifa linahitaji shilingi 13,867,656,392 kwa ajili ya ununuzi wa mbegu, madawa ya magugu na zana za kilimo ambapo uzalishaji wa mahindi utahitaji shilingi 2,630,550,000.00, mchele shilingi 1,989,500,000.00, maharage shilingi 863,190,000.00, mafuta ya kula shilingi 385,050,000.00, mboga na viungo shilingi 398,417,500.00 na nyama shilingi 7,600,948,892.00. Kwa kuwa SUMAJKT haiwezi kupata fedha hizi kwa kupitia bajeti, Wizara yangu imeagiza itafute wawekezaji kutoka ndani au nje watakaoweza kushirikiana nao katika shughuli za kilimo na ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili SUMAJKT iweze kuendesha shughuli zake kitaalamu inahitaji kuimarisha utendaji wake. Nimeuagiza Uongozi wa SUMAJKT kutafuta wataalamu wa masuala ya biashara, kilimo, ufugaji na ujenzi. Vile vile nimeliagiza Shirika hilo litafute mikopo yenye riba nafuu kutoka mabenki ili kuendesha miradi yake kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Matrekta; wakati wa Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2012/2013 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, Serikali kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) lilipata mkopo kutoka Serikali ya India wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 40.

Kupitia mkopo huo, SUMAJKT waliingiza matrekta, zana na vifaa vya kilimo vyenye thamani ya shilingi 69,146,318,781.00. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kufikia mwezi Septemba 2012 matrekta 1,833 yalikuwa yameuzwa, ambapo kati yake matrekta 275 yameuzwa kwa fedha taslimu shilingi 8,270,481,780.00. Aidha, matrekta 1,558 na zana za kilimo zenye thamani ya shilingi 53,675,837,001.00 ziliuzwa kwa mkopo kwa wadau mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Wilaya, vikundi vya uzalishaji mali, SACCOs, na watu binafsi wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, urejeshwaji wa mkopo unakwenda sambamba na mikataba iliyosainiwa. Mpaka sasa jumla ya shilingi 14,575,490,929.00 zimerejeshwa. Hata hivyo, Shirika bado lina zana za kilimo na vipuri vyenye thamani ya shilingi 7,200,000,000.00. Miongoni mwa zana hizo ni pamoja na *power tillers*, pampu za umwagiliaji, *trailers*, *rotavator*, na *seed drill*. Kufuatia mafanikio ya mradi huo, tumepokea maombi mbalimbali kutoka kwa wananchi yanayofikia 4,000 ya kuuziwa matrekta.

Kati ya maombi hayo waombaji 73 wamekwisha toa fedha za utangulizi (*deposit*) kiasi cha shilingi 273,603,599.00. Kwa ujumla mradi wa matrekta umetekelezwa vizuri na mahitaji yameonekana kuwa makubwa. Kutokana na mahitaji yaliyopo mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya India kuhusu Awamu ya Pili ya mkopo wa matrekta wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 92 yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shughuli za Shirika la Mzinga. Katika mwaka 2012/2013 Wizara ya Ulinzi na JKT imeendelea kuimarisha shirika la Mzinga. Shirika hili linaendelea na uzalishaji kufuatia kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ukarabati wa kiwanda cha uzalishaji wa mazao ya kijeshi. Shirika linaendelea kufanya jitihada za kupata malighafi pamoja na kukuza ujuzi wa wafanyakazi wake ili kuongeza tija na ufanisi. Hata hivyo, utekelezaji wa malengo haya utategemea sana upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya sheria ya Makampuni Sura 212 Shirika la Mzinga limeweza kuanzisha kampuni tanzu ya Mzinga Holdings ili kulipatia Shirika hilo mapato na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini. Hivi sasa Mzinga Holdings imefanikiwa kupata miradi midogo ya ujenzi wa majengo.

Aidha, Wizara imeipa Mzinga Holdings jukumu la kuendesha maduka yasiyolipiwa kodi (*Duty Free Shops*) kwa ajili ya kuwahudumia wanajeshi na familia zao vikosini. Mpaka sasa kampuni hiyo imeshafanya ukarabati wa majengo katika

vikosi vya 24 KJ Kigoma na 23 KJ Biharamulo. Duka la Kigoma tayari limeanza kutoa huduma kwa wanajeshi na lile la Biharamulo linatarajiwa kuanza kazi ifikapo mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Mzinga Holdings pia lina mpango wa kuanzisha maduka yasiyolipiwa kodi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kagera, Mwanza na Shinyanga. Hivi sasa Shirika hilo linaendelea na taratibu za kupata hati miliki za viwanja katika Mikoa hiyo. Ili kutekeleza azma hii Shirika linahitaji shilingi bilioni 6.5. Kwa kuwa Shirika hili haliwezi kupata fedha zote kwa mara moja litatekeleza miradi hii kwa awamu kutokana na makusanyo ya fedha zitakazopatikana katika miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shughuli za Shirika la Nyumbu. kwa upande wa Shirika la Nyumbu, Shirika hili limekusudia kuimarisha shughuli za utafiti katika teknolojia ya mambo ya kijeshi. Shirika la Nyumbu limeweza kufanya utafiti katika teknolojia za magari, uhandisi na miundombinu ya majengo. Katika tafiti zake Shirika limekamilisha matengenezo ya gari la deraya kwa ajili ya kutumika katika sekta ya ulinzi. Aidha, utafiti wa gari la nyumbu kwa ajili ya matumizi ya kijeshi umeendelea kuimarishwa.

Vile vile Shirika la Nyumbu linaendelea na utafiti wa kuzalisha mtambo wa kuchuna mkonge ili kupata nyuzi na pampu za umwagiliaji. Aidha, utafiti kuhusiana na "engine" na "gearbox" kwa ajili ya matumizi kwenye matrekta madogo unaendelea vizuri. Shughuli za uzalishaji wa vipuri vya mashine zinazotumika kwenye viwanda na mitambo pia unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtandao wa Mawasiliano Jeshini; Mtandao wa Mawasiliano Jeshini; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kuboresha Mtandao wa Mawasiliano Jeshini ili uweze kutoa huduma za mawasiliano bila ya kutegemea mitandao ya kibiashara ya simu. Kazi hii imegawika katika awamu mbili.

Katika awamu ya kwanza mradi umekusudia kuboresha mawasiliano ya ndani ya vikosi. Katika awamu ya

pili mradi una lengo la kuimarisha mawasiliano kati ya kikosi na kikosi kwa kutumia mfumo wa *satellite*. Sambamba na jitihada hizo, Wizara inatekeleza mradi wa mawasiliano salama utakaowezesha kuwepo mawasiliano ya kisasa baina ya vikosi vya Jeshi nchi nzima. Utekelezaji wa mradi huo ulianza mwezi Novemba, 2012 hadi sasa umefikia asilimia 30. Mradi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upimaji na Ulipaji kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi. Jeshi la Wananchi wa Tanzania lina mahitaji makubwa ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa makambi, makazi ya wanajeshi na maghala ya kuhifadha silaha. Vile vile Jeshi linahitaji ardhi kwa ajili ya kuendeshea mafunzo na mazoezi ya kijeshi.

Kutokana na mgongano kati ya mahitaji ya ardhi kwa Jeshi na Wananchi, Wizara yangu imekuwa ikikabiliwa na migogoro mingi. Kwa kuwa maeneo mengi ya Jeshi hayajapimwa, wananchi hutumia fursa hiyo kuyavamia. Hivi sasa kuna maeneo yapatayo 80 yenye migogoro katika mikoa mbalimbali. Kwa bahati mbaya upimaji wa maeneo ya Jeshi haufanyiki kwa kasi kutokana na ufinyu wa bajeti.

Wizara yangu ina mpango wa kununua vifaa vya kisasa vya kupimia ardhi kwa matarajio kwamba kazi ya upimaji itafanywa kwa haraka zaidi na hatimaye kuepusha uvamizi wa maeneno ya Jeshi unaofanywa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua kadhaa kutatua migogoro hiyo ikiwemo upimaji na ulipaji wa fidia ya ardhi zilizochukuliwa na Jeshi. Wizara imekamilisha kulipa fidia katika eneo la Kiharaka (Mapinga) mkoani Pwani. Aidha, katika mwaka huu wa fedha Wizara ina mpango wa kulipa fidia ya maeneo ya Mwakidila –Tanga, Cheyo – Tabora na Mwantini – Shinyanga. Wizara yangu itaendelea kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi mbalimbali kadri hali ya upatikanaji wa fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa kupambana na UKIMWI; Wizara ya ulinzi imeendelea

kutekeleza mkakati wa kupambana na maambukizi ya UKIMWI kwa kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga ili kuzuia maambukizi mapya.

Wizara imekuwa ikihimiza upimaji wa hiari kwa maafisa, askari na watumishi wa umma na vijana wa JKT kwa kutumia waelimishaji rika. Aidha, kwa wale ambao tayari wameshathibitika kuwa wameambukizwa virusi vya UKIMWI wamekuwa wakipatiwa dawa za kupunguza makali ya virusi (ARVs) bure katika vituo vya huduma na matibabu (care and treatment centres) vilivyoko katika hospitali kuu za kanda na huduma ya lishe katika maeneo ya kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Mazingira; katika kuendeleza hifadhi ya mazingira, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatekeleza zoezi la kudumu la upandaji miti katika maeneo ya vikosi vyote ya Jeshi.

Aidha, Wizara inaendelea kuvihimiza vikosi kuweka miundombinu ya kudhibiti majitaka kama vile kujenga mabwawa ya maji taka (*sewers septic tanks*) na kujenga vyoo bora katika makambi. Vile vile elimu ya mazingira imeendelea kutolewa kwa vijana wa JKT ili vijana waweze kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazohusu usafi na hifadhi ya mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto za Utekelezaji wa Mipango na Bjeti ya mwaka 2012/2013; changamoto kubwa zinazoikabili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni mbili. Kwanza ni kutokukidhi kwa ukamilifu mahitaji ya kutekeleza mipango yake ya kila mwaka ya kuendeleza Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa. Mahitaji ya mipango ya jeshi letu ni makubwa kama ilivyo kwa majeshi mengine duniani ikilinganishwa na uwezo mdogo wa Serikali.

Athari za hali hiyo ni kuwepo kwa upungufu wa mahitaji muhimu ya kiulinzi, yakiwemo ya ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi, utoaji wa huduma kwa wanajeshi na ulipaji duni wa huduma muhimu za maji, umeme, mafuta na vilainisho. Changamoto hii pia imesababisha Jeshi la Kujenga

Taifa kufupisha muda wa uendeshaji wa mafunzo ya Mujibu wa Sheria kwa vijana waliomaliza kidato cha sita kutoka miezi sita iliyokusudiwa awali na kuwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili ni upatikanaji wa fedha za maendeleo. Katika kipindi hiki fedha za maendeleo zilitolewa kwa kuchelewa na kwa kiwango pungufu. Kielelezo cha hali hii ni, mapokezi ya fedha hizi kwa mwaka 2012/2013 ambapo hadi sasa mafungu yote matatu ya Wizara yamepokea jumla ya shilingi 135,700,000,000.00 sawa na asilimia 33.2 ya shilingi 408,189,566,000.00 zilizoidhinishwa.

Hali hii imesababisha kulimbikiza madeni ya kimikataba na kuathiri miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo upimaji wa ardhi ya maeneo ya jeshi na kutokamilika kwa zoezi la kulipa fidia ya maeneo yaliyochukuliwa na jeshi. Kwa ujumla changamoto hizi ambazo zimeendelea kwa muda mrefu sasa zimekuwa kikwazo cha utekelezaji wa majukumu ya Ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Mwaka 2013/2014; mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2013/2014 unakusudia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa Jeshi katika kutekeleza majukumu yao kulingana na Dira na Dhima ya Wizara. Vile vile Wizara inakusudia kukamilisha miradi ambayo haijamalizika pamoja na kulipa madeni ya ununuzi wa vifaa. Kwa hivyo, Wizara yangu itakuwa na jukumu la kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupunguza tatizo la wanajeshi kuishi uraiani kwa kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 6064 kukarabati na kuimarisha miradi ya ujenzi inayoendelea.

(ii) Kulipatia Jeshi zana na vifaa vya kijeshi ikiwemo vifaa vya uhandisi wa medani, ndege vita na magari.

(iii) Kukarabati mitambo na miundombinu katika Mashirika ya Mzinga na Nyumbu ili kuimarisha shughuli za viwanda na kuendeleza teknolojia ya masuala ya kijeshi.

- (iv) Kuboresha mawasiliano ya simu ndani ya Jeshi baina ya vikosi na kwenye makambi ya jeshi.
- (v) Kulipa mikopo ya kimkataba ukiwemo wa *NSSF*.
- (vi) Kupima na kulipa fidia ya ardhi katika baadhi ya maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa kwa ajili ya shughuli za kijeshi.
- (vii) Kujenga maghala ya kuhifadhia silaha na zana za kijeshi.
- (viii) Kulipia gharama za matumizi ya huduma za umeme, maji na simu kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu ya kimsingi zikiwemo operesheni za kiulinzi na mafunzo.
- (ix) Kulipia stahili mbalimbali za Maafisa, Askari, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi wa Umma ikiwemo mishahara, posho za chakula kwa ajili ya wanajeshi, matibabu, likizo, maziko na mafunzo.
- (x) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani; napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watu mbalimbali kwa michango waliyoitoa katika kutayarisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu. Nawashukuru Katibu Mkuu Bw. Job D. Masima, Naibu Katibu Mkuu Injiniya Mussa I. Iyombe, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Davis A. Mwamunyange, Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali Samuel A. Ndomba, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Raphael M. Muhuga, Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga, Meja Jenerali Dkt. Charles N. Muzanila na Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumbu, Kanali Anselm Bahati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo (Makao Makuu ya Wizara), Wakuu wa Matawi (NGOME), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Makamanda wa



4 MEI, 2013

Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Jeshi la Anga na Jeshi la Wanamaji, Maafisa, askari na Watumishi wa Umma wanaofanya kazi chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Vile vile namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha Hotuba hii kwa wakati. Mwisho nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kuiongoza Wizara hii. Nawaomba waendeleo kufanya hivyo ili tuweze kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2013/2014. Makadirio ya Mapato. Kwa mwaka 2013/2014 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekadiria kukusanya Mapato kiasi cha Shilingi 68,206,000.00 katika mchanganuo ufuatao:-

(a) Fungu 38 - NGOME .....	Shilingi .....	1,501,000.00
(b) Fungu 39 - JKT .....	Shilingi .....	46,703,000.00
(c) Fungu 57 - WIZARA YA ULINZI .....	Shilingi .....	20,002,000.00
<b>Jumla .....</b>	<b>Shilingi .....</b>	<b>68,206,000.00</b>

Mheshimwa Naibu Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kutekeleza majukumu yake katika Mwaka 2013/2014 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,102,999,529,000.00 ambazo kati yake Shilingi 857,417,502,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 245,582,027,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa Bajeti hiyo kwa kuzingatia Mafungu ya Wizara ni kama ufuatao:-

#### **FUNGU 38 - NGOME**

Matumizi ya Kawaida Sh. 651,015,373,000.00  
Matumizi ya Maendeleo Sh. 10,000,000,000.00

**Jumla ya Makadirio kwa Fungu 38**  
**Sh. 661,015,373,000.00**

4 MEI, 2013

**FUNGU 39 - J K T**

Matumizi ya Kawaida Sh 187,301,634,000.00

Matumizi ya Maendeleo Sh. 6,000,000,000.00

**Jumla ya makadirio kwa Fungu 39**

**Sh. 193,301,634,000.00**

**FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI**

Matumizi ya Kawaida Sh. 19,100,495,000.00

Matumizi ya Maendeleo Sh. 229,582,027,000.00

**Jumla ya Makadirio kwa Fungu 57**

**Sh. 248,682,522,000.00**

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho; hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ([www.modans.go.tz](http://www.modans.go.tz)). Naomba kutoa Hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, kwa Hotuba yako. Hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushukuru sana, Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa ninaomba nimwite Msemaji wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa Niaba ya Kamati anakuja Mheshimiwa Omar Rashid Nundu. (*Makofi*)

**MHE. OMARI R. NUNDU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni na 99(9) na 117(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba *Hansard* ioneshe Taarifa nzima ya Kamati kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu pamoja na amani ya nchi kadhaa za Afrika zenye migogoro kwa kupeleka wanajeshi ili kulinda amani. Aidha, Jeshi letu limeshiriki kutoa huduma mbalimbali katika majanga yaliyolikumba Taifa kama ambavyo Wizara imeeleza, ikiwemo janga la mafuriko, kuporomoka kwa majengo na mengineyo. Kwa upande wake, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kudumisha nidhamu na uzalendo miongoni mwa vijana kwa kuwapatia mafunzo ya kijeshi. Ni imani yetu kwamba, majeshi yetu yataendelea kutekeleza majukumu waliyokabidhiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, yenye mafungu matatu ambayo ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Fungu 57, Jeshi la Kujenga Taifa - Fungu 39, na Ngome - Fungu 38.

Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2013/2014 iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Waziri ilikuwa na maeneo mahususi yafuatayo: Utekelezaji wa Maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ilipojadili bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2012/2013; utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013; Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka 2012/2013, iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa. Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati uliotekelezwa ni pamoja na:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kwamba, Rasimu ya Sera ya Ulinzi wa Taifa imekamiliwa na imewasilishwa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kupata maoni. Aidha, marekebisho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa na Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, yatafuata baada ya Sera ya Ulinzi wa Taifa kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mrejesho wa Serikali ulionyesha kwamba, hatua za awali zimechukuliwa kwa kuongeza idadi ya vijana 5,000 wanaojiunga na Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria kwa muda wa miezi mitatu. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kuwa, muda wa mafunzo hayo uongezwe na kufikia angalau miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala yanayohitaji kufanyiwa kazi zaidi; Kwanza, Utaratibu wa kushughulikia mahitaji ya Wanajeshi ili kuepuka uwepo wa malimbikizo ya madai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba,

Bajeti inayotolewa kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hailingani na mahitaji halisi ya Wizara hiyo. Kwa mfano, wakati Jeshi limeruhusiwa kuajiri wanajeshi wapya, kiwango cha fedha kinachotolewa kama likizo, gharama za huduma za umeme na maji hakikidhi mahitaji. Ni maoni ya Kamati kwamba, ufumbuzi wa changamoto ya bajeti kutokidhi mahitaji utapatikana iwapo Wizara itatengewa fedha kulingana na mahitaji yake.

Pili, Chuo cha Ulinzi wa Taifa ni muhimu na kina mahitaji makubwa. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Chuo hiki kiliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni mbili tu. Hata hivyo, hadi kufikia Machi, 2013 ambayo ni robo tatu ya mwaka, Chuo kilipokea shilingi bilioni 1.3, sawa na asilimia 67 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haikuridhishwa na mtiririko wa utoaji wa fedha za Bajeti ya Chuo hiki na hivyo kuishauri Serikali ijipange kuhudumia Chuo hiki ambacho ni muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Tatu, kuzagaa kwa silaha nchini kunakotokana na Kampuni binafsi za kigeni kutumia vyombo binafsi vya ulinzi; Jeshi la Wananchi wa Tanzania ndilo lenye dhamana ya ulinzi wa eneo la Tanzania mipakani ikiwemo Bahari ya Hindi. Kutokana na kukithiri kwa vitendo vya kiharamia katika eneo la Bahari ya Hindi, Kampuni za kigeni zikiwemo meli za mizigo na zile zinazofanya shughuli za utafiti wa mafuta na gesi katika eneo hilo, zina utaratibu wa kutumia kampuni za ulinzi za kigeni ambazo zimeruhusiwa kutumia silaha katika kutekeleza jukumu hilo kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti kuzagaa kwa silaha nchini ambako moja ya chanzo chake ni matumizi ya kampuni binafsi za kigeni za ulinzi, Kamati inasisitiza kwamba, Jeshi la Wananchi wa Tanzania lihusike kusimamia vyombo hivyo binafsi vya ulinzi vya kigeni pale wanapofanya kazi katika maeneo ya Mipaka ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha

wa 2012/2013, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, iliidhinishiwa jumla ya shilingi 678,363,492,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Mafungu yake matatu. Aidha, shilingi 408,186,566,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii, Kamati haikuridhika na Mtiririko wa Fedha za Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na hivyo kushauri kwamba, fedha zilizobaki zipelekwe katika Wizara kabla ya tarehe 30 Juni, 2013, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yake kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi 68,206,000. Aidha, imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,102,999,529,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Kati ya fedha hizo; shilingi 857,417,502,000 zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 245,582,027,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya Kamati kwamba, fedha za bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa zinazoidhinishwa na Bunge zitatolewa kwa wakati ili kuwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kuimarisha hali ya ulinzi na usalama wa nchi, Kamati inatoa maoni na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kazi kubwa ya ulinzi wa mipaka yetu ambayo imeendelea kuwa salama. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika ili kuzuia mambo ambayo ni hatarishi kwa usalama wa nchi yetu, kama vile wahamiaji haramu ambao wamekuwa moja ya chanzo cha kuzagaa kwa silaha nchini na wafugaji toka nchi za jirani wanaosababisha migogoro ya malisho. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti wahamiaji haramu ili kudumisha amani na usalama katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati inakutana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tayari Mwaka wa Fedha wa 20/2 2013 ulikuwa umeshafikia robo ya tatu. Hata hivyo, fedha za maendeleo ambazo zilikuwa zimeshatolewa na Hazina ni shilingi 130,000,000,000, sawa na asilimia 33.4 tu ya bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi 389,186,566,000. Kamati inaiona hali hii ni hatari sana kwani inaonesha wazi kwamba, shughuli za Maendeleo za Wizara hii zitafanyika kwa kiasi kidogo sana. Kamati inaitaka Serikali kuwa na mwelekeo maalumu wa bajeti ikiwa ni pamoja na kuainisha vipaumbele ili shughuli zilizokusudiwa kwenye bajeti zitekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kwamba, kwenye mipaka yetu kuna tatizo la kung'olewa kwa alama za mipaka (*beacons*) na hivyo kusababisha wageni kuvamia maeneo ya mipakani ambayo hayaruhusiwi kwa makazi (*no man's land*). Kamati inatambua kwamba, suala la alama za mipaka haliihusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pekee, bali Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo ina jukumu la upimaji ardhi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa yenye jukumu la kuratibu mahusiano baina ya nchi na nchi. Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, iratibu na kuzielekeza Wizara hizo kuandaa mkakati wa pamoja katika kupata suluhisho la kurudisha alama za mipaka ya nchi. Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ihakikishe kwamba, suala la ujenzi na ukarabati wa barabara za ulinzi mipakani ambalo ni muhimu kwa usalama wa Taifa, linawekewa Mkakati Maalumu wa utekelezaji wake Kitaifa badala ya kuachiwa kwenye ngazi za Halmashauri pekee kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukamilishwaji wa Sera ya Ulinzi wa Taifa ikiwa ni hatua za awali katika kuhuisha Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Kamati ilielezwa kwamba, Rasimu ya Sera hiyo imewasilishwa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kupata maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaiomba Serikali

kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kusimamia mchakato huu muhimu mapema iwezekanavyo, ili kuweka msingi katika kuhuisha Sheria ya Ulinzi wa Taifa ambazo zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa ujenzi wa nyumba 10,000 za makazi ya askari ni hatua muhimu katika kuboresha makazi ya askari nchini. Awamu ya kwanza ya mpango huu itakuwa na ujenzi wa nyumba 6,064 ambazo zimetengewa kiasi cha shilingi bilioni 8.5 katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua za makusudi ilizochukua kuboresha makazi ya askari nchini. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kwamba, mpango wa ujenzi wa nyumba zilizobaki 3,936 pamoja na mgawanyo wa nyumba zote 10,000 kimikoa, pamoja na ile tuliyosikia kwamba baadhi ya mikoa imeshagawiwa nyumba hizo, uwekwe wazi pamoja na hatua zilizofikiwa kutekeleza Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu 2004, Kasma ya 220100 - *Office and General Supplies and Services*, fedha iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ni shilingi milioni 28.4 ikilinganishwa na fedha iliyotengwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ambayo ni shilingi milioni 5.6. Tofauti ya shilingi milioni 22.8 ni kubwa na haina maelezo ya kuridhisha. Kamati inapendekeza Kasma 220100 ibakie na kiasi cha shilingi milioni 5.6 kilichopangiwa katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ongezeko hilo la shilingi milioni 22.8 lipelekwe kwenye Kasma 227500 iliyopangiwa kutumia shilingi milioni mbili na hivyo kuwa na jumla ya shilingi milioni 24.8 kwa ajili ya kugharamia shughuli za upimaji na ramani, kwani maeneo mengi ya Jeshi yamekuwa na migogoro ya mipaka na Wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, Fungu 57 liliidhinishwa kiasi cha fedha shilingi



15,850,052,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013, Fungu hili lilipokea na kutumia shilingi 11,266,465,850.00, sawa na asilimia 71.1 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kamati inaisisitiza Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu 38 - Ngome:

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuendelea kujenga na kuimarisha maghala nchini, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Pia tunawashukuru wafadhili ambao wanashirikiana nasi katika hili. Hata hivyo, Kamati haikuridhika na kasi ya utoaji fedha kwa ajili ya utekelezaji wa jukumu hilo kwani hadi kufikia Machi, 2013 ambayo ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha, ni asilimia 30 tu ya bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa imetolewa. Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali itoe fedha zilizobaki kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 kwa wakati, halikadhalika Fedha za Mwaka 2013/2014 kwa ajili ya utekelezaji wa jukumu hilo muhimu pia zitolewe zote mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kinacholipwa kwa ajili ya posho ya chakula ni shilingi 7,500 kwa siku kwa askari mmoja. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Kasma hii ilitengewa shilingi 121,634,328,209. Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Kasma hii ilitengewa shilingi 121,664,031,000 na Mwaka 2013/2014 Kasma imetengewa kiasi hicho hicho cha shilingi 121,664,031,000. Pamoja na kwamba, Jeshi liliruhusiwa kuajiri askari wapya, hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya chakula kwa askari hao wapya kwa miaka mitatu ya fedha mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa, stahili za posho ya chakula kwa askari zinashughulikiwa kwa wakati hasa kwa hao Wanajeshi wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, kiasi cha fedha kilichotengwa katika kasma 229933 kwa ajili ya kuwasafirisha Wanajeshi wanaotegemewa

kustaafu mwaka 2013/2014 ni shilingi bilioni 4.6. Kwa kuwa wastaafu hawa wameitumikia nchi hii kwa uaminifu, kujituma na upendo mkubwa na wanatazamiwa kuendelea kuwa na uaminifu kwa nchi yao hata baada ya kustaafu, Kamati inaitaka Serikali itoe fedha za kuwezesha wanajeshi wote wanaotarajiwa kustaafu katika mwaka 2013/2014 kuwarejesha makwao mara watakapostaafu pamoja na mizigo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kurejesha Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wanaohitimu kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Kamati inawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliojitolea kupata mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, nawapongeza sana wale Wabunge 22 waliohimili mchakamchaka kule wakarudi salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kuwa yenye tija, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Serikali iandae Mafunzo Maalumu ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Watu Maalum kama vile Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Wahariri wa Vyombo vya Habari na wengineo ili kujenga dhana ya uzalendo kwa makundi haya muhimu yenye ushawishi mkubwa kwa jamii.

(b) Serikali iongeze muda wa utekelezaji wa mafunzo hayo kuwa angalau miezi sita.

(c) Serikali iridhie pendekezo la Kamati kuwa, kuhitimu Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa iwe ni mojawapo ya kigezo muhimu ili katika kujiunga na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kama vile Jeshi la Wananchi, Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji, Uhamiaji na Usalama wa Taifa. Kamati inaamini kwamba, Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yatarejesha uzalendo ambao kwa kiasi kikubwa umepungua miongoni mwa vijana sambamba na kumomonyoka kwa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), lilianzishwa ili kuzalisha mali kibiashara kwa Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1974. Moja ya majukumu ya Shirika hili ni ulinzi kwa kutumia Kampuni ya *SUMA Guard Ltd.* Ili kuwezesha Shirika hili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Serikali ichukue hatua za makusudi kuliwezesha Shirika hili liweze kuzalisha kwa faida na hivyo kuweza kutoa gawio kwa Jeshi la Kujenga Taifa katika kila mwaka wa fedha. Hatua hii ni muhimu katika kupunguza utegemezi wa JKT kwa Serikali.

(b) Serikali itoe mwongozo kwa mashirika yote ya ulinzi binafsi, kuwatumia vijana waliopata mafunzo ya JKT, ambao wanao ujuzi wa kutosha katika masuala ya ulinzi na matumizi ya silaha.

(c) Serikali itumie Shirika la *SUMA Guard Ltd.* kufanya ulinzi wa mabenki na baadhi ya makazi ya Viongozi ili kutoa nafasi kwa Jeshi la Polisi kushughulikia majukumu mengine ya kijeshi tofauti na ilivyo kwa sasa, ambapo askari wengi wa Jeshi la Polisi wanatumika katika ulinzi wa mabenki na nyumba za viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Majeshi ya Tanzania ikiwemo Jeshi la Kujenga Taifa, yanasifika kwa kutengeneza samani nzuri na zenye ubora kwa matumizi ya ofisi na nyumbani. Kamati inaishauri Serikali kuandaa Sera Maalum ya kuelekeza Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali na Halmashauri, kununua samani za maofisini na nyumba za watumishi na viongozi wanaostahili, kutoka majeshi yetu ikiwemo Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, kwa ushirikiano mkubwa alioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na

Matumizi ya Wizara hii. Vilevile, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake zote, kwa ushirikiano walioipatia Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2013/2014. Uzoefu wao katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Ulinzi na Usalama umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah – Mwenyekiti, Mheshimiwa Dokta Muhammed Seif Khatib – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Athumani Ngwilizi, Mheshimiwa Kapteni John Zefania Chiligati, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Injinia Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mheshimiwa David Mciwa Mallole, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mheshimiwa Dokta Augustino Lyatonga Mrema na Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge na kwa kipekee namshukuru Ndugu Peter Magati, Katibu wa Kamati hii, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa, Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, ili ulinzi wetu uimarike na shughuli za uchumi kwenye Majeshi yetu ziendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, napenda kuchukua fursa hii kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JW) ni Jeshi la Ulinzi na kwa maana hiyo, lengo lake kuu ni kulinda usalama wa mipaka ya nchi yetu dhidi ya uvamizi kutoka nje. Hii ina maana kwamba, Jeshi letu siyo jeshi la uchokozi au la mashambulizi ingawa katika kujilinda linaweza kuvuka mipaka yetu ili kuzuia uvamizi dhidi ya nchi yetu. Katika jitihada za kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya uvamizi, Jeshi letu linafanya kazi kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Jeshi letu linashiriki katika operesheni mbalimbali za kulinda amani chini ya Mpango wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Jambo hili ni jema na linaongeza sifa kwa Jeshi letu katika Jumuiya ya Kimataifa. Jambo muhimu ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia ni kuhusu maslahi ya kiuchumi na kiusalama ambayo Taifa litapata kwa kushiriki operesheni mbalimbali za kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Wizara hii, Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Serikali ilikiri kwamba, hali ya usalama katika mpaka wa Tanzania na Malawi siyo shwari kutokana na mgogoro wa mpaka katika Ziwa Nyasa. Taarifa hiyo, iliwatia hofu Watanzania hasa pale Serikali iliposema kuwa “tuko tayari kwa lolote”; maneno yaliyoashiria vita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kauli ya

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni kwamba, Malawi imejitoa katika mazungumzo ya usuluhishi baina yake na Tanzania juu ya mgogoro huo. Kujitoa huko kunamaanisha kwamba, hali ya usalama katika mpaka wa Ziwa Nyasa bado ina mashaka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni nini msimamo wa Serikali kuhusu suala la mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa Wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani juu ya kuondolewa kwa alama za mipaka (*beacons*). Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kurudisha haraka sana alama za mipaka zilizoondolewa ikizingatiwa kwamba, alama hizo ndizo zinazoonesha Mpaka wa Utawala wa Amiri Jeshi Mkuu. Hivyo, kuondolewa kwa alama hizo kunaweza kuwa na lengo la kupunguza eneo la utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizopeleka Wanajeshi katika Mpango wa Kulinda Amani wa Umoja wa Afrika na ule wa Umoja wa Mataifa. Pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutambua umuhimu wa ushirikiano wa kijeshi katika Jumuiya ya Kimataifa katika kulinda amani, bado Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutafakari kwanza maslahi ya Taifa na ya Wanajeshi wenyewe kabla ya kujiunga na operesheni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefikia hatua ya kutoa wazo hili kwa kuwa masuala ya ulinzi na usalama ni masuala nyeti sana na kusipokuwa na mipango madhubuti hasa yenye kuzingatia masilahi ya Taifa, nchi inaweza kuingia katika matatizo makubwa hasa ya kiuchumi kwa kujiingiza katika operesheni za kijeshi zisizo na faida kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeiona barua ya wazi kwa Wananchi na Bunge la Tanzania, iliyoandikwa na Kiongozi wa Kikundi cha Waasi cha M23 cha Congo DRC. Katika barua hiyo, Kiongozi huyo ametishia kwamba, Kikundi cha M23 kisilaumiwe kwa mauaji ya halaiki

yatakayotokea kwa Raia wa Tanzania endapo Serikali itaendelea na mpango wa kupeleka askari wake kujiunga na Mpango wa Umoja wa Mataifa wa kulinda amani nchini Congo DRC.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba, majeshi yetu yako imara na kamwe hayawezi kuacha kutimiza wajibu wao kwa sababu tu ya barua ya vitisho kutoka kwa Kikundi cha Waasi cha *M23*. Pamoja na kutambua uimara na uhodari wa Jeshi letu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu kwa maswali yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa nchi ya Malawi nayo imepeleka vikosi vya jeshi kwenye Mpango wa Umoja wa Mataifa wa kulinda amani Congo – DRC, Serikali inalihakikishiaje Bunge hili kwamba wanajeshi wetu watakuwa salama, ikiwa kuna mvutano kati ya Malawi na Tanzania kuhusu mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa?

(ii) Serikali ina mkakati gani wa kunufaika kiuchumi inapoingia katika operesheni za kijeshi katika Mataifa mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza maswali haya kwa sababu Tanzania ilifanya wema kipindi ilipoingia katika harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Bara la Afrika ili zipate uhuru wao. Kambi Rasmi ya Upinzani inazipongeza nchi kama Afrika ya Kusini, Namibia na Msumbiji kwa kutambua mchango wa jeshi letu katika kupigania uhuru wao na hivyo wameamua kuruhusu Watanzania kuingia katika nchi zao bila masharti ya viza. Kambi Rasmi ya Upinzani inazitaka nchi nyingine vilevile kutambua mchango wa jeshi letu katika operesheni mbalimbali katika nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukitumia fedha nyingi kusaidia Mataifa mengine kiulinzi. Kwa kuwa hatuna sera au mipango ya kunufaika baada ya kusaidia nchi nyingine, tunaendelea kuwa maskini. Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka sera na mipango ya

kuinufaisha nchi hasa kiuchumi endapo majeshi yetu yatakwenda kusaidia kulinda amani katika Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali ya CCM kwamba, isiwachukulie wanajeshi na askari wengine kama watumishi wa kawaida wa kada nyingine. Wanajeshi ni silaha iliyo hai na silaha iliyo hai ikiwa na upungufu haiwezi kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wanajeshi wafanye kazi kwa moyo na kwa weledi, ni lazima maslahi yao yaboreshwe na yatolewe kwa wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwapa mara moja fedha za posho ya chakula (*Ration Allowance*) wanajeshi wote wanaokwenda nje ya nchi kwa operesheni mbalimbali za kijeshi kwa kuwa ni haki yao lakini na fedha zilizoidhinishwa na Bunge ni kwa ajili yao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kwa kipindi chote ambacho askari wetu walikuwa hawapewi fedha hizi zilikuwa zinakwenda wapi na kwa matumizi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazoikabili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni pamoja na migogoro ya ardhi. Mara kadhaa kumekuwepo na utata kati ya mipaka ya maeneo ya jeshi na makazi ya Wananchi, jambo ambalo limezua mgogoro kati ya jeshi na Wananchi. Hata hivyo, tatizo la kutokuwepo kwa mipaka thabiti au taarifa za wazi kwa Wananchi kuhusu maeneo ya jeshi, limesababisha Wananchi kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba, endapo kungekuwa na mipaka thabiti inayotenganisha ardhi ya Jeshi na makazi ya Wananchi, migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na Wananchi ingeweza kuepokwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa bajeti wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, baadhi



ya malengo ya matumizi ya fedha zinazoombwa na Wizara hii ni pamoja na kulipa mikopo ya *NSSF*; kugharamia upimaji wa ardhi; na kulipa fidia ya ardhi katika maeneo yaliyochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili mambo matatu kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Serikali ilikopa fedha nyingi katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *PSPF* kwa ajili kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma, Nyumba za Polisi, Nyumba za Usalama wa Taifa, Bodi ya Mikopo, ujenzi wa Ukumbi wa Bunge na kadhalika; na kwa kuwa Mfuko wa *PSPF* sasa unaelekea kufilisika kutokana na tabia ya Serikali kutolipa madeni, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni kiasi gani cha fedha Serikali itakachotoa kulipa mkopo wa *NSSF* na itamalizia lini kulipa deni hilo ili kuinusuru *NSSF* isije ikafilisiwa na Serikali kama ilivyotokea kwa *PSPF*?

(ii) Ni maeneo yapi yaliyochukuliwa na Jeshi ambayo fidia inatakiwa kulipwa?

(iii) Ni lini Serikali itaweka mipaka thabiti katika maeneo ya Jeshi na kuitangaza mipaka hiyo Wananchi waifahamu ili kuepusha migogoro inayoweza kutokea baina ya Jeshi na Wananchi kwa kutojua mipaka halisi na hivyo kuleta mwingiliano wa matumizi ya ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, ili kufikia lengo la kuwa na Jeshi la Kisasa, lenye zana bora za kijeshi, lazima bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ioneshe dhamira hiyo kwa kujitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, Serikali haina nia ya kutimiza azma ya kujenga Jeshi la kisasa kwani Bajeti ya Wizara hii huwa haitekelezwi kikamilifu. Kwa mfano, katika bajeti ya 2012/2013, fedha za maendeleo zilizokuwa zimeshatolewa na Hazina hadi mwezi Machi, 2013 katika Fungu 57 ni asilimia

33.4 tu ya fedha zilizokuwa zimeidhinishwa. Kambi Rasmi ya Upinzani haina hakika kama asilimia 66.6 ya fedha za maendeleo zilizobaki zitaweza kutolewa na kutumika kikamilifu kabla ya mwaka mpya wa fedha, yaani tarehe 1 Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutofanya mzaha na bajeti ya maendeleo katika Wizara hii kwani kwa kufanya hivyo inaweka hali ya ulinzi na usalama wa Taifa hili kuwa mashakani. Masuala ya ulinzi na usalama hayasubiri, kama tunataka kuwa na Jeshi la Kisasa inabidi kufanya hivyo sasa. Kwa mfano, tukivamiwa leo, lazima tupambane leo, hatuwezi kusema tusingi mwaka kesho ili tuwe na Jeshi la Kisasa ndiyo tujilinde. Hivyo bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni lazima itekelezwe yote na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa randama ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa miaka mitatu mfululizo bajeti ya posho ya chakula kwa Wanajeshi (*Ration Allowance*), imekuwa ni kiasi kile kile, haiongezeki wala haipungui. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini hali hiyo inatokea ikizingatiwa kwamba kuna Wanajeshi wanaostahili kulipwa posho hiyo wanaongezeka na wengine kupungua kwa maana ya kustaafu au kufariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa muda mrefu imekuwa ikipigania maslahi ya Wanajeshi wetu ili yaboreshwe na yaendane na gharama halisi za maisha. Aidha, tumekuwa tukipigania mafao ya Wanajeshi wastaafu ili waishi maisha bora baada ya kazi kutokana na utumishi wao uliotukuka kwa Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani imeshtuka sana baada ya kuona Randama ya Fungu 38 (Ngome), katika fedha za kuwasafirisha Wanajeshi wastaafu ni shilingi bilioni 4.6 tu zilizotengwa tofauti na mahitaji halisi ya shilingi bilioni 10.02. Hii ina maana kwamba, karibu asilimia 60 ya Wanajeshi wanaotegemewa kustaafu mwaka 2013/2014 watahindwa kwenda makwao kutokana na ukosefu wa fedha za kuwasafirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni fedheha kubwa kwa Serikali hii ya CCM kushindwa kuwapa Wanajeshi hawa wastaafu ambao waliweka maisha yao rehani kwa miaka mingi kuilinda nchi yetu na Serikali hii ya CCM na sasa Serikali hii ya CCM haioni tena thamani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi sasa wameshazoea tabia ya Serikali hii ya CCM kuwahadaa na kuwapuuza wastaafu. Ilifanya hivyo kwa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya zamani, imefanya hivyo kwa kubeza hoja ya Kambi ya Upinzani ya kuwalipa wazee wote pensheni walau ya shilingi 20,000 kila mwezi kwa kulumikia Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaonya Serikali kwamba, isije ikathubutu kuwatelekeza Wanajeshi wastaafu kama ilivyofanya kwa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kuwa itakuwa inajenga mazingira ya Jeshi kutokuwa na imani na Serikali, jambo ambalo matokeo yake siyo mazuri kwa ulinzi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na milipuko katika ghala za silaha iliyotokea katika Kambi za Jeshi za Mbagala na Gongo la Mboto, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipiga kelele sana na kuitaka Serikali kutofanya mzaha na masuala ya usalama katika Kambi za Jeshi kwa kisingizio kwamba, fedha hazitoshi. Aidha, tuliikumbusha Serikali kwamba ni muhimu kujiweka tayari kukabiliana na maafa mara tu yatokeapo kwa kuwa maafa na ajali hutokea ghafla bila taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada nyingi za Kambi Rasmi ya Upinzani kusesitiza bajeti ya Wizara hii kutekelezwa kwa ukamilifu, bado Serikali hii ya CCM imeendelea kupuuza azma nzuri ya Kambi ya Upinzani Bungeni na badala yake imeendelea kutenga fedha kidogo ya ujenzi na ukarabati wa ghala za silaha kana kwamba, haikujifunza kitu wakati wa ajali ya mlipuko wa ghala za silaha ilipotokea ambapo watu walipoteza maisha na mali zao kuharibiwa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, kwa sababu

fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ghala za silaha mwaka jana (2012/2013), zilikuwa ni shilingi bilioni 14, lakini fedha zilizotolewa na Hazina hadi mwezi Machi, 2013 ni shilingi bilioni nne, sawa na asilimia 28 tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, licha ya Amiri Jeshi Mkuu kuahidi kwamba, atahakikisha kuwa ujenzi wa maghala ya silaha utafanyika haraka kwa kuwa analichukulia suala hilo kwa uzito mkubwa. Licha ya bajeti ya ujenzi wa maghala ya silaha mwaka jana kutotekelezwa ipasavyo, mwaka huu wa fedha Wizara imetengewa shilingi bilioni tano tu ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni tisa, sawa anguko la asilimia 65, ukilinganisha na mwaka jana. Hata hivyo, haijulikani kama hii shilingi bilioni tano inayoombwa katika mwaka huu wa fedha itatolewa yote na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa fedha yote iliyobaki (shilingi bilioni kumi) katika bajeti ya 2012/2013 ili kukamilisha ujenzi na ukarabati wa maghala ya silaha kabla ya mwaka mpya wa fedha kuanza. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa fedha yote shilingi bilioni tano inayoombwa katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 mara moja mwaka mpya wa fedha utakapoanza ili ujenzi na ukarabati wa maghala ya silaha umalizike. Serikali ijenge utamaduni wa kuzuia maafa mapema na siyo kusubiri maafa yatokee ndipo fedha zitolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kuikumbusha Serikali kwamba, Jeshi ni miongoni mwa maeneo yanayobadilika mara kwa mara kiteknolojia kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani. Kwa hiyo, ni jambo muhimu kuwekeza sana katika taaluma za kijeshi kwa kuwasomesha Wanajeshi sambamba na kununua zana za kijeshi za kisasa ili kuweza kwenda sawia na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika medani za kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu, Serikali hii ya CCM imekuwa haitoi kipaumbele katika kuendeleza taaluma za Wanajeshi, sambamba na kutunza vifaa vya Jeshi

vilivyoligharimu Taifa fedha nyingi. Napenda kutoa mifano ya baadhi ya vikosi ambavyo havitendewi haki kwa maana ya kutumika chini ya kiwango, kutowekeza katika taaluma husika na utunzaji duni wa vifaa ya kikosi.

Kikosi cha Wanamaji (*Navy*) kinatumika chini ya kiwango, licha ya kikosi hiki kuwa na wahandisi wa usafiri majini wallobobea, Serikali hii ya CCM imekuwa ikitoa zabuni za kutengeneza vivuko kwa wakandarasi wengine kwa gharama kubwa wakati Wanajeshi wenye taaluma hiyo wapo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa zabuni za kutengeza vivuko kwa kikosi cha wanamaji kwa kuwa wana taaluma hiyo na pia kwa kufanya hivyo wanapata nafasi ya kufanyia mazoezi taaluma zao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa zabuni za ujenzi wa barabara na madaraja maeneo ya mipakani kwa kuwa Jeshi lina wataalamu wa kutosha na ni vizuri zaidi kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kikosi cha Anga (*Airwing*), kina marubani mahiri, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri utoaji wa mafuta kwa ajili ya mazoezi ya ndege vita upewe kipaumbele. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka kipaumbele cha kutunza ndege vita kwa kujenga viota vya kuhifadhi ndege zetu za kivita. Lengo la kufanya hivi ni kuziweka ndege zetu katika utayari wa kazi na siyo kuziweka kwa ajili ya maonesho tu kipindi cha Sherehe za Kitafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza taaluma za kikosi cha wana anga, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasomesha marubani wengi zaidi ili kuongeza ufanisi katika kikosi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo vijana wengi wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kujitolea na kupata mafunzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kutumia silaha za moto na mbinu mbalimbali za kijeshi. Vijana hawa wamalizapo mafunzo hurudi majumbani mwao, kwa

kuwa hawapati ajira ya moja kwa moja Jeshini. Kukaa mtaani bila kazi husababisha vijana hawa kujihusisha na vitendo vya kihalifu; na kwa kuwa wana mafunzo ya kijeshi, hali huwa mbaya zaidi kwa upande wa raia kwani huwa ni vigumu kupambana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nia ya vijana hawa wanapojunga na JKT huwa ni nzuri na mategemeo yao ni kupata ajira katika taasisi mbalimbali za kijeshi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana hawa pindi inapotangaza nafasi za kazi katika Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa lenyewe. Katika kuajiri katika kada hizi, aliyepitia JKT awe na sifa ya ziada ya kuajiriwa ili kutoa motisha kwa vijana wengi kujiunga na JKT na kupata mafunzo mbalimbali ikiwemo nidhamu na uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni vigumu vijana wote waliopata mafunzo ya JKT kupata ajira ya moja kwa moja katika Jeshi hilo au katika Taasisi nyingine za Kijeshi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya utaratibu ili vijana wanaojunga na JKT wapate pia mafunzo ya ufundi chini ya *VETA*. Baada ya kuhitimu vyeti vyao vitambulike kwamba wamepata mafunzo ya *VETA* ili waweze kuvitumia kutafuta ajira katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba, endapo Jeshi la Kujenga Taifa litatumika vizuri na kwa maana ya kujenga Taifa kweli kweli, linaweza kuleta mageuzi makubwa katika uchumi wa nchi yetu. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga maeneo maalumu ya uzalishaji kwa JKT ambayo yanaweza kutumika kwa Kilimo na Ufugaji ili kulisaidia Taifa kujikimu kwa chakula. Aidha, maeneo ya uzalishaji kama vile Ranchi za Taifa ambazo kwa sasa uzalishaji wake unapungua, zinaweza kuwekwa chini ya uungalizi wa JKT ili kufufua uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, Jeshi la Kujenga Taifa linaweza kusaidia kuleta mageuzi ya uchumi (*economic transformation*) katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitoa pendekezo kwamba, kwa kuwa JKT inashughulika pia na utunzaji wa mazingira, basi utunzaji huo uwe ni wa nchi nzima siyo tu katika Makambi ya Jeshi kama ilivyo sasa. Pendekezo hilo lilisomeka hivi:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pendekezo kwa Jeshi la Kujenga Taifa kuendesha OPERESHENI MAALUMU YA KUPANDA MITI NCHI NZIMA kwa kushirikiana na Wananchi. Operesheni hii iendeshe kwa utaratibu ule ule kwa watakaojunga na JKT kufanya mafunzo ya vitendo wakishirikiana na Wananchi katika kutunza mazingira."*

*"Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, Taifa hili litaepushwa na unyemelezi wa jangwa na athari za tabia nchi zinazotokana na uharibifu wa mazingira. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka mabadiliko katika Jeshi la Kujenga Taifa ili kazi zake ziwe ni za Kujenga Taifa kweli na siyo kujenga na kuendeleza Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kama ilivyo sasa."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama ushauri huu umechukuliwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji au umetupwa. Aidha, kama ushauri huu umechukuliwa ni lini utaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kawaida ya Serikali hii ya CCM kuhitimisha hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kutoa majibu mepesi ya kubeza, lakini ukweli unabaki palepale. Hata hivyo, safari hii chukueni ushauri huu kimyakimya na kuufanyia kazi kwa masilahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inayoongozwa na CHADEMA, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Natse, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye *Gallery* ya Spika tuna ugeni na ningeomba kumtambulisha Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi - Jenerali Davis Mwamunyange, ambaye ameambatana na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi - Luteni Jenerali Samwel Ndomba. Tunawakaribisheni sana hapa Bungeni, tunawashukuruni sana kwa kazi nzuri ya kulinda Taifa letu na tunawatakia kila la kheri katika kazi zenu. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na uchangiaji. Naomba nimwite mchangiaji wetu wa kwanza, tunaendelea na dakika kumi kumi zetu, mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ajiandae.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Wizara nyeti sana, muhimu sana kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa letu kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amezungumza na Mwenyekiti wa Kamati na Waziri Kivuli alivyozungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maeneo matatu tu ya kuchangia; la kwanza ni Jeshi la Kujenga Taifa. Mwaka 1994 *IMF* na *World Bank* walikuja hapa wakatuambia kama hamhitaji Jeshi la Kujenga Taifa futeni na sisi sijui tuliingiwa na mdudu gani. Nasema sisi kwa sababu ya kuchukua *responsibility* ya kiuongozi kwa wote, maana wengine hatumo tulikuwa shule, ninyi sijui mliingia mdudu gani mkasitisha Jeshi la Kujenga Taifa. Madhara yake ni nini? Madhara yake ni kwamba, tumejenga Taifa la watu goigoi na kuna *means* kwamba tunaenda Jeshi la Kujenga Taifa kujenga uzalendo, hatujengi uzalendo jeshini hata kidogo, kwa sababu ujenzi wa uzalendo ni mchakato kuanzia kwenye familia mpaka kwenye majukumu ya kikazi ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshini tunaenda kujenga utii, uaminifu na uhodari. Sasa hivi jamii ya Watanzania utii sifuri, uaminifu una mashaka makubwa, uhodari hakuna na ndiyo maana tumekuwa ni Taifa ambalo tunajiingalia kwa



mabaya zaidi kuliko kwa mema ambayo nchi hii inafanya. Nilipokuwa Kambini Mgambo pale Tanga, katika kundi la vijana 1400 waliokuwa wameingia Jeshini wakati tunaanza na sisi, 300 waliumwa wakaondoka Jeshini kwa sababu ya aina ya Taifa ambalo tunalitengeneza, Taifa la watu goigoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusirejee makosa tuliyoyafanya mwaka 1994 ya kusitisha Jeshi la Kujenga Taifa, tuliimarisha zaidi na wale wote ambao hawakupita wajengewe mazingira ya kupita Jeshi la kujenga Taifa. Tuweke utaratibu watumishi wote wa Umma; Walimu, Madaktari watu walioko kwenye Mashirika ya Umma, wajengewe utaratibu hata kama utakuwa ni wa miezi miwili, waende Jeshini. *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani hapa nilipotoka Jeshini akawa ananitania anasema Jeshi gani la wiki tatu! Wabunge waliokwenda Jeshini walitaka kutuma ujumbe kwa vijana wenzao, *a strong massage* kwamba, unaweza ukawa ni Mbunge, Mheshimiwa unakaa kwenye viti vyekundu, lakini ukaweza kwenda kujitoa kwa ajili ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana wiki tatu ni chache sana, lakini ule ujumbe ambao umekwenda kwa vijana, *inspiration* ambayo imekwenda kwa vijana, ninaamini vijana wengi sana miaka inayofuata wataenda jeshini. Kwa hiyo, ninachokiomba ni kwamba, tuangalie namna ambayo tutaweza kurekebisha na Kambi ya Upinzani Bungeni imesema kwenye hotuba yake, vijana ambao wanatoka jeshini watoke na stadi za maisha wasitoke tu na ujuzi wa ulinzi au kulima na kadhalika. Watoke na stadi za maisha, kwa maana hiyo kila Kambi ya JKT tuigeuze iwe ni Kambi ya JKT na iwe pia ni Chuo cha Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuunganishe nguvu za VETA, SUMA JKT na Jeshi la Kujenga Taifa ili kijana anayetoka pale kama ni *Mechanical* atoke na *u-mechanical*, kama ni ufundi uashi atoke na ufundi uashi na kadhalika na tusipende katika masuala kama haya ya kujenga nchi kuwa na sababu za bajeti haitoshi. Nimeona hapa kwenye Hotuba kuna sehemu Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, SUMA JKT wakatafute

wawekezaji kwa ajili ya miradi yao mbalimbali; hapana kuna mambo ambayo hatuwezi kuyaruhusu Jeshini, kuna mambo ambayo ni lazima tuchukue *responsibility* sisi kama nchi. Moja, ni hili la kuhakikisha kila Kambi na ningependa mimi kwa kweli kambi ya kwanza na *pilot* kwa mwaka ujao wa fedha iwe kambi ya Mgambo ndiyo kambi niliyotoka. Shaban Robert anasema titi la mama tamu au siyo eeh, ndiyo Kambi niliyokwenda tuanze na Kambi ya Mgambo. Kambi ya Mgambo ina ardhi kubwa, inalima mbegu kwa ajili ya Wananchi wetu na kadhalika, tuanzie kule tuwafundishe vijana wetu watoke na ujuzi, tusiwatoe tu na mafunzo ya kijeshi. La pili, titi la mama tamu, halafu Mheshimiwa Naibu Spika naomba umhamishe huyu ananisumbua katika kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine linasemwa lakini halijasemwa vizuri; tunaajiri watu Polisi, tunaajiri watu Jeshini, tunaajiri watu Uhamiaji, tunaajiri watu Tanapa, tunaajiri watu Bandari, tunaajiri watu kwenye vitu ambavyo vinaendana na ulinzi, tunaenda kuchukua watu mtaani wakati kuna vijana ambao wamepitia Jeshi la Kujenga Taifa wanabaki hawana kazi. Tuache, ajira zozote za maafisa wanyama pori kuanzia sasa, za uhamiaji, za polisi na maeneo mengine yote Bandari, Ulinzi na kadhalika, sharti la kwanza liwe Cheti cha JKT ndiyo. Tuache kwenda kuchukua watu mitaani kwa sababu ni watoto wa wajomba zetu, ni watoto wa shangazi zetu, ni wadogo zetu na kadhalika, tuchukue hawa ili kuwa-*encourage* hawa vijana ambao wameenda Jeshi la Kujenga Taifa na kuna sababu nyingine inasema kwamba, wanaojitolea wengi ni darasa la saba. Nini kazi ya Serikali si muwajenge hawa kama mnataka wafike *form four* si muwape *opportunity* wafike *form four*? Kwa nini muwanyime fursa za ajira kwa sababu tu hawakupata fursa ya kusoma huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Kamati imelieleza, Kambi ya Upinzani imelieleza, lakini Mheshimiwa Waziri hakulisema, nalo ni DRC. Sisi ndiyo nchi ambayo ina mpaka mrefu zaidi na DRC kuliko nchi nyingine yoyote ile zaidi ya kilomita 1100 Ziwa Tanganyika. Vurugu zikitokea Mashariki ya

DRC, tunaoathirika zaidi ni sisi kwa sababu wakimbizi hawaendi *Central African Republic* kwa sababu kuna fujo, hawaendi Rwanda kwa sababu wamegombana na Wanyarwanda, hawaendi Burundi hali ni tete wanakuja Tanzania tunagombana nao *resources* hizo hizo mazingira yanaharibika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa M23 wameandika barua lakini ni lazima tuwaoneshe kwamba sisi ni Taifa huru lililompiga Idd Amini, tusiruhusu kikundi chochote kile kwa lolote lile, kiitisha Tanzania na ni lazima hawa wawe ni somo kwa hawa wengine ambao wanatuchokonoa. Tuna sababu za majukumu ya Kimataifa kule DRC, tuna sababu za majukumu ya Usalama wa nchi yetu kule DRC, tuna sababu za kiuchumi kule DRC, wala mtu asitutetereshe. Hizi propaganda ambazo wamezianza, tusikubaliane nao, ni lazima tuhakikishe DRC inakuwa *stable*, tumechelewa mno. Walimuua Lumumba tukakaa kimya, Mobutu amekaa amepora nchi ile kwa miaka tumekaa kimya, hatuwezi kukaa kimya tena, lazima tujipange vizuri tuhakikishe tunakwenda kuishinda vita ile, kama ni vita, kama ni kulinda amani, ni lazima tujipange vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa Jeshi, tusingependa kusikia tena kashfa mbalimbali Jeshini. Tungependa Jeshi liwe safi. Yale mambo ya zamani ya MEREMETA na kadhalika, yasirudie tena Jeshini. Hapa juzi juzi, SUMA JKT walikuwa na tatizo la matrekta, yasirudie tena haya, lazima Jeshi liwe safi kuliko chochote kile ili libakie kuwa tegemeo letu. Tusiruhusu tena na Mkuu wa Majeshi yuko hapa na Mnadhimu Mkuu yupo hapa, hii ndiyo *message* ambayo ni lazima muwe nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, *pension* kwa Wanajeshi; Wanajeshi wanalalamika sana pale Kawe kwa dada yangu Halima, ndiyo Wanajeshi wengi wanakaa pale. Kamati imeelezea hapa vizuri sana taarifa ambayo ameisoma Mheshimiwa Nundu, kuna tatizo kubwa sana la mafao ya Wanajeshi. Tusiruhusu Wanajeshi wetu kunung' unika ndiyo hivi vi-M23 vitakuja na kusema kwamba Wanajeshi

wenyewe hawalipwi vizuri na kadhalika na mengine hatuwezi kuyasema hapa kwa sababu wanatusikia, wanafuatilia wajue leo tunasema nini. Cha msingi ni kwamba, tusiruhusu Wanajeshi kunun'gunika na vitu vidogo vidogo vya *pension* na kadhalika, tuwalipe Wanajeshi wetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Msabaha.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nashukuru kupata nafasi hii. Kipindi kilichopita natumai katika sehemu hii niliweza kuzungumza kuhusu maeneo ambayo Wanajeshi wamechukua sehemu ya Cheju, Kijiji cha Ujamaa Zanzibar na nilisema kwamba, Waziri husika tuna wajibu wa kuonana na Wananchi kuweza kuzungumzia suala hili ili upatikane ufumbuzi, lakini hadi leo tunakutana tena bado hatujaweza kuonana na Wananchi kupata ufumbuzi katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waziri husika hivi sasa tuna wajibu kikao hiki kuzungumza lini tutakwenda Cheju kuonana na Wananchi wa Cheju kuhusu maeneo ambayo mmeweka sehemu zenu, mmehodhi, mmechukua maeneo hayo. Pia katika kitabu chako hiki, ulizungumzia sana kuhusu mambo ya zana kwamba utanunua zana.

Mimi nahisi, ukinunua nguo inahitaji kutunzwa kwa kufanyiwa usafi. Nguo ni lazima ifuliwe na ndiyo itadumu na siyo kwamba kila siku utakuwa unanunua nguo mpya. Sasa tuna wajibu katika Jeshi letu kuangalia zana tulizonazo ziko katika hali gani. Sitaki kuzungumzia sana hili, lakini nikisema hivyo nafikiri Waziri husika ananielewa. Tuna wajibu wa kuangalia zana na vifaa tulivyo navyo viko katika hali gani, kabla hatujapanga kununua vifaa vingine vipya. Hapo

namwachia Mheshimiwa Waziri.

Tatu, uhamisho; Wanajeshi wengi wanalalamika kwamba, wamekuwa hawapati haki zao pale wanapohamishwa. Wengine wanashushwa vyeo kutoka *sergeant* kuwa *corporal* kwa sababu ya kukaidi kwenda walikohamishiwa, ama kwa kutokuwa nauli au kutokana na umbali wa anakotakiwa kuhamia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, suala hili linatakiwa kurekebishwa ili wanapopanga kumhamisha askari, wahakikishe mipango yake ya uhamisho inakamilishwa kabla ili kuweza kufanikisha safari yake kwenda kule alikohamishiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu JKT. Mimi ni mmoja wa waliokwenda kuhudhuria mafunzo JKT na nilikuwa Kigoma kule Burombola. Pamoja umri wangu nilionao, lakini watoto wanajua huyu mzee yukoje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda kule tukaona mengi na tutazungumza yale ambayo yanahusika. Kwanza, kuna tatizo la maji. Maji ni kitu muhimu sana na kwa bahati nzuri Ziwa Tanganyika liko karibu sana. Hata hivyo, nashangaa ni kwa nini mahali kama pale pawe na tatizo la maji pasipo kutafutiwa ufumbuzi ili kuwawezesha vijana wa eneo lile kupata maji! Jambo linalonishangaza sana, pale tuliacha Vijana wasiopungua 1500 ambao wanahitaji mambo mengi na kubwa zaidi likiwa ni maji. Maji ni uhai wa mtu, hivyo naomba suala hili lilikebishwe.

Pia, niongelee matibabu katika kambi zetu kwa ujumla. Nina wajibu wa kuzungumza mambo niliyoyaona pale *physically*. Kwa kweli hali ilivyo, hairidhishi. Sehemu yenye vijana 1500 na vijana hawa walipojaza fomu zao shuleni waliambiwa kwamba taratibu za matibabu zitafanywa huko, lakini leo mtoto anakwenda pale anakosa matibabu kwa sababu hana fedha ya kununua dawa! Hii ni hatari kubwa sana, ilibidi baadhi yetu sisi tuwe *ATM* ili kuwasaidia vijana. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Acha bwana!

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Huo ndiyo ukweli ulivyo. Sasa hii ni hatari. Ukiuliza unaambiwa dawa zinakuja lakini hazijafika, hii ni hatari kwa watoto wetu. Tunaweza kuwakosa watoto wetu katika hali kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kutoka Kigoma kwenda Kambini ni mbaya. Wakati mwingine vijana wale inabidi waletwe mjini kwa matibabu, kwa sababu pale kambini ujuzi wa hospitali ni mdogo; hivyo, inabidi watoto wapelekwe mjini kwenye hospitali kubwa kwa ajili ya matibabu zaidi. Tuna wajibu wa kurekebisha barabara, angalau ziwekewe kifusi ili gari likipita kusiwe na matatizo. Zikirekebisha zitarahisisha usafiri, kwa sababu kama kuna mgonjwa ameugua ghafla inabidi awahishwe hospitali, hivyo barabara zikarabatiwe angalau hata kwa kumwagiwa kifusi.

Suala lingine ni vyoo. Vyoo havitoshi na vilivyopo ni vibovu na vinaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko. Hili ni suala muhimu na wala hatuhitaji kupata msaada nje. Ninyi wenyewe mnatakiwa kujipanga na kuweza kurekebisha hivyo vyoo, kwani kukarabati choo hakuhitaji msaada kutoka nje ya nchi. Kwa kweli haihitajiki bajeti kubwa ya Serikali kutengeneza vyoo. Mambo kama haya ni muhimu kurekebisha, kwani kwenye Kambi za Jeshi wanapelekwa watoto ambao ni Taifa la kesho, hivyo wanahitaji kukua wakiwa na afya njema. Baada ya muda wao ndiyo watakuwa Wabunge na watakuwa hapa ndani, sisi hatutakuwepo, nadhani ndiyo lengo la kuwaandaa watoto wetu kukua wakiwa na afya nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu na ni lazima lilisitizwe sana ni kuhusu ajira. Imani ya watu wengi na vijana wengi ni kwamba, wakimaliza Mafunzo yao JKT watapata ajira. Ndiyo maana Vijana wako tayari kwa hali yoyote wajiunge na JKT kwa matumaini kwamba wataajiriwa. Tujiulize, je ni kweli Serikali itamudu kuajiri vijana wote? Hiyo siyo kweli!

Tunataka vijana wetu tuwaondolee imani hiyo

kwamba, wakitoka Jeshini watapata ajira wote, bali tuwaandae ili wakimaliza waweze kujajiri wenyewe. Hivyo basi, ni lazima kila Kambi iwe na Chuo cha *VETA* na vijana waandaliwe katika maeneo mbalimbali kama kuwa mafundi umeme, ujenzi, uashi na kadhalika. Kwa mfano, kambi niliyokuwepo mimi, kuna Ziwa Tanganyika, hivyo vijana wakifundishwa uvuvi pia itawasaidia. Kama vijana watafundishwa kuvua wakiwa hapo Kambini wanaweza kusaidia kuongeza kitoweo, kwani watavua samaki na samaki hao watatumiwa na wao wenyewe. Suala hili ni muhimu na litawasaidia sana. Hivyo, Serikali iwajibike kutafuta boti, mashine na vijana wajifunze uvuvi ili wakimaliza mafunzo ya Jeshi na kama hawajaajiriwa, basi vijana wetu waweze kujajiri wenyewe. Wanaweza kuvua Bahari ya Hindi au Ziwani kwani hizo rasilimali zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee kuhusu mawasiliano. Kule hakuna mawasiliano; hivyo, mawasiliano yapelekwe ili likitokea tatizo wazazi waweze kuwasiliana na watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba niunge mkono hoja. Ahante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Kassim Issa. Bado tunaendelea na uchangiaji wa Makamanda wetu. Mheshimiwa Mariam Msabaha, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kasembe.

**MHE. MARIAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Hotuba hii hasa ukizingatia kuwa mimi ni Mwanajeshi wa Akiba. Ujuzi tulikuwa nao lakini pia tulienda kukumbushia. Nawashauri Viongozi wote ambao hawajapitia JKT au ni Wanajeshi wastaafu waende tena wakajifunze kwani siku hizi Jeshi limebadilika.

Nashauri ili mtu awe na sifa ya kuajiriwa na Serikali, basi awe na cheti cha mafunzo ya Jeshi kwani atakuwa kiongozi shupavu. Tunamwona Mheshimiwa Dkt. Harrison

Mwakyembe, aliyepita Kikosi 221, Wizara yake anavyoipeleka puta. Viongozi wote tuliokwenda Burombola tumekomaa, kwa sababu tulikuwa tunapambana na majambazi sugu, kulikuwa hakuna kulala. Kazi ilikuwa kwenda kwenye Mipaka ya Kongo na Ziwa Tanganyika. Naipongeza Serikali yangu na jitihada ziongezwe zaidi katika vikosi vyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi ni askari ambao hawalalamiki, wanastahimili magumu, wametulia sana, ingawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, kwa kweli wanahitaji pongezi. Watu wanaotafuta uchokozi, naomba mjue kwamba, Jeshi lipo imara na lina silaha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakufunzi wa 221 wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kikosi hiki ni kikosi mama na kipo mpakani Kigoma, kinapambana na magaidi, majambazi sugu yanayotoka Kongo, kinazuia uingizwaji wa silaha halamu kutoka Rwanda au Kongo, kinafanya kazi usiku na mchana bila kulala. Jambo la kushangaza, Wanajeshi wanafanya kazi ngumu katika mazingira magumu, nyumba zao zinavuja na hakuna umeme, lakini ni watiifu. Kikosi hicho kinachukua Wakufunzi wengi, lakini miundombinu ni hafifu. Mimi menyewe nilikuwa hapo Jeshini Burombola, nimevumilia hali hiyo ngumu mpaka nilipotoka nilipewa nishani ya utiifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wanajeshi wawe wanafanyiwa *check-up* kwani wanafanya kazi kwa muda mrefu wakiwa wamesimama, hawapati muda wa kupumzika. Hivyo, naomba wawe wanapelekwa mara kwa mara kwenye vipimo vya afya zao, wawe wanapelekwa kufanyiwa *check-up*, ili kuwaepusha na vifo vya ghafla vinavyosababishwa na matatizo ya *pressure*. Naomba jambo hili lizingatiwe, kwani ni muhimu kwa Wanajeshi wetu.

Pia, askari wa kike wanafanya kazi ngumu sana bila kupumzika; naomba wapandishwe vyeo, wapewe zana za kazi ili kuwapa moyo wa kutenda kazi kwa juhudi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee vijana



wetu tunaowapeleka JKT. Naomba niipongeze Serikali kwa kurudisha Mafunzo ya Jeshi kwa Vijana wetu na pia niwapongeze vijana kwa kukubali kujiunga na JKT. Hii itasaidia kuondoa Viongozi goigoi.

Naiomba Serikali ikubali kwamba, isiajiri watumishi ambao hawajaenda kupata mafunzo JKT. Niwaombe pia Viongozi wote waliopo sasa, Wabunge ambao hawajaenda JKT na Wabunge wale walioenda JKT lakini wakatoroka, waende JKT. Kama sheria ilivyopitishwa na Bunge letu Tukufu na kama ikiwezekana iongezwe miezi sita au mwaka, mkirudi hapa mje na spidi gavana.

Suala lingine, hawa *sergeant* tutawapumzisha, mkienda JKT Bunge litatulia kwani hakuna mtu atakayeweza tena kuiibia Serikali, kwani watakuwa wakakamavu. Hakuna kupitisha bajeti mbovu kama mtu atakuwa amepitia JKT. Mwanajeshi yeyeto siyo mwizi na anakuwa mtiifu kwa Serikali yake. Hivyo, naomba Viongozi wote wapite Jeshini ili wawe waaminifu. Hakuna mtu kugombea Ubunge kama hajakipita JKT.

Wabunge waende JKT ili wawe wazalendo na nchi yetu, wawe wakakamavu na baadaye waweze kupambana na Serikali.

Kuhusu vijana wanaojiunga na JKT, wakimaliza masomo yao kuna baadhi wanapata ajira, kuna baadhi wanarudi mitaani bila ajira. Naishauri Serikali yangu, jambo hili liangaliwe kwa makini kwani tunatengeneza majambazi watarajiwa katika Serikali yetu. Ukimaliza Mafunzo ya Jeshi unakuwa umekomaa kwa kila kitu, kwani unakuwa mkakamavu na shupavu, hata ukiamua kupiga ngumi ukuta unapiga tu, ukiamua kwenda kupambana na majambazi Benki unaweza. Sasa kama hawa vijana hujawapa ajira na kwa vile wameshakuwa wakakamavu na wana mbinu za vita, Serikali ijue kwamba hawa ni majambazi watarajiwa.

Naiomba Serikali, askari wanaojiriwa na Jeshi la Magereza basi wawe wamepita JKT. Askari wanaokwenda

kujiunga na Jeshi la polisi pia wawe wamemaliza JKT. Kusipelekwe ndugu na jamaa wanaotoka mitaani. Pia kwa wale ambao watoto wao wamewashinda wasiwakimbize Jeshi la Polisi. Kama mtoto kakushinda mpeleke JKT, akirudi atatulia na atakuwa mzalendo katika nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe wito kwa Viongozi wetu, waweke mikakati ya kuendeleza Jeshi letu na kuliweka katika hali nzuri ya utayari. Tuangalie vifaa vya Jeshi vilivyoharibika vikarabatiwe na Ndege za Jeshi zikarabatiwe pia. Vitu vyote vinavyojulikana na vifaa vya Jeshi viwe tayari wakati wote na muda wowote, ili kama tukio likitokea vifaa vya kazi viwepo kwa wakati; usiviache vitu vile viharibike au kuchakaa.

Kuna Wanajeshi wana ujuzi mbalimbali wa ufundi. Tuwatumie Wanajeshi wetu katika Ujenzi wa miundombinu yetu kama barabara, madaraja, fukwe za bahari na kadhalika. Wale wanaosema Wanajeshi wanakula pesa za bure, naomba wabadili usemi huo kwani wanafanya kazi ngumu sana. Kazi ya Jeshi ni ya kujitoa mhanga kupoteza roho yako. Wanajeshi wanakuwa hawana raha na familia zao kwa ajili ya kulumikwa Taifa.

Wanajeshi wanapostaafu wajengewe nyumba na wapewe pesa za kujikimu wakirudi uraiani ili waweze kuwekeza katika miradi mbalimbali. Wanajeshi wanakaa kambini kwa muda mrefu mpaka wanakosa nguvu ndiyo wanarudi uraiani wakiwa hawana nyumba za kuishi.

Naiomba Serikali iwaangalie Wanajeshi wetu, wawapatie nyumba za kukaa. Utengenezwe utaratibu kama ni kuwakopesha au kama kuna njia yoyote ya kuwawezesha Wanajeshi wetu kupata nyumba ufanyike ili Wanajeshi wetu wapate makazi bora kipindi wanapostaafu.

Pia, Wanajeshi wetu wanapostaafu wapewe kiinua mgongo kwa wakati na wasiwe watu wa kufuatilia mara kwa mara, kwa sababu hawa wapo tayari kwa lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Msabaha. Kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Mariam Kasembe, niwaambie tu kwamba, kwanza Naibu Spika wenu nimepita JKT mwaka mzima. Nimepata maoni mbalimbali wanasema Jenerali Mwamunyange atakapondoka hapa, aondoke na *Platoon* moja angalau. Vile vile nimepata mapendekezo hapa kwamba aondoke na *Platoon* ya kikosi cha akina mama tu! (*Makofi/Kicheko*)

Sasa mapendekezo yaliyoko hapa ni Mheshimiwa Moza Abeid, Conchesta Rwamlaza, Elizabeth Batenga, Waziri Samia Suluhu, Mheshimiwa Waziri Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Waziri Sophia Simba, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Naomi Kaihula, na *Platoon Commander* wao ni Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa mariam Kasembe tuendeleo na uchangiaji!

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia angalau kwa dakika kumi juu ya Wizara yetu tuliyonayo kwa siku hii ya leo.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kushukuru hotuba zote zilizotolewa hapa, zimeelezea mambo ya msingi, nami nasema Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, basi hebu ajaribu kuzingatia kwa sababu yamezungumzwa mambo mengi hasa kwenye ile hotuba ya Kamati, yamezungumzwa mambo mengi ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nachangia hotuba ya Waziri Mkuu, yapo mambo makubwa mawili ambayo niliyazungumza na kwa siku ile nilitarajia kwamba ningeweza kupata majibu, lakini sikuweza kupata majibu. Lakini niseme kwa siku ya leo ninayo furaha kubwa kwa sababu yale niliyokuwa nimeyazungumza yamo ndani ya

hotuba ya Waziri, yapo ndani ya hotuba ya Kamati, hata kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani nayo yamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niyazungumzie hayo mambo mawili. La kwanza, nilizungumza juu ya vijana wetu wanaokwenda JKT. Vijana wanaokwenda JKT kwa hivi sasa ni wengi sana.

Kama alivyozungumza Mheshimiwa Yahaya kwamba vijana wetu wengi wanajitokeza kwenda JKT wakiwa na matumaini makubwa sana ya kuweza kupata ajira. Mimi ni mmojawapo niliyekuwa nimekwenda JKT. *(Makofi)*

Tulipokuwa tunapata tano, tulikuwa tunapata muda wa kuzungumza na vijana wetu. Waliopita JKT watajua maana ya tano ni nini. Kama hujakwenda, sijui. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wetu walikuwa wanatuomba sana tufikishe kilio chao juu ya suala la ajira zinazotokea nje wakati wao wako Jeshini. Nafasi zenyewe ni nafasi za Jeshi, nafasi za Polisi, za Magereza, TANAPA, Bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hili suala, haiteti maana yoyote, tunapeleka vijana 4000, 5000 JKT, halafu wao wako JKT wanajitolea, huku nje tunatoa nafasi za ajira kwa vijana ambao wako Mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana walioko JKT wanapata mafunzo mazuri sana. Vijana wale wameshakuwa mahodari, watiifu kiasi kwamba kama tutaamua Polisi tukawachukua vijana waliotoka JKT, Magereza tukawachukua vijana waliotoka JKT, Jeshi tukawachukua vijana waliotoka JKT, tutaunda Jeshi letu ambalo kwa kweli litakuwa na utii na tutaachana na haya mambo ya malalamiko ambayo tunawalalamikia Polisi kwamba sasa hivi tunaajiri Polisi ambao kwa kweli hawana maadili mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niungane na wote ambao wametoa wazo hili, na ninamwomba Mheshimiwa Waziri, akiona jambo lolote limezungumzwa na watu wengi, ajue kwamba lina msingi ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata Mwenyezi Mungu anasema kuliko na wengi na Mungu yuko huko huko. Ukiona hili jambo linazungumzwa kwa wingi namna hiyo, tunaomba ulitilie baraka, tuachane na suala la kutoa ajira huku nje; ajira zote zitoke ndani ya JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili ambalo nililizungumza ambalo wenzangu wengi wamelizungumza lakini naomba nisisitize, ni hili suala la kuwapa mafunzo ya ufundi vijana wetu ambao wako JKT. Haileti maana yoyote kijana anakaa kule miaka miwili anafanya kazi za kujenga Taifa; miaka miwili ni mingi vijana wale wanafanya kazi nzuri, shughuli za kilimo, ufugaji, lakini baada ya miaka miwili anapomaliza, anarudi tena kijijini hajui hata akaanzie wapi. Lakini kumbe kama tutapeleka haya mafunzo, vijana wetu watakuwa wanaondoka pale wakiwa na angalau na taaluma fulani wanaporudi nyumbani, wanakwenda kujiendeleza na lile ambalo wamejifunza kutoka kule JKT. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba, sisi kwa kuwa ni Wabunge, naamini kama Wizara itaandaa mpango mzuri wa kuanzisha haya mafunzo katika JKT, sisi Wabunge tutakuwa kifua mbele katika kupigania Wizara hii ipewe fedha za kutosha ili suala hili liweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilivyokuwa JKT Bulombora. Hali ya Bulombora ni mbaya sana kwenye huduma muhimu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, tumewaacha vijana wetu wale wa mujibu wa sheria ambao watakaa kule kwa miezi mitatu. Ninakuomba sana tena sana, watakapokuwa wanamaliza mafunzo yao, uende ukawafungie mafunzo yao wewe mwenyewe kule Bulombola, ili uweze kuona fursa ya haya tunayoyazungumza kuhusu Bulombora.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia huruma, inashangaza, ile Kambi haina umeme. Umeme wake ni wa jenerata, lakini kwa mshahara huo huo mdogo wanaopata hawa Askari wetu, inabidi wachangishane wao wenyewe, fedha zao za mfukoni kwa ajili ya kununua mafuta ya jenereta ndipo wapate umeme. Umeme unawashwa kuanzia saa moja na nusu au saa mbili kwa ajili ya kubana matumizi, ikifika saa tano Kambi yote ni giza. Hii ni hatari! Kwa kweli naomba Wizara iwafikirie wale wenzetu waweze kupata umeme wa uhakika ili ile Kambi pamoja na ulinzi ullopo, uweze kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Kambi yenye watu zaidi ya 2000 kwa sababu 1500 ni wale vijana waliokuja kipindi hiki tu, lakini wapo wale wa OP Sensa ambao bado wako pale. Kwa hiyo, Kambi ina zaidi ya vijana 2000, lakini maji hakuna. Jamani, Serikali inashindwa nini kuyatoa maji ambayo yako karibu kwenye Ziwa Tanganyika wakaletewa wale vijana pale Kambini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazingira yaliyopo, vijana wanajitahidi usafi, lakini suala la maji ndilo ambalo linaweza likakamilisha usafi katika maeneo yoyote. Naomba sana, Mheshimiwa Waziri afikirie suala la maji katika Kambi ile, ni ya muhimu mno. Naomba atakapokuwa anajumuisha atuambie atafanya nini kuhusu suala la maji pale pamoja na hilo suala la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwenzangu Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa alizungumzia vilevile suala la matibabu. Pana Zahanati nzuri sana, lakini pamoja na uwingi wa vijana wetu walioko pale, watumishi katika Zahanati ile wako watano tu. Hivi watu watano wanawezaje kuwahudumia watu zaidi ya elfu mbili na kitu? Naomba ufanyike utaratibu haraka, waweze kuongezewa watumishi pale ili waweze kusaidiana kutoa huduma muhimu kwa vijana wetu.

Vilevile pamoja na kuwaongezea watumishi katika Zahanati, naomba vilevile suala la madawa lizingatiwe. Mimi mwenyewe kwa bahati mbaya nilipopata msukosuko kidogo

nililazwa pale. Huduma ni nzuri, lakini suala la madawa walikuwa wanalazimika kufuata dawa Mjini. Kwa hiyo, suala la madawa pale ni muhimu sana. Dawa ziende kwa wakati na hasa ukizingatia ile Kambi iko kule mpakani. Tusiwasahau jamani wenzetu ambao wako pembezoni. Tusije tukajali tu Kambi zilizoko Mijini, lakini wenzetu wanateseka na ndiyo wanaofanya kazi kubwa kule za ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba nizungumzie suala la nyumba za Askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona nyumba zao inatia huruma sana. Nyumba inauliza, nikuuwe saa ngapi? Hizi nyumba zilizo nyingi siyo kwamba imejenga Serikali, wamejenga wenyewe! Sasa kama Askari wanajitolea kujenga nyumba wenyewe, Serikali inashindwa nini kuwa-*support* watu kama hawa ikawajengea nyumba bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakae mbali, wakae mpakani, hata nyumba bora hakuna! Kwa kweli wale wanaokaa kule, kama kungekuwa kuna uwezekano, wangekuwa wanapewa posho zile za kujikimu kwa ajili ya mazingira magumu. Wenzetu wako katika hali ngumu!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa yake Mheshimiwa Waziri nimesikia zimepatikana fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari, naomba awaangalie sana; katika Kambi kama hizo ambazo hazina nyumba hata moja iliyokuwa bora, sikuona nyumba hata moja iliyokuwa bora. Nyumba zote kwa kweli zimejengwa tu ovyo ovyo, hivyo hivyo, lakini wanavumilia, wanakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho, vijana wetu hawa wa *Form Six* tumewapeleka, lakini ninachoomba, kabla ya vijana hawa hawajapeleka Jeshini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Loh! Kengele ya pili!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Niliyekuwa nazungumza ni AKC 4513. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atafuatiwa kwa kifupi sana na Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Waziri Bernard Membe ajjandae.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kusema kwamba nchi yetu bado iko salama. Lakini nataka tu niseme kwamba hivi sasa pamoja na kwamba tunao ushirikiano wa nchi jirani, yaani kama tuko kwenye *East Africa*, tuko kwenye *SADC* na kadhalika, lakini bado wenzetu wanajimarisha sana kiulinzi, pamoja na kwamba tuko pamoja katika ushirikiano. Silaha wanazonunua na bahati nzuri wanazipitisha kwetu hapa, tunazona, ni za kisasa sana kuliko hata tulizonazo.

Sasa tunapata mashaka kwamba kweli katika ushirikiano wetu bado tunaaminiana kuwa tunaishi kama majirani, kama ndugu au vipi? Kwa nini wenzetu wanajitayarisha zaidi kuliko sisi? Sasa haya ni masuala lazima tuyaulize. Kwa maana hiyo, naiomba sana Serikali, hii Bajeti ya maendeleo ambayo inahusu hasa kununua silaha za kisasa kama wanavyofanya wenzetu, ili tuwe tayari, naomba sana hili tulizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna matatizo, Kamati ya Bajeti ipo, tukae kitako pamoja tuone namna gani tunaweza kulitatu tatizo hili. Tusikae tu kwa sababu tuko kwenye ushirikiano, wenzetu wanajitayarisha, sisi bado hatujitayarishi. Hili lazima tulifanyie kazi na wenzetu ambao wanafanya kazi nzuri ya ulinzi, wawe na uhakika kwa sababu Askari siyo kupiga *salute*, Askari ni kuhakikisha anayo zana nzuri ya kufanyia kazi. Kama hakuna zana nzuri, hata akiwa na nidhamu ya kiasi gani, bado haiwezi kumsaidia. Kwa hiyo, hilo lilikuwa la kwanza, ningomba tulifanyie kazi.



Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna Askari wastaafu, kuna Askari wanaohamishwa na kadhalika, kuna *about 36 billion Shillings* hawajapata. Sasa ukiliweka hili deni mwaka huu na mwakani kwa kiwango hicho cha Shilingi bilioni 36 ni kikubwa sana. Naomba sana Wizara ya Fedha ijitahidi sana kupata malipo haya kabla ya Juni, ili lisiendelee hili deni la kwenye *OC* ambalo baadaye litaleta matatizo mbele ya safari, na hasa tukizingatia kwamba hawa ndugu zetu wamestaafu, wengine wanataka kurudi majumbani kwao, tunaendelea kuwakopa, umasikini unazidi kuwaongezekea. Mimi naomba hili lifanyiwe haraka hizi *36 billion Shillings* wanzodaiwa na wastaafu na kadhalika ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, Jeshi la Marekani linanunua dola 35 maji pale Afghanistan, kwa sababu wanayatoa Pakistan, wana-*escort* mpaka yafike pale salama. Baada ya kugundua hilo, kwa kutumia taaluma waliyonayo ndani ya Jeshi na hili ndilo ambalo nataka kusema sana, wameweza kuvumbua *Water Purification System* inayoweza kuwasaidia kupata maji safi na salama kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jeshi, bahati nzuri Jeshi limekamilika kama Serikali, Idara zote ziko zote, kama unavyoziona za Serikali, na Jeshini zipo. Ningeomba sana hizi Idara za Utafiti, hivi vikosi vya kisayansi, vya wataalam wa kisayansi walivyomo ndani ya Jeshi, wapewe zana waimarishwe ili waweze kujitegemea katika masuala mbalimbali na kuuza teknolojia nje. Hii teknolojia ninayokwambia wanaita *4G, Water Purification System*, ni taaluma iliyopatikana ndani ya Jeshi. Baada ya kupatikana imeuzwa kwa Makampuni ya nje kama teknolojia mpya. Kwa hiyo, Jeshi limepata fedha kwa kuuza teknolojia, waliuza lakini vilevile imewasaidia na wao kufanya kazi.

Kwa hiyo, ninachojaribu kukisema ni kwamba ndani ya Jeshi wako wataalam mbalimbali. Hivi vikosi vya kitaalamu viimarishwe ili viweze kutoa taaluma yao kuuza nje. Hizi taaluma nyingi unazoziona hasa katika Jeshi la Marekani, ni taaluma zinazotoka ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye *4G Mobiles, Telephone*, ni taaluma iliyotoka ndani ya Jeshi. Wakishatumia kwa muda mrefu wanawapa watu. Kwa hiyo, wako wataalam ndani ya Jeshi, kama tunawaendeleza vizuri, tuna hakika kabisa, tunaweza kabisa Jeshi letu likafika mahali likasaidia uchumi wa nchi kwa maana ya kutoa taaluma ambayo tunaihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu JKT; niliwahi kwenda Korea, nikamkuta Naibu Waziri mwenzangu akaniambia nakwenda likizo, lakini ninakwenda kazini, kwenye Kambi. Likizo yake anakwenda kambini, na mimi nikabaki kwenye kambi nyingine. Kemisura akasema *socialism is rice; rice is socialism*, yaani ujamaa ni kula na kula ni ujamaa. Sasa hapa katika kitabu chetu hiki, unamkuta mwanajeshi bado analipwa Sh. 7,600/= kwa mlo. Ni ndogo sana! Tunaelewa *constrains* za Bajeti, lakini Sh. 7,600/= hawezi kweli huyu mtu akala na akafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu, kwa sababu tunayo SUMA JKT, hebu tu-*focus* katika suala la *production* ya chakula. (*Makofi*)

Hii miradi yote mingi ukiichukua kwa pamoja ukiigawa, tunaweza tukapata matatizo. Lakini tu-*consolidate*, tu-*focus* kabisa kwamba sasa Jeshi lijitegemee kwa chakula lenyewe na *the same time* tutumie kambi hizi hizi; Jeshi hili litoe chakula *surplus* liuze kwa Taasisi nyingine. Tulifanya 1983 kwa Magereza tukafanikiwa vizuri tu, bahati mbaya hatukuwa *sustainable*, mambo yakaharibika katikati. Lakini Jeshi la Magereza lilikuwa na tatizo kama hili, tukalikabili, tukakaa kitako pamoja, tukaangalia ni vitu gani wanahitaji, wakapatiwa kwa wakati mmoja, wakafanya kazi.

Sasa hebu tuangalie, kama wana *20,000 hectares* kuzalisha *100,000 hectares* siyo tatizo hata kidogo! Ni kazi ya mwaka mmoja tu; lakini wapewe *inputs* za kutosha, wapewe maelekezo ya kufanya ili tuandokane na hiyo *ration* ya chakula ambayo tunaitegemea zaidi kununua nje na

kadhalika. Kwanza kwa usalama, ni vizuri kama tutauziana wenyewe ndani.

Kwa hiyo, ningependa SUMA JKT badala ya kuwa na miradi mingi, wanahitaji *resources* nyingi, pengine waangalie kwa ku-*focus* ili wafikie malengo. Kwa mfano, tumekuwa na kiwanda cha madawa, tungetegemea leo madawa Jeshini hayana matatizo kwa sababu tuna kiwanda chetu cha madawa. Lakini ukienda kwenye kiwanda cha madawa chenyewe haki-*perform* inavyotakiwa. Kwa hiyo, nafikiri tuwe *focused*, kama ni *capita investment*, ifanywe ya kutosha kabisa ili tuweze kupiga hatua badala ya kurudiarudia kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulisema ni kwamba, Mheshimiwa Waziri amesema vizuri tu suala la amani ya nchi yetu. Najua tunaweza tukaimba tu nyimbo kama amani, amani, amani, lakini lazima kuna vitu ambavyo kama hatukuviangalia, amani hii inaweza ikavurugika wakati wowote. Huwa nasema amani ni sawasawa na yai jeteta. Yai jeteta likianguka linatawanyika moja kwa moja.

Kwa hiyo, la kwanza ningeomba kauli zetu tunazozitoa zisiashirie kwa aina yoyote ile kwamba amani inaweza ikavurugika. Kauli tu! Kauli ni kitu kibaya sana. Kauli inachochea, inahamasisha na inatoa elimu. Kwa hiyo, tujitahidi sana kuepukana na kauli ambazo zinaweza kusababisha nchi yetu ikaingia katika vurugu na ikaondokana na amani tuliyonayo. (*Makofi*)

Nalisema hili kwa nini? Hawa wakubwa, mwaka juzi kwenye *IPU* tuliona ajenda moja *very interesting*. Walisema: "*Distribution of power and not wealth.*" Nikaitafakari sana, nikasema hawa wanakusudia nini? Sasa nilipoona ile *Arab spring*, juzi naangalia Syria, baada ya wale *Arabs* kuteka maeneo mawili ya mafuta, ndiyo wakubwa sasa wamekaa wanasema, sasa tunaondoa *embargo* ya mafuta. Mnaweza mkauza mafuta. Lakini wakauliza, hivi nyinyi vita vyenu hivi

mnavyopigana pigana, vinawa-*cost* kiasi gani kwa siku?  
Wakasema *about 50 million dollars*.

Kwa hiyo, tatizo sasa ni kuyaondoa haya mafuta mliyoteka yakatufikia sisi. Wakasema ndiyo. Wakawa tayari kuwapa fedha kwa sababu tayari wameshateka nini? Mafuta. Nasi tukipiga kelele hivi, hii gesi itagawanywa tu. Watakuja hapa, watasema kwamba bwana ni *democracy* na nini, kumbe *focused* ni gesi, *focus* ni mafuta. *There is nothing!* Wamegawana mafuta Iraq, wamegawana mafuta Libya, leo wanagawana mafuta Syria. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kauli zetu na vitendo vyetu, lazima tuangalie kwamba rasilimali zetu tulizonazo ni sehemu kabisa ya kuvunjika kwa amani ya nchi. Siyo kwamba tunafanya sisi, hapana. Wanatuchochea tu sisi ili wapate hizo rasilimali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na Mkutano Arusha, tulialikwa kwa *investor*, nikawauliza tu kwamba hivi sisi tutakuwa salama kiasi gani kwa raslimali hii ambayo tunayo? Hawakujibu! Wakanyamaza kimya! Kwa sababu hawafaidiki na raslimali kama tupo kwenye amani. Watafaidika na raslimali zetu kama tupo kwenye vita. Ndiyo *DRC* na mahali pengine popote pengine. (*Makofi*)

Kwa hiyo, moja ambalo naliomba sana na tena naliomba sana kwa Watanzania wenzangu wote, ni kwamba tunaweza tukaona jambo la kawaida kuchochea jambo lolote lile. Kesho mnachochea kuchinja kitoweo na kadhalika, mnaliona la kawaida tu; kesho mtachochea kitu kingine na kesho yake mtasema gesi, tufanye hivi; wenzetu hao wanapalilia hivyo na ndiyo maana wamepaliliwa hata Malawi leo, wanapiga kelele, siyo bure! Kuna raslimali gani baadaye watakaa wazigawe wazichukue? Wanafanya hivyo! Hawana dini nyingine zaidi ya kugawana raslimali zetu. (*Makofi*)

Ninaomba sana Ndugu zangu, tujitahidi sana kwa kauli zetu na vitendo vyetu kudumisha amani ya nchi yetu.

Tunaweza tukawa na makosa na matatizo yetu, lakini tutafute *solution* ya kutatua matatizo yetu wenyewe. Tukiwa na matatizo kwenye CUF, basi tutakaa wenyewe kwenye CUF tuyatatie, wakiwa na matatizo CHADEMA, basi watakaa CHADEMA watatie na wakiwa CCM basi watakaa CCM watatie, wala siyo dhambi wakiunda hata Kamati kumi. Lakini watatie matatizo yao. Tukae pamoja tu-*solve our problems internally*. Hata *ma-DC* wakiwa na matatizo, watayatatie matatizo yao ndani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Tujitahidi kutatua matatizo yetu. Kwa hiyo, naomba sana amani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Deo Sanga dakika tano!

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa namna ambavyo Waziri amewasilisha hapa namna ambavyo wanavyolinda mipaka yetu, hususan na sisi wa Mkoa wa Njombe na hasa Ludewa mpaka wa Malawi na Tanzania kwa namna ambavyo wananchi kule walikuwa na hofu sana kwa taarifa ambayo Waziri ameisema hapa, nimefarijika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine niseme tu kwamba kule Makambaku tuna tatizo la mipaka juu ya wananchi na vijiji hususan Kata ya Mlowa, Kata ya Mahongole na Kata ya Kitandililo. Nimewahi kuongea na

Waziri na alinahidi kwamba angeweza kuja kuongea na viongozi hawa ili atembelee aone eneo ambalo linazungumzwa. Nirudie tena kumwomba sana Mheshimiwa Waziri kama ambavyo aliahidi kuja na hajaja ili kuongea na viongozi juu ya mipaka ambayo inapakana na Jeshi letu. Wananchi hawa hawana tatizo, kwani Jeshi ni mali yao. Kwa hiyo, wako tayari uje kuongea nao kuhusu mipaka ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine wamesema wenzangu hapa juu ya vijana ambao wamekuwa wakienda JKT. Jambo hili wakati fulani linaletwa kwenye Wilaya zetu na linapoletwa kwenye Wilaya zetu wakati fulani linakuwa kama lina kificho, unasikia tu watu wameshakwenda JKT na wameshaajiriwa au wameshakwenda Magereza au wameshakwenda Polisi.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kamba jambo hili linaposhuka Wilayani basi lipelekwe kwenye Vijiji husika ili watu wote katika Wilaya hiyo wapate taarifa kwamba sasa kunahitajika vijana wa kwenda JKT au Polisi au Magereza, ili watu waweze kujaza kwa namna ambavyo Serikali imetangaza kuliko ilivyo sasa, yanakuja kutoka matangazo, watu wanapokwenda kwenye maeneo husika, wanaambiwa tayari nafasi zimeshajaa. Jambo hili liwe wazi, kwani litasaidia sana kuliko ambavyo lipo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya mafao hasa ya wajane. Wajane wa Askari wakati wanapofuatilia kutoka kwenye Wilaya na Mikoa kuja Makao Makuu, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana. Wakati fulani wamekuwa wakitujia sisi viongozi wa kisiasa kutuomba kwamba kila ukifuatilia hupati majibu.

Naomba sana Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Usalama iweze kuliona hili kuweka Kitengo Maalum ambacho kitakuwa kinashughulikia jambo hili kwa muda na wakati kuliko ambavyo iko sasa watu wanakwenda kwa muda mrefu, hawapati majibu, wakati fulani wengine wanakata mpaka tamaa kupata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu waliozungumzia habari ya kwenda JKT. Nilisema kipindi kile kilichopita kwamba hata sisi tupo tayari kwenda JKT ili tupitie huko, tuwe wakakamavu kama ambavyo Mjumbe mmoja amechangia hapa, nami nitakuwa tayari muda utakapofika kwenda huko. Naomba niorodheshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba wakati Waziri anafanya majumuisho, aniambie hili suala la kufuatana na mimi kwenda Makambako kwa ajili ya kwenda kuzungumza na wazee wa Makambako kwa ajili ya mipaka ya Jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa dakika ulizonipa na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Clement, dakika tano tafadhali.

**MHE. AMINA CLEMENT ANDREW:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninakushukuru kwa kunipa dakika tano za kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa masikitiko makubwa japo hapa Bungeni siyo mahali pa kusikitika, lakini kwa masikitiko makubwa na majonzi, mwaka 2012 nilipochangia hotuba hii niliomba kwamba kule Zanzibar kuna kijiji kimoja kinaitwa Unguja Ukuu ambapo Wanajeshi wanafanyia mafunzo wakati wa mafunzo. Nilichokuwa nimekiomba, ni kwamba kile kijiji sasa hivi kimezungukwa na wanavijiji wengi.

Kwa hiyo, Wanajeshi niliwaomba watafute maeneo mengine mbadala ili kufanya mafunzo yao ya Kijeshi. Kwa sababu zamani Wanajeshi walipokuwa wakifanya mafunzo walikuwa wakifanya nje ya mji sana, hawaonekani, wala hawasikiki na mtu yeyote wakati wakiwa kwenye mafunzo. Lakini sasa hivi wako karibu na vijiji na pale panatokea matukio tofauti.

Mwisho mwa mwaka uliokwisha, watoto wakiwa wanacheza kwenye maeneo hayo, walikuta chuma wakakichezea. Chuma kile kililipuka na mtoto akafariki papo hapo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri sana kwamba kabla Wanajeshi hawajakwenda kufanya mafunzo, itolewe elimu kwa wanavijiji pindi wanapokuta mambo kama hayo, watoto wasichezee au wakatazwe kwenda. Lakini sijui watakatazwa kwa njia gani wakati kule ndiyo maeneo watu wanalima na kufanya shughuli za ufugaji. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali hili eneo la Unguja Ukuu, Kae Pwani, Tindini na Kikungwi kuangaliwe kwa macho ya huruma kwa sababu matukio mengi yameshatokea, nyumba zimeshabomoka na pia mpaka watoto wameshafariki dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwajulisha Watanzania wote kwamba Wanajeshi katika nchi hii ya Tanzania ni wafanyakazi wenye kazi ngumu kuliko Tanzania yote, kwa kazi yao wanayoifanya ya kutulinda na kututetea. Nasi tuna haki, tuwatetee. Wanajeshi huwa wanapelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kupata mafunzo kuja kuilinda nchi yetu. Hivyo basi, naiomba Serikali mafunzo hayo huwa yanachukua muda wa wiki mbili na kule wanakwenda kusoma mafunzo magumu ya kivita na kurusha ndege. Kwa mfano, juzi tumeona zile ndege zinazozunguka angani, zinaning'inia, hatari tupu!

Kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba yale mafunzo ya Kijeshi yanayokwenda kuchukuliwa nje ya nchi kwa muda wa wiki mbili, waongezewe angalau mwaka mmoja kwa sababu siyo rahisi mtu kwenda kucheza juu angani, ambapo hakuna mti wa kuzuia, hakuna ardhi ya kusimama labda ikidondokea kule kule juu, kutumia wiki mbili kufanya mafunzo yale.

Vile vile naomba Wanajeshi tumesema tuwatetee, lakini hatuwatetei, ni haki yao. Katika Jimbo langu Ubago kuna nyumba za Wanajeshi, zile nyumba hazifai, wanaporudi makazini Wanajeshi wanakaa sehemu mbaya ya



kujipumzisha na kufanya mambo mengine ya nyumbani, lakini nyumba zao mbaya hazijafanyiwi ukarabati kwa muda mrefu, nyumba hazina maji, akina mama na watoto wahangaika kwenda kutafuta maji mbali. Lakini pia na maeneo wanayofanyia kazi Kambini kama Ubago na Kambi nyingine, bado ni chakavu sana, mbovu na hazina maana. Kwa ufupi ukijivunia kusema hawa ndio wanajeshi wa Tanzania wanaotulinda hata ukimleta mgeni, basi atakucheka, "kweli hawa ndio wanaowalinda, mnawafanyia mambo kama haya!" Naiomba sana Serikali!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kidogo nielekee kwenye pesa za ujuzi za Wanajeshi. Wanajeshi kuna kipindi wanakwenda kwenye masomo, na wakiwa kwenye masomo huwa wanachanganyika kwa maana ya Koplo, Sajenti, Luteni na vyeo vingine tofauti tofauti. Wanasoma darasa moja na wanapata ujuzi mmoja, lakini wakati wa kuongezewa zile pesa za ujuzi wanapewa pesa tofauti na wakati watu hawa wamekwenda kusoma darasa moja. Pengine Koplo alipasi vizuri sana, lakini anayepewa pesa nyingi pengine ni Luteni au cheo kingine. Mtanisamehe, hivyo vyeo sivijui vizuri, lakini cheo kingine anapewa pesa zaidi kulingana na cheo chake. Kwa hiyo, naomba mafao haya wapewe sawasawa kwa sababu wote wamesoma darasa moja, lisifanywe hili kwa sababu huyu ana cheo kikubwa, apewe pesa nyingi, hapana! Wakati wa cheo kikubwa hizo pesa zitapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee kwenye posho za nyumba wanazokodi Wanajeshi wanaoishi uraiani. Ile posho ya nyumba wanayopewa ni ndogo hasa kwa mtu mwenye familia. Sasa hivi maisha kwa vyovyote yamekuwa yapo juu. Pesa zile kidogo hazitoshi kwa watu wenye familia kukodi nyumba. Naiomba Serikali hili ilitazame kwa kuwa tunajua Majeshi mchango wao ni mkubwa sana katika nchi yetu, tunawategemea sana walinde, watulize amani na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee kidogo kwenye kiinua mgongo cha Wanajeshi. Wanajeshi wakiwa wanataka kuacha kazi kabla ya miezi 18 huwa Mwanajeshi yule

anahangaika pilikapilika huku na huku. Anatoka Zanzibar kile siku ukimwuliza anakwambia mimi nakwenda Hazina kuharakia mafao yangu nitakapoacha kazi. Je, ni kwa nini Wizara hii haisimamii kikamilifu hawa Wanajeshi wanaotarajiwa kuacha kazi karibuni wakashughulikiwa mafao yao ili anapoacha kazi apewe pesa zake za kiinua mgongo bila ya matatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo sana nielekee kwa wanajeshi wanaokwenda Darful Sudan. Huu utaratibu wa kwenda Darfur Sudan ni mzuri kwani Wanajeshi wanakwenda kule vizuri, pia wanapata mafunzo na pia wanalinda na majirani zetu. Huu utaratibuni mzuri sana, lakini umeingia kidogo hitilafu, kwani Wanajeshi wanaporudi Darfur wakitoka kule wanakuwa wamechoka sana, wakifika hapa wanatakiwa wapumzike, na ile pesa yao waikute tayari imeshatengenezwa ili wakifika tu nchini wapewe pesa yao ili wafanye mambo mengine. Je, ni kwa nini Wanajeshi hawa wanaporudi kutoka Darfur wanakuta zile pesa bado, mpaka wahangaike wiki mbili au tatu ndiyo wapatiwe mafao yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu dakika tano za mwisho, halafu Mheshimiwa Waziri Membe!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa sababu umenipa muda wako mwenyewe, yaani *Speakers control time*. Kuna jambo muhimu sana nataka kulizungumza kwa dakika tano kuhusiana na bajeti ambayo imeombwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 41 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kwamba bajeti nzima ambayo inaombwa ni zaidi ya Shilingi trilioni moja. Ngome wanaomba Shilingi bilioni 661, *JKT* wanaomba Shilingi bilioni 193 na Wizara wanaomba Shilingi bilioni 248 ambapo jumla ukifanya *additions* ni zaidi ya Shilingi trilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni fedha nyingi sana. Ninachotaka kuzungumza ni kwamba bajeti ya maendeleo ni ndogo sana. Ukiangalia haya mafungu, bajeti ya maendeleo kwa Ngome ni Shilingi bilioni 10, JKT ni Shilingi bilioni sita, Wizara ya Ulinzi ni Shilingi bilioni 229. Kwa hiyo, jumla ni kama Shilingi bilioni *240 plus out of one trillion*.

Mheshimiwa Naibu Spika, majeshi katika nchi zilizoendelea ndiyo *centres of excellence* katika *research and development* ya teknolojia. Watu wengi hawafahamu, lakini *computer* zilianzia Jeshini wakati wa Vita vya Pili vya Dunia. *Computerya* kwanza ilitengenezwa ili kuvunja ile *code*, lakini sijui *code* kwa Kiswahili ni nini; ya Wajerumani wakati wa Vita vya Pili vya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, majeshi ni mahali pa kutengenezea teknolojia ya hali ya juu. Teknolojia hii ya kwenda kwenye *outer space* ya kupeleka binadamu mwezini na kwenye angaza juu, imeanzia Jeshini, ndiyo ikishatoka Jeshini inasambaa *to the rest of the economy*. Kwa hiyo, ukiwekeza katika *research and development* kwenye *Military*, unatengeneza teknolojia ambayo baadaye ina-*flow down to the rest of the economy*. Mimi siyo mchumi, lakini Wachumi wanasema ni *multiplier effect*.

Kwa hiyo, *research and development* kwenye *military* ni muhimu sana siyo tu kwa ajili ya masuala ya ulinzi, lakini vilevile kwa ajili ya masuala ya kiuchumi. Wamarekani kuna kitu wanaita, *the Military Industrial Complex*. *Military Industrial Complex* ndiyo hii ninayoizungumzia, Majeshi *a centres of excellence* katika *development of high-tech* halafu hiyo *high-tech* inatengeneza *not only armaments* bali pia inaingia kwenye *Civilian use*. (*Makofi*)

Sasa kwa utaratibu wetu huu wa kupeleka fedha yote kwa ajili ya kula sasa hivi, tunaweka mafungu makubwa makubwa, *more than eight hundred billion* kwa ajili ya matumizi ya *hand to mouth*, tunaacha *research and development*, hatufiki! Hatufiki! Jeshi ni mtumiaji mkubwa sana wa raslimali, usipoangalia Jeshi ni mtumiaji mkubwa wa

raslimali ambazo hazizalishi. Ukinunua kifaru, hujanunua trekta. Ndiyo maana ukienda nje ya jengo la *UN* kuna sanamu pale nzuri sana, imesema: *Let's bit swords into ploughshares*, tuvunje hizi Bunduki na Majambia ya vita tutengeneze majembe ya kulimia.

Sasa tukiwa Taifa la wajanja, tutaelekeza fedha nyingi katika *research and development* ili iingie *to the rest of the economy*.

Matumizi yetu ya Kijeshi siyo tu yatupatie ulinzi ambacho ni kitu kizuri sana lakini vilevile yatutengenezee teknolojia itakayotumika kwenye sehemu nyingine za uchumi wa kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hicho tu ambacho nilitaka kukisema. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kufufua mafunzo ya JKT kwa vijana wa Tanzania. Naomba mafunzo hayo kwa Waheshimiwa Wabunge yaliyoanza, yaendeleo, maana vijana wanafundishwa mambo ya ulinzi na uzalendo. Pia naipongeza Serikali kwa kuanzisha Chuo cha Ulinzi na Taifa *NDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali itoe mafunzo ya lazima ya viongozi wote wa Vyama vya Siasa na pia Wabunge wote wenye umri mkubwa katika Chuo hiki. Ninaamini mafunzo haya yataimarisha uzalendo na kuipenda nchi miongoni mwa makundi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naiomba Serikali kutoa fedha zote zinazopangwa kwa Jeshi wakati wa bajeti

Kamati ya bajeti ya Bunge ifuatilie kwa karibu sana bajeti ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama katika hotuba yake kuhusu barabara za pembezoni, hilo ni muhimu sana kwa ulinzi wa nchi yetu, siyo tungoje uvamizi. Mimi tangu kuingia Bungeni nilionesha umuhimu sana wa hizo barabara hasa katika mwambao mwa Ziwa Tanganyika, hakuna barabara kabisa. Sasa ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuna Vituo vya Jeshi katika mwambao mwa Ziwa Tanganyika vya Kasanga, Kirando na Ikola. Katika Mikoa ya Rukwa na Katavi sasa hakuna kabisa barabara za kuaminika kwenye vijiji hivyo na vijiji vingine hakuna barabara kabisa. Vijiji hivyo ni Kalila, Milombe, Kazovu, Isaba, Chongo, Kate, Kisambala, Ninde, Msamba, Lyapinda, Mwinza, Lusebwa na Izinga.

Kwa kuwa Jeshi wana vifaa na madaraja, tunaomba Jeshi letu lisaidie hizo barabara maana Halmashauri zetu hazina uwezo kabisa; usafiri wa kutegemea majini tu na Ziwa Tanganyika huwa linachafuka sana na uwezekano wa kutumia *boat* ni hatari sana wakati wa mawimbi makubwa. Hivyo barabara ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tujengewe barabara itakayounganisha nchi za *DRC Congo*, Zambia na Burundi kupitia Vijiji vya Kasanga, Kirando, Ikola na Kigoma ambako kuna Makambi ya Jeshi ili itusaidie ulinzi wetu.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameeleza majukumu ya Wizara ya Ulinzi, pia kazi ambazo zimepangwa kutekelezwa kwa mwaka 2013/2014. Ni ukweli usiopingika kwamba majukumu hayo na malengo yaliyopangwa yanahitaji hela za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ihakikishe fedha zinazooombwa na Wizara hii zinatolewa kama zilivyoombwa. Jeshi letu ndiyo uhai na uti wa Mgongo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ihakikishe fedha imeruhusu watu binafsi na Makampuni ya Watu Binafsi kumiliki silaha. Naomba sera hii iangaliwe upya hasa kwa sababu silaha hizi zimetumika vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iyaelekeze Makampuni ya Watu Binafsi iwatumie askari wetu wastaafu kwa shughuli za ulinzi hasa kwa sababu wao tayari wana viapo vya kulinda maisha ya Watanzania. Hivyo, kwa vyovyote vile hawawezi kugeuka na kuanza kuwaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ianzishe Mfuko Maalum wa kuwahudumia Askari wetu ambao wamepata ulemavu wa maisha wakati wakitimiza majukumu yao ya kulinda nchi yetu. Pia mfuko huo uhudumie familia za Askari wetu hao wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Askari wetu wametolea mhanga maisha yao, naiomba Serikali yetu iwajengee wote makazi ya kudumu kulingana na nyadhifa zao halafu uwekwe utaratibu wa kuwakata fedha kidogo kidogo kutoka kwenye mishahara yao hadi wanapostaafu wawe wamemaliza kulipia nyumba hizo. Kwa kufanya hivyo, tutawapunguzia kadhia ya ukosefu wa makazi baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba pia Serikali itenge fedha za kutosha ili itekeleze milipuko chakavu na kununua mingine kwa ajili ya ulinzi wa Taifa letu. Pia iyakague maghala ambayo yanahifadhi milipuko hiyo ili kuepusha maafa kama yale yaliyotokea Kigamboni na Gongolamboto.

Mheshimiwa Naibu Spika ili kuondoa migogoro na wananchi, naishauri Serikali iyapime Makambi yote na

kuyapatia Hati Miliki na wananchi wasiruhusiwe kujenga makazi yao karibu na Kambi za Majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wakati nachangia hotuba ya Waziri wa Maliasili - Mheshimiwa Kagasheki, niliomba Serikali ilitumie Jeshi letu lianzishe *operation* chakaza majangili, ili kulinda wanyamapori katika hifadhi zetu za Taifa. Watalii wengi huja nchini kuangalia wanyama, hivyo wakiangamia wanyama hawa, watalii hawatakuja tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nashauri Serikali na Jeshi letu kupitia JKT lianzishe kilimo kikubwa cha kisasa ili Taifa liondokane na aibu ya kuagiza chakula cha msaada kutoka nje.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yafuatayo yazingatiwe na mengine nipate ufafanuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali ya kisiasa kutokuwa na utulivu nchini Congo – *DRC* kwa muda mrefu, kumekuwepo matukio ya uvunjifu wa amani katika Mikoa ya Rukwa na Katavi na hasa ndani ya Ziwa Tanganyika na wakati mwingine Vijiji vimekuwa vikiingiliwa na waporaji mara kwa mara. Kwa mfano, Kijiji cha Msamba kimeshuhudia wafanyabiashara wake wakivamiwa na silaha za kijeshi na kuporwa zaidi ya mara tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kata ya Kala Kijiji cha Mpsa kimekuwa kikivamiwa na kuporwa mali za wafanyabiashara wake mara kwa mara. Vile vile wafanyabiashara na wavuvi wamekuwa wakivamiwa mara kwa mara wakiwa katika shughuli zao ndani ya Ziwa Tanganyika, naomba Serikali inijulishe ina mpango gani kuthibiti mpaka wa Ziwa Tanganyika ambao ni mrefu sana na hakuna kituo kikubwa cha kijeshi ukiacha Kiteule cha Kirando na Ikola. Napendekeza na kuhimiza, ni lini mpango wa kujenga Kambi Wilayani Nkasi utaanza ili kuthibiti matukio

haya yanayotishia amani katika Ukanda wote wa Ziwa Tanganyika kwa Mikoa ya Katavi na Rukwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, SUMA JKT naipongeza Serikali kwa mpango wake wa kuimarisha kilimo nchini kupitia Jeshi kwa kuanzisha Shirika. Hili tayari mabadiliko katika kilimo yameanza kuonekana, kwani tayari wananchi wengi wamepanua kilimo kwa matumizi ya matrekta. Kwa sababu hiyo, tishio la njaa nchini limeanza kutoweka, kwani uzalishaji mazao ya nafaka unapanda siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iipatie SUMA JKT mtaji wa kutosha na tunaridhika na kazi yake ya kusambaza zana za kilimo. Upo uvumi wa wafanyabiashara kuwa SUMA JKT haifanyi vizuri au ina matrekta na zana zisizo na ubora siyo kweli, nikiwa mdau, matrekta ni mazuri na yanafanya kazi vizuri. Naomba Serikali iwaongezee mtaji SUMA JKT iweze kumudu mahitaji makubwa yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tusiruhusu kabisa undugu, ubinamu na ushemeji katika ajira za Jeshi. Twende na maadili na pia jiografia sawia nchi mzima Jeshi. lazima liunganishe watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri Waheshimwia Wabunge waendeleo kutengewa nafasi ya kwenda Jeshini kadiri wanavyopata nafasi, kwani ni jambo zuri na mfano wa kuigwa kwa viongozi na wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa vijana wote kupitia JKT uimarishwe na mafunzo ya ufundi yaongezwe JKT. Vile vile muda uongezwe ili mafunzo yatolewe ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri *intake* maalum ianzishwe na ichukue miaka miwili na wafundishwe ulinzi na ufundi ili wanapotoka baada ya kuhitimu wakachangie nguvu kazi katika sekta za kiufundi na kuzalisha kwa viwango.



**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ihakikishe ulinzi wa mipaka ya nchi unaimarishwa hasa maeneo ya baharini na Maziwa Makuu. Mfano, kuweka kikosi cha ulinzi katika Ziwa Victoria hasa maeneo ya Ukerewe, kwani ni mpaka kati ya nchi za Kenya, Uganda na nchi za jirani kama Somalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wote wanaomaliza mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa waajiriwe ili kuondoa mianya ya wahitimu kuwa wahalifu uraiani kwani watakuwa na mafunzo ya kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama yanafanya kazi kubwa ya kulinda usalama wa nchi yetu, inatupasa kuwalipa vizuri kadri iwezekanavyo ili kuondoa manung'uniko kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Jeshi la Kujenga Taifa lifundishwe stadi za kazi kama vile ufundi uashi, umakenika, useremala na kadhalika ili kuwawezesha vijana wanaomaliza JKT kujiajiri.

**MHE. HAMOUD ABUU JAMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema na kuniwezesha nami nichangie bajeti hii muhimu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa ya mwaka 2013/2014. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake nzuri na makini. Napenda kulipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri inayoifanya ya kulinda nchi na mipaka yetu. Kufanya hivyo kunaiweka nchi yetu katika hali ya usalama, amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba nchi inapokuwa salama, ndipo watu wake huweza kuishi kwa amani na utulivu. Amani na utulivu vinapotawala katika nchi, watu wake huwa na uhuru wa kufanya shughuli mbalimbali kwa ajili ya kujipatia mahitaji yao ya kila siku na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yao. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuweza kudumisha amani na utulivu katika Taifa, kuchukua vijana wengi zaidi, kwani kiwango cha

kuchukua vijana kujiunga na Jeshi kwa awamu mbili kila mwaka bado hakijitoshenzi. Kufanya hivyo, kutatua tatizo lililopo hivi sasa la wananchi kulalamikia utaratibu uliopo wa kuwapata vijana hao, kwani kumekuwa na urasimu kwa baadhi ya maeneo hasa Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matatizo ya kuzagaa na matumizi mabaya ya silaha. Naomba niishauri Serikali kwamba ni vyema Makampuni ya kigeni yasiruhusiwe kuweka walenzi wao na badala yake Makampuni hayo yapewe ulenzi na vyombo vyetu vya dola. Vilevile Serikali yetu imekuwa na malengo mazuri sana kwa kuanzisha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria; lakini idadi ya vijana wanaojiunga imekuwa ndogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi. Ni vyema Serikali ikajipanga kuongeza idadi hiyo kadiri inavyofaa. Hata hivyo, Serikali iboreshe maslahi ya Wanajeshi wetu pamoja na mazingira yao ya kuishi na kufanyia kazi. Uwekwe utaratibu wa kushughulikia madeni binafsi ya wanajeshi na kuepuka kuongezeka kwa madeni yasiyolipwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Chuo cha Ulinzi wa Taifa kina umuhimu mkubwa katika mustakabali wa Taifa letu, Serikali iweke utaratibu wa kutenga fedha za kutosha kuendesha mafunzo kwa watu wanaokusudiwa na kuzitoa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamekuwa wakilalamikia sana tatizo la wanajeshi kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga wananchi pale inapotokea tatizo. Hali hiyo imekuwa inawajengea uwoga wananchi pale wawaonapo wanajeshi wakipita Mitaani. Matukio hayo yamekuwa mengi na siyo mageni kutokea. Naiomba Serikali iwakumbushe hawa ndugu zetu kufuata sheria na taratibu zilizopo na kuacha kujichukulia sheria mkononi.

Pia kumetokea matatizo ya raia kuvaa nguo za Jeshi ilhali sio wanajeshi na kufanya vitendo vya kihalifu na udanganyifu. Nashauri Serikali kuwachukulia hatua kali watu hao na kama ikifahamika, nguo hizo wamepewa na ndugu

zao ambao ni Maafisa wa Jeshi, basi wachukuliwe hatua kali za kinidhamu ili kukomesha tabia hiyo haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba izingatiwe pia kwa Jeshi letu kupatiwa vifaa vya kisasa ili kwenda na wakati na Majeshi ya nchi nyingine; kuwapatia mafunzo ya Kijeshi Maafisa wetu nje ya nchi ili kujifunza mbinu mbalimbali za kisasa. Naiomba Serikali kuzidi kuliboreshea kiutendaji Jeshi letu la Majini ili kulipa wigo mkubwa wa kufanya doria katika mipaka yetu baharini na pia kutoa ulinzi kwa Makampuni ya Ulinzi kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inakabiliwa na uhalifu mkubwa. Kuna magendo ya sukari na mahindi yanayovushwa kutoka Tanzania kwenda nchi za jarani za Kenya na Uganda. Jeshi la Polisi limekuwa likijitahidi kuzuia magendo hayo, lakini inavyoonekana linashindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushindwa huku kulisababisha Waziri Mkuu wa Tanzania - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kutangaza kwamba atakuwa tayari kutumia Jeshi la Wananchi kuwekwa mipakani ili kupambana na wafanya magendo ya sukari na mahindi. Kwa bahati mbaya, kauli hiyo ya Waziri Mkuu haikutekelezwa na biashara ya magendo imeendelea kushamiri hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania sasa hivi imeshamiri ujangili mkubwa. Tembo na faru wanamalizika kwa kasi kubwa sana. Wakati huu wa amani nashauri Jeshi la Wananchi wa Tanzania litumike kupambana na uhalifu huu, wakishaudhibiti dhipo Jeshi la Polisi liachiwe.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Mheshimiwa Nahodha Vwai, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Majenerali, Maafisa na Viongozi

wengine wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na ya kujitoa kitaifa kwa kutuhakikishia usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye suala la Jeshi la Kujenga Taifa. Naiponza Serikali kwa kurejesha mafunzo kwa vijana kupitia JKT. Lakini naomba vitengo vilivyomo katika JKT kwa suala la ujasiriamali liimaliswe kwa kutumiwa kutoa huduma kwa ukubwa zaidi kwa jamii. Badala ya Vikosi vya uzalishaji kutumika kujitosheleza wenyewe tu, watumiwe na jamii kwa kulipwa kujenga nyumba za watu binafsi, kulima na kufanya kazi nyingine kwa *Contract*. Hii itawawezesha kupata kipato, lakini vilevile Watanzania tutajivunia vikosi kazi vya vijana wetu.

Kwa hali hii, JKT ijipange kibiashara kuweka *Management* nzuri na usimamizi bora ili kujiendesha kibiashara. Watafute wataalm wa kuwatengenezea mfumo wa kibiashara wenye vitengo mbalimbali na kujiwekea mahitaji ya kujiendesha. Wanaweza kuanza kwa kuingia ubia na Makampuni toka Israel, Afrika Kusini, Marekani na hata China na Vietnam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo yenyewe ya JKT, tunaomba Uongozi uhakikishe usalama wa vijana wa kike dhidi ya vitendo vya unyanyaswaji wa kijinsia ikiwa ni pamoja na ubakaji. Jeshi liweke wazi *Code of Conduct*, aina ya adhabu zitakazotolewa kwa watakaotenda maovu hayo. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akijibu hoja atueleze:-

- (1) Taratibu zilizopo zinazosimamia unyanyaswaji wa jinsia Jeshini?
- (2) Adhabu zipi zipo na hutumika kwa kosa hili?
- (3) Hatua zipi zipo kuhakikisha makosa haya hayatokei au yanapungua?
- (4) Waathirika hupata fidia gani toka Jeshini kwa madhara haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwahakikishia wazazi na vijana usalama huu peke yake, kutawawezesha vijana kujitokeza kwa wingi.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, bajeti ya Wizara ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya Makambi yetu ya Majeshi. Kwa mfano, maji yamekuwa ni tatizo sugu katika Makambi kadhaa kama Bulombola na mengineyo. Nyumba za Askari imekuwa nalo ni tatizo la muda mrefu. Askari wa Jeshi wanafanya kazi ngumu, lakini makazi wanayoishi ni hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kumekuwa na uhaba mkubwa wa sare za Askari na buti kwa ajili ya mazoezi. Mgao unapita baada ya muda mrefu, hivyo kupelekea Askari waishi maisha ya udhalili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu, hususan wanaomaliza bila hata ya kuwa na ujuzi wowote.

Napenda kushauri Vyuo vya Ufundi vingejengwa katika Makambi mbalimbali ili watoto waweze kujijiri mara baada ya kumaliza mafunzo yao na siyo tu kufikiria kufanya ujangili kwa sababu wamepata mafunzo ya silaha.

**MHE. GOODLUCK J. MADEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha - Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa uongozi wake mahiri kwa Wizara hii muhimu kwa ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Bwana Job Masima – Katibu, Eng. Musa Iyombe - Naibu Katibu Mkuu, Gen. Davis Mwamunyange na Makamanda kwa kazi yao nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1984 Serikali ilitwaa ardhi ya Kijiji cha Oldonyosambu Kata ya Oldonyosambu Wilayani Arumeru na kukabidhi Kikosi cha Ulinzi wa Anga. Serikali iliahidi kuwapatia wananchi wa kijiji hicho ambao ardhi yao ilichukuliwa ardhi mbadala huko Oljoro - Laroi. Ardhi iliyotolewa ilikabidhiwa Viongozi na Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ambao waligawana wao na ndugu zao badala ya kuwapatia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa wananchi hao wa Oldonyosambu wanaendelea kutaabika, kwani hawana pa kuishi, kulima, wala pa kuzika wapendwa wao wanapofariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itimize ahadi ya kuwapatia wananchi ardhi ikiwezekana kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya JKT ya majuma matatu yaliyotolewa kwa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi, hayakidhi mahitaji ya kupata mafunzo ya msingi ya ulinzi. Muda uongezwe kwa angalau wiki sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa ni Jeshi muhimu sana kwa nchi yetu ingawa wako baadhi ya Wanajeshi/Watumishi wa Jeshi hilo sio waaminifu kwa kushirikana na wahalifu kulihujumu Taifa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwabaini watumishi hao na kukomesha hali hiyo ili kullijengea heshima Jeshi letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombelo Kata ya *CHITA*, kuna Kambi ya Jeshi. Kambi ya Jeshi hiyo ilikuwa na mgogoro wa ardhi na wananchi wa Chita, hadi kupelekea wananchi kujiorodhesha na kutaka msaada wa kisheria na

kutoa taarifa (*notice*) ya kusudio la kumshitaki Mkuu wa Kikosi kwa kuwaporaa mashamba yao na kuwakodisha kwa Sh. 40,000/= kwa ekari, pia kuwapiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla kusudio hilo halijamaliza muda wake wa siku 90, ambapo lilikuwa linakwisha mwezi Februari, 2013, Mkuu wa Kambi/Kikosi hicho alikubali kukaa kikao cha pamoja kati ya Jeshi, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero na wananchi ili wakubaliane kuhusu mipaka ya Kijiji na Jeshi. Matokeo ya kikao hicho, kilizaa matunda ya kukubaliana mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkuu wa Jeshi (Mkuu wa Kikosi) alishakodisha wananchi, na wananchi walishalima na kupanda mpunga na mahindi katika mashamba, na kwa kuwa muafaka uliofikiwa kuna mashamba yalibaki kwa Jeshi ambayo yalikodishwa; hivyo Jeshi lingetumia busara kuacha watu waliokodishwa waruhusiwe kuhudumia mazao yao na hatimaye wavune na kuacha maeneo hayo kwa Kikosi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi nitoapo maelezo haya, Mkuu wa Kikosi/Kambi ya Chita, ameamua kuwazuia wananchi aliyokodisha mashamba kwa kuwapatia risiti, wasiingie kwenye mashamba aliyowakodisha na kupelekea wananchi kushindwa kuhudumia mazao yao na kuyavuna. Je, hii ni haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wananchi wa Chita wanataka kusikia kauli ya Serikali kuhusu dhuluma hiyo inayofanywa na Kiongozi huyo wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. PROF. ALHAJ JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara hii muhimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao ya wataalm bila kumsahau Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mambo mawili kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 niliahidiwa kwamba wananchi wa Jimbo la Urambo Magharibi wangejengewa Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika Mji wa Kaliua. Kutokana na ahadi hii, wananchi wa Kaliua kwa kupenda sana kuwa na Kambi hii, walitenga eneo. Viongozi Waandamizi wa Jeshi na wananchi walikuja kukagua eneo hilo na kuridhika na eneo hilo. Tunaomba Wizara sasa waanze utekelezaji wa ahadi na hasa ukizingatia kuwa Kaliua sasa ni Wilaya mpya inayojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya mpya ya Kaliua inajumuisha na eneo ambalo lilikuwa linaharibiwa na wakimbizi wa kutoka Burundi waliongia nchini tangu mwaka 1972. Wakimbizi hawa sasa muda wa kurudi kwao ulishafika na wengine wamepewa uraia kwa sharti la kuwasambaza nchi nzima. Hapo Ulyanhulu kuna miundombinu mingi iliyojengwa na Umoja wa Mataifa, Serikali na Wafadhili wengine kama *OPEC*. Kupitia utaratibu huu, tulipata bahati ya kujengewa Kituo cha kisasa cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (*VETA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu eneo hili litabaki wazi kwa kiasi kikubwa hasa baada ya kuondoka hawa wageni-wakazi, yako mazungumzo kwamba eneo hili la hati ya makazi lichukuliwe na JWTZ. Viongozi Waandamizi wa JWTZ wameshatembelea mara kadhaa eneo hili, na inaelekea wanaridhika nalo. Miongoni mwa Taasisi zitakazochukuliwa na JWTZ ni pamoja na *VETA*. Nimeambiwa na wananchi wangu kuwa JWTZ wameahidi kuwa itakapofikia hatua hiyo, basi JWTZ watatujengea *VETA* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, *VETA* hiyo ijengwe katika Mji wa Kaliua Wilaya Mpya ya Kaliua. Nasema hivyo kwa sababu ziko tetesi za Wilaya ya Urambo iliyokuwa Wilaya mama ya Kaliua kutaka kuteka nyara kituo hiki kipya cha *VETA*. Naomba na kusisitiza kwamba Kituo hiki cha *VETA*



Mpya kijengwe Kaliua katika Wilaya Mpya ya Kaliua kwa kuzingatia kuwa ile *VETA* ya zamani itakayochukuliwa na JWTZ imo katika eneo hili la Wilaya Mpya ya Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kukushukuru tena na kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi wa JKT kwa kutimiza ahadi ya kurejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu. Tumeshuhudia ahadi hiyo ikitimizwa kwa ari kubwa na kwa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, hata hivyo napenda kupata majibu juu ya ahadi ya kuanzishwa kwa Kambi mpya ya JKT Wilayani Manyoni kama Serikali ilivyoahidi. Awali ahadi ilitolewa na Serikali tangu Bunge la Tisa kuwa itaanzishwa Kambi Sanjaranda upande wa Manyoni na Ndasho (upande wa Iramba).

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali naomba majibu juu ya ahadi hii hususan pale Sanjaranda Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja ya Wazara hii.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja, kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa Bajeti, Wizara inakabiliwa na changamoto nyingi sana ambazo zote ni muhimu kwa Taifa hili. Ni vyema Serikali ikazingatia na kuongeza Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la mipaka kwenye Makambi ya Jeshi, hivyo kuleta usumbufu katika uendeshaji wa shughuli zake. Maeneo mengi yamevamiwa ama kwa raia kujenga au kulima na shughuli nyingine nyingi. Hili ni tatizo. Ni vyema juhudi za makusudi zifanyike ili kuepuka migogoro ambayo ingeweza kuepukika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba makazi ya Wanajeshi yaboreshwe kwa manufaa yao ili wawe na makazi bora kwao na familia zao.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na ulinzi wa mipaka. Hali ya mipaka katika nchi yetu siyo shwari sana, kwani kumekuwa kukitokea uharibifu kutoka nchi jirani kama Congo ambapo wavamizi wamekuwa wakivuka katika Ziwa Tanganyika na kuwavamia wavuvi na kuwanyang'anya *engine* za boti na hata zana za uvuvi na pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika mipaka ya Zambia, Tunduma na Malawi (Kasumulu) kumekuwa na uvushaji wa vipodozi feki na kuuza nchini Tanzania kwa wingi hali ambayo haifichiki, na vipodozi hivyo vimeleta madhara makubwa kwa watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wetu mipakani hawatoshi. Naishauri Serikali kufanya hima kuongeza Askari katika mipaka yetu ya Zambia na Malawi na kwingineko kama upungufu unavyoonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Askari wetu waongezewe mishahara mizuri na marupurupu ili wasiwe chachu ya tamaa na kupokea rushwa na kuruhusu magendo mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Serikali iwajali kwa kuwapa sare mpya zenye hadhi, wasisubiri mpaka zichakae ndipo wapewe. Pia wapewe buti kwa ajili ya kazi zao za doria, *radio call* kwa ajili ya mawasiliano ya haraka na nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia katika Viwanja vya Ndege kuimarisha ulinzi kwa kuongeza Askari walioajiriwa na Serikali na siyo kutumia Askari wa Makampuni binafsi ya Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anapofanya hitimisho, anihakikishie Serikali imejianda vipi kukabilliana na wavushaji magendo katika mipaka ya Kasumu na Tunduma Zambia ambayo mpaka sasa mipaka hiyo ina mianya ya njia za panya nyingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kupambana na Ukimwi, ni suala mtambuka. Serikali ihakikishe inasogeza huduma za kupima maambukizi ya Ukimwi katika kila Kambi ya Jeshi na kutoa ushauri nasaha. Pia dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi zipatikane bila kukosa. Elimu ya Ukimwi ipatikane bila kuumauma ili vijana wetu waelewe na kuliogopa janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti inayotengwa katika Wizara hii ni ndogo ukilinganisha na majukumu mengi yanayoendeshwa na Wizara hii. Serikali ifikirie sana ili Wizara hii iendeshe shughuli zake kwa usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala wa bajeti unapaswa kujikita katika maeneo mawili, mapato na matumizi. Hata hivyo, mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa miaka ya fedha 2011/2012, 2012/2013 na 2013/2014 imejikita zaidi katika matumizi kuliko mapato. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweke mkazo pia katika eneo la mapato kwa kuwa ina fursa ya kufanya uzalishaji na kuongeza uwezo wa kujitegemea iwapo ufanisi utaongezwa katika vitega uchumi vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha Shilingi milioni 68.2 tu kilichopangwa kukusanywa na Fungu 38 – Ngome, Shilingi milioni 1.5; Fungu 39 – JKT, Shilingi milioni 46.7 na Fungu 57 – Wizara, Shilingi milioni 20; ni kiasi kidogo sana. Iwapo Serikali

imewekeza Shilingi bilioni 20 kwenye nyumba peke yake, tafsi yake ni kwamba fedha nyingi za Umma zimelela ambazo zingewekekwa kwenye miradi yenye tija ingelisaidia Jeshi na Wizara. Aidha, pamoja na vitega uchumi vilivyotajwa kwenye Hotuba ya Waziri, maelezo yatolewe kuhusu vitega uchumi ambavyo miaka ya nyuma vilielezwa kuwa vimefilisiwa au kuhamisha hisa zake, lakini vimejitokeza tena kwenye vitabu vya Serikali.

Mfano, Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu imeitaja Kampuni ya Meremeta kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kuwa mchakato wa kuifilisi ulikuwa unaendelea mpaka mwanzoni mwa mwaka 2013. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ieleze ni mapato kiasi gani Jeshi na Wizara inapata kutokana na ufilisi huo. Iwapo Jeshi na Wizara kwa pamoja wamepata hasara, ni hatua gani zimechukuliwa kwa waliozembea au kutumia vibaya rasilimali za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mapato ya Wizara hii ni chini hata ya asilimia moja (1%) ya Bajeti wakati Wizara ina fursa ya kuwasilisha asilimia kumi (10%) ya Bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani kutaka bajeti iliyopitishwa na Bunge kutolewa katika kipindi kilichobaki kabla ya tarehe 31 Juni, 2013, ili kuepusha malimbikizo ya madeni na vipaumbele kuweza kuzingatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni mbaya zaidi kwa upande wa fedha za maendeleo ambazo zilitolewa kwa wastani wa asilimia 33. Katika kufanya hivyo, kipaumbele kiwekwe katika ujenzi na ukarabati wa maghala ya silaha ili kuepusha maafa kama ilivyojitokeza kwa upande wa Kambi za Jeshi za Mbagala na Gongolamboto.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika utatuzi wa migogoro kati ya Kambi za Jeshi na wananchi na kujenga ujirani mwema, naomba mrejesho kuhusu hatua zilizochukuliwa juu ya masuala niliyoyaeleza mwaka 2011 na

2012 kuhusu Kambi ya Jeshi iliyopo Karibu na Makaburi katika Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wa awali, niliwasilisha kuhusu hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuwa masuala yafuatayo ya nyogeza ni muhimu yazingatiwe. Fungu 38 - Ngome; kifungu 1001, kasma 270,300, ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Ulinzi wa Taifa ni muhimu katika mwaka wa fedha 2014/2015 ikaongezwa kiwango cha kufika Shilingi bilioni saba ambayo ndiyo mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kiwango kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kitolewe chote kwa wakati tofauti na ilivyokuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa, naunga mkono pendekezo la kutoa kipaumbele kwa wahitimu wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa katika nafasi za mafunzo na ajira katika Jeshi la Wananchi, Polisi, Magereza, Zimamoto, Uokoaji, Uhamiaji, Vikosi vya kuzuia Ujangili na Usalama wa Taifa. Aidha, wahitimu wote wa JKT ambao wanataka kufanya kazi za Ulinzi waingizwe katika orodha ya wafanyakazi watarajiwa wa Shirika la *SUMA Guard Ltd*. Kampuni ya *SUMA Guard Ltd* ijengewe uwezo wa kujitegemea na kupata mapato kutokana na ulinzi wa nyumba za Viongozi na Taasisi mbalimbali za Umma pamoja na Kampuni binafsi zinazohitaji ulinzi kutoka kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuongeza ufanisi wa SUMA JKT, mapitio yafanyike kuhusu amri iliyotolewa na Mheshimiwa Rais mwaka 1982 katika tangazo la Serikali Na. 116 kupitia *the Corporation Sole Establishment Act* na badala yake itungwe Sheria ya SUMA JKT. Kiwango cha uwekezaji ambao JKT inaweza kufanya kinahitaji mfumo thabiti wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kurejesha mafunzo ya JKT, uambatane pia na mapitio ya Sera na Sheria

zinazosimamia mfumo mzima wa Kambi na mafunzo hayo. Mafunzo ya JKT kwa vijana yahusishe pia mafunzo ya Stadi za Maisha na Stadi za Kazi ikiwemo ujasiriamali ili kuwawezesha vijana kujajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafunzo ya vitendo ndani ya Makambi, Kampuni tanzu ya SUMA JKT ya ujenzi ya *National Service ConstRuction Department* itumike kufanya kazi za vitendo kupitia kandarasi mbalimbali na kuwezesha JKT kupata mapato na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu 57, uwamuzi wa kisera kupeleka vikosi *DRC* pamoja na kujibu maswali yaliyohojiwa na Kambi ya Upinzani, naomaba Mheshimiwa Waziri arejee niliyohoji mwaka 2011/2012 kuhusu kashfa za ufisadi na silaha haramu katika maeneo ya vita ambavyo baadhi ya wanajeshi walituhumiwa.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa hotuba nzuri pamoja na kazi nzuri inayofanyika kutokana na Wizara hii hasa ulinzi na usalama wa Taifa letu, bila kuwasahau watendaji wote wa wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Wanajeshi wetu wastaafu waliopigana vita vya Uganda mwaka 1978/1979 ambao walifanya kazi nzuri sana. Wanajeshi hawa wamesahaulika hasa malipo ya mafao na pensheni. Kulingana na maelezo yao ni kwamba, Serikali ilitoa tamko kupitia vikao vya Bunge la bajeti la mwaka 2008 na 2009 kuwa Serikali ina mpango wa kuanza kuwalipa mafao na pensheni wapiganaji wote walioshiriki vita vya Kagera mwaka 1978/1979.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yake Waziri aliahidi kuwa Wizara yake itaanza kuwalipa mafao na pensheni hao wapiganaji. Hivyo, kupitia mchango huu Wanajeshi hawa wastaafu wakiwemo wa Jimbo la Busanda, Geita wangependa kujua ni lini mashujaa hawa wataanza

kulipwa mafao hayo na pensheni. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, suala hili lipatiwe ufafanuzi ili wananchi hawa wasikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA ABDULLA SAADALLA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza utendaji mzuri wa Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie *Mutual Defense Part ya EAC*; napendekeza makubaliano haya na mjadala wake uchukuliwe kwa uangalifu sana.

Tatizo ni kwamba, nchi za jirani (*EAC*) baadhi yao huwa na ajenda za kutumia vita au uvamizi wa nchi nyingine kwa maslahi ya kujiendesha kiuchumi. Mfano, Rwanda imebainika kuwa inatumika kwa kupitia nchi hiyo kama *transit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa madini hayo hasa hutokea Kongo (uthibitisho upo), lakini pili tuthamini uhusiano wetu na *SADC* kwani ni wakongwe na kusaidiana kwa hali na mali. Tatu, tujiepushe kama ni *political Shield* ya kutotengwa na Mataifa mengine juu ya kuongezeka kwa migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, operesheni ziwe na ukweli; Kuna operesheni nyingi na zenye gharama nyingi zinazofanywa na vikosi vyetu ndani ya *EAC*. Inasikitisha kuwa matukio makubwa na majanga ya uharamia, kuzama kwa meli, mafuriko makubwa na kadhalika. Hatujaona hata kidogo *involvement* ya *EAC* katika majanga haya. Kamwe hufika kutoka Afrika ya Kusini wakati jirani hawajihusishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za mkopo *against NHC*, nilipendekeza kuwa kwa makubaliano na *NHC* wanajeshi wapewe mikopo na kukatwa tangu wanapoanza kazi ili mwishowe wakati wa kustaafu iwe tayari wameshapata angalau nyumba za kukaa na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupenya kwa silaha kutoka nchi jirani na Maharamia; ulinzi uimarishwe bila ya woga kwani kuna mwelekeo wa kupenya silaha nzito na za kivita kutoka nchi jirani, pamoja na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa jinsi ilivyojikusisha na uokozi katika majanga yote. Pongezi kwa kuanzisha JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba, Kikosi cha kwenda DRC kiendeleo kwenda kulinda amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tudumisha *phenomena* ya *Geographical Shield* kama tulivyojipusha na *Al-Shabab* na kupeleka majeshi katika *AMISOM*. *Kenya is Geographically a shield* na pili tuendeleze kama iwezekanavyo kutumia *phenomena* ya *Political shield* kama tunavyotumia katika mahusiano yetu na Mataifa mengine ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa kazi nzuri inayofanywa ya kulinda nchi pamoja na raia wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kubwa kwa kurejesha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, kwa sababu mafunzo hayo yanawaimarisha vijana katika masuala muhimu yahasuyo maisha yao; kama ilivyoielezwa kwenye kitabu cha bajeti ya Wizara ukurasa wa 19 aya ya 32 kwamba JKT inaandaa vijana kuwa wazalendo, wenye maadili mema, moyo wa ujasiri, upendo wa mshikamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia kwa juhudi zinazofanyika katika kuhimiza Hifadhi ya Mazingira. Makambi yote ya Jeshi yameshiriki kikamilifu katika *programme* za kupanda miti, kusafisha Makambi ya Jeshi na



Jiji la Dar es Salaam. Naomba msaada zaidi wa kusafisha Jiji la Dar es Salaam ili kuliweka katika mandhali nzuri na kuvutia.

Mheshimiwa Naibu Spika, . Kwa kuwa mafunzo ya JKT yameanza rasmi, nashauri kianzishwe Kitengo cha Ushauri Nasaha ili vijana wenye matatizo wapate sehemu ya kupata ushauri hasa katika masuala yahasuyo usongo wa mawazo, mahusiano, maradhi na kadhalika. Baadhi ya vijana wanapatwa na matatizo makubwa na wanakuwa na hofu ya kueleza matatizo yao kutokana na mfumo wa JKT. Ni vyema Kitengo cha Ushauri Nasaha (*Counselling and Guidance*) kikaanzishwa ili kupata ushauri unapohitajika.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu naomba nijielekeze katika ukurasa wa 19, mafunzo ya Jeshi La Kujenga Taifa kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika Wizara hii nikiwa kama Askari mwenye no. AKC 4317 SG Ritta Kabati. Nianze na kuipongeza kwa kurudisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria. Kurudi kwa mafunzo haya ni imani yangu, sasa tunakwenda kurudisha yale maadili yaliyomomonyoka uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwa Serikali. Nimehudhuria mafunzo haya katika Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Msange, Kikosi 823 J.K Tabora, chini ya *Major* Mkarawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeamua kweli na tuna dhamira ya kweli ya kuwasaidia vijana wetu, ni vyema Serikali ikafanya uboreshaji wa Makambi haya ili vijana wetu tunaowapeleka pale kwa ajili ya mafunzo wasione kama mahabusu au kwenda kuwaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe uzoefu wa Kambi ya Msange. Kambi ile inahitaji umeme, hakuna gari la kikosi wala gari la kubebea wagonjwa, kunahitajika madawa ya kutosha hasa kutokana na idadi kubwa ya vijana waliopolekwa katika

kambi hiyo, miundombinu ya maji safi na maji taka. Kambi ile ilikuwa na vijana zaidi 1700, pia mabweni ni machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ni vyema Serikali ikafanya maboresho kwa askari wanaotoa mafunzo hayo. Iwapatie mikopo kwa ajili ya vyombo vya usafiri na nyumba za kuishi. Wakufunzi wengi wanaishi nje ya kambi, kuna umbali mkubwa kutoka wanapoishi na kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwepo na ulipukaji wa mabomu katika makambi kama vile, mlipuko ule wa Kambi ya Mbagala, mlipuko wa mabomu kambi ya ukonga na kadhalika. Naomba kupata tamko kuhusu yale makambi yaliyoko jirani na wananchi, je, wananchi wamevamia mipaka au makambi ndio yamevamia mipaka ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na mwingiliano huo ili kuwaondolea hofu wananchi walio karibu na Makambi kama Kambi ya Mbagala, Ukonga, Lugalo, Mwenge na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba naishauri Serikali kutokana na kazi nzuri inayofanywa na askari wetu wa Jeshi la kujenga Taifa kutumiwa na Wizara ya Ujenzi, bali kikosi hiki kitumike kujenga nyumba za Askari Polisi, Magereza na kadhalika ili kupunguza tatizo la makazi ya Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile ningeomba Serikali ijitahidi kufanya maboresho makubwa kwa maslahi ya askari wetu. Pia askari waliostaafu wapatiwe *special allowance* ya nyumba za kuishi tumeshuhudia wanajeshi wengi wanaostaafu wanaishi maisha ya shida sana wakati wamepigania nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mikakati iliyowekwa ni mizuri iwapo tu itatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu nayapeleka katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya JKT; kwanza niipongeze Serikali kurudisha utaratibu wa vijana wanaomaliza vyyo vikuu na kidato cha sita kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria. Hatua hii, nafikiri itasaidia sana kuwapa vijana wetu nidhamu, uwajibikaji na uzalendo kwa nchi yao na watakaowatumikia. Lakini niombe Serikali, muda wa sasa uliopangwa kulitumikia Jeshi (JKT) ama kwa mujibu wa Sheria, ama kwa kujitolea uongezwe ama urudi kama utaratibu wa miaka ya nyuma. Muda wa kulitumikia Jeshi uwe ama miezi tisa (9) au mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kuwachukua vijana wanaojiunga na Jeshi la wananchi, JWTZ, Jeshi la Magereza na majeshi mengine, napendekeza kwamba, badala ya kuwachukua vijana wapya kutoka mitaani, vijana walioko katika makambi ya JKT, ama vijana ambao tayari wameshamaliza mafunzo yao ya JKT, ndio wapewe kipaumbele kujiunga na JWTZ na majeshi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matrekta ya SUMA JKT, naomba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na sisi Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi, watusogezee huduma hiyo, kama ambavyo kwa Mikoa ya Kanda ya Kati, matrekta hayo yamesogezwa Dodoma. Pamoja na kuomba kusogezewa huduma hiyo, naomba masharti na taratibu za kupata mkopo wa matrekta hayo yalegezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho ya Hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, nitaomba anipe majibu, ni lini huduma hii ya matrekta ya SUMA JKT italetwa Kikosi cha Jeshi cha Nyumbu, Kibaha. Kwa miaka mingi, Kikosi cha Jeshi cha Nyumbu Kibaha kimeonesha uwezo wa

kiteknolojia katika vitengo mbalimbali kwa muda mrefu, ikiwa ni pamoja na kuunda magari na *machineries* mbalimbali. Kikosi hiki cha Nyumbu, ni vema kiongezewe pesa na kisimamiwe kikamilifu ili kiweze kutimiza ndoto na malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Shamsi Vuai Nahodha, Bwana Job Masima, Injinia Mussa Iyombe, Jenerali Davis Mwamunyange, Jenerali Samuel Ndomba, Meja Jenerali Muhuga, Meja Jenerali Dkt. Muzanila na Kanali Anselm Bahati; pamoja na Wakuu wote wa Idara na Vitengo vya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kujitosheleza kwa chakula ni jambo jema sana na lenye umuhimu mkubwa sana katika malengo ya kujitosheleza kwa chakula, pamoja na kuongeza mapato ya JKT. Ni wakati muafaka sasa JKT ikaandaa upya mkakati wa kuweza kufikia malengo haya. Ni imani yangu katika Bajeti hii eneo hili litapewa kipaumbele ili mpango huu uweze kuanza. Naipongeza Wizara kwa kuliona hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendana na wakati, ni vyema Sheria ya *The National Defense Act, 1966* ikafanyiwa mapitio ili kuona kama bado inakidhi mahitaji ya wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa majukumu na mipango mbalimbali iliyopo katika Wizara hii nashauri, uoperembaji na tathmini (*monitoring and evaluation*) ifanyike mara kwa mara kwa vipaumbele vinavyotekelezwa na Wizara hii ili kufikia malengo, lakini pia kwa kutumia kiasi hicho hicho cha fedha kinachotengwa ili kilete tija. Vile vile ni muhimu jukumu la *Risk Management* likajumuishwa ili kuhakikisha *Risk* mbalimbali zinazuiwa kabla hazijajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara kwa kupeleka wanajeshi wetu katika *peace keeping mission*

mbalimbali. Inasemekana mahitaji ni makubwa, hivyo basi, ni vyema Jeshi letu likapeleka wanajeshi wengi zaidi kwani ni njia ya kuwajengea uzoefu/mbinu mbalimbali wanajeshi wetu pamoja na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wataalam na hasa Makamanda wetu wakiongozwa na Jenerali Davis Mwamunyange akisaidiwa na Luteni Jenerali Samuel Ndomba kwa kufanya kazi nzuri ya ulinzi katika mazingira magumu ya ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kurejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Mafunzo haya ni muhimu katika kujenga nidhamu na uzalendo kwa vijana wetu ikiwa ni pamoja na Wabunge vijana. Nawaomba Makamanda wawe na programu nzuri ya kuhakikisha vijana hao wanapata mafunzo mazuri yenye *impact* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilishukuru Jeshi la Ulinzi kwa kuhakikisha mpaka wa Wilaya yangu ya Ngara na Burundi kuwa shwari baada ya chokocho za hapa na pale. Hata hivyo, wananchi wa Ngara hawajaelezwa juu ya hatima ya Askari wawili wa Jeshi la Ulinzi waliouawa, wananchi wawili wa Kijiji cha Mumilamila cha Wilaya na Ngara, wananchi ambao hawakuwa na hatia yoyote. Mauaji hayo yalifanyika mwaka 2011, mpaka sasa hatujui kesi hiyo iliishia wapi. Wanajeshi hao walikuwa wanalinda mpaka wa Burundi na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii ili Jeshi letu liwe na zana za kivita za kisasa, lengo likiwa ni kulifanya Jeshi letu liwe *deterrent* kwa adui yeyote kutoka nje. Inawezekana kukatokea kiongozi wa nchi jirani wa aina ya Idd Amini, hivyo *preparedness* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni matumizi mazuri ya wanajeshi katika kulijenga Taifa wakati wa hali ya usalama. Wanaweza wakatumika katika ujenzi wa madaraja, barabara na kadhalika. Jeshi pia liwe tayari kulisaidia Jeshi la Polisi pale Jeshi hili linapozidiwa katika kutunza amani ndani ya nchi. Mimi binafsi chokochoko za udini zinanitia wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi lisaidie kuimarisha Jeshi la Mgambo na kuwapa mafunzo ya kijeshi raia. Lengo la Baba wa Taifa lilikuwa ni kumfanya kila Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 kuwa katika hali ya kijeshi au Jeshi la akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupiga marufuku ununuzi wa samani kutoka nje ya nchi hasa Malaysia ni vizuri SUMA JKT ikajiimarisha katika kutengeneza samani zenye ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika ya Mzinga na Nyumbu ni mashirika yaliyoanzishwa na Baba wa Taifa kwa lengo la kuimarisha Jeshi letu ili liwe la kisasa. Shirika la Mzinga lina jukumu la kuzalisha mazao ya kijeshi, silaha mbalimbali, na kadhalika. Nyumbu lilianzishwa ili lifanye utafiti katika teknolojia za magari na lilianza kutengeneza magari ya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishiriki katika ku-*promote* Shirika hili la Nyumbu nilipokuwa Katibu wa *SCOPO (Presidential Standing Committee on Parastatal Organizations)* au Kamati ya Rais ya kusimamia Mashirika ya Umma kati ya mwaka 1986 – 1991. Natumaini kiwanda hiki kimeendelezwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ione umuhimu wa mashirika haya mawili ya Mzinga na Nyumbu katika uhai wa Jeshi letu na watoe Bajeti ya kutosha. Nafurahi kusikia kwamba Nyumbu wanafanya utafiti kuhusu *Engine* na *Gearbox* kwa ajili ya matumizi kwenye matrekta madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni maslahi ya Wanajeshi. Wanajeshi wetu wanastahili kupata maslahi mazuri na pensheni nzuri wanapostaafu kwani wanafanya

kazi nzuri ya kulinda mipaka yetu. Ni matumaini yangu kwamba, Wanajeshi wote wameshaingia mpango wa Bima ya Afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Bima hii itawasaidia sana pindi watakapostaafu. Bima hii ni kwa Askari na wenza wao mpaka kufa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wetu na Kenya upande wa Rombo ni mrefu sana, una njia ambazo sio rasmi zaidi ya 320. Hali hii inatoa mwanya kwa wahamiaji haramu na magendo kupitia katika mpaka huu. Nimekwishaarifu mara kadhaa kwamba, Wasomali na raia wa Eritrea hupita maeneo ya Tarakea na Holili na kuhifadhiwa na wenyeji na katika Mji wa Himo. Hali kadhalika baadhi ya Askari Polisi wasio waaminifu wamegeuza hali hii kuwa biashara. Natoa ushauri kwamba, Jeshi liangalie uwezekano wa kuweka Kikosi karibu kwa ajili ya kuangalia mpaka huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya Askari Mgambo ni mazuri, lakini wanaojunga wachujwe vizuri kwani baadhi yao wanapomaliza wanajiunga katika vikundi vya uhalifu, siasa na kuwanyanyasa wananchi kwa kujichukulia sheria mkononi. Hali hii inapelekea kudharaulika kwa Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo naipongeza Wizara, Jeshi pamoja na viongozi wake na naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hakika wote tunafahamu hali halisi, madhara na mmomonyoko wa maadili kwa baadhi ya vijana wetu kwa kukosa kujengewa uwezo au kupata mafunzo haya muhimu ambayo kimsingi yanajenga ari ya uzalendo, ukakamavu, uhodari na moyo wa kufanya kazi kulingana na mazingira uliyomo au majukumu uliyokabidhiwa na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kwa kumpongeza Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa

(JKT) na Wizara kwa ujumla kwa kukubali kurudisha mafunzo haya ambayo kwa miaka 19 sasa hayakuwepo. Jambo ambalo limeweka pengo kubwa la uwajibikaji kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumpongeza Kanali Rashid Aus Kanole, Mkuu wa Kikosi cha 835KJ Mgambo Tanga, pamoja na waandamizi wake katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku katika kufanikisha shughuli zote za Kikosi na malezi ya vijana hapo kikosini. Hakika nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naomba niongelee matatizo au changamoto zilizopo hapo kikosini 835KJ Mgambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri; hakika Kikosi hakina usafiri wa uhakika, maana Kikosi kina gari moja tu la Mkuu wa Kikosi ambalo limechoka, kiasi kwamba likiharibika shughuli za kituo zinakwama. Kikosi hakina gari la wagonjwa na gari kwa ajili ya shughuli nyingine za Kikosi; hii ni hatari kubwa sana maana kama gari hili likiharibika shughuli zote zinakwama. Naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuwapatia magari kwa ajili ya mahitaji tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri kwa maaskari kikosini; hakika hili ni tatizo kubwa sana. Kuna baadhi ya Askari wanaishi kilomita 16 toka kikosini na hawana usafiri wa kueleweka na hutumia pikipiki zao binafsi kiasi kwamba mvua inaponyesha shughuli zinakwama na hata wakati hamna mvua, maana watafika wamechafuka na hata hivyo ni gharama kubwa ya usafiri. Naomba Askari hawa wafikiriwe usafiri, wapewe gari la kuwachukua na kuwarudisha kazini ili wawe na morali ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi ya Askari; hakika makazi yao ni duni sana na wanahitaji kupewa nyumba nzuri kulingana na hadhi zao. Hakika hili ni hitaji la msingi sana. Serikali ifanye haraka kutekeleza zoezi la ujenzi wa nyumba za watumishi hawa mapema iwezekanavyo.



Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Askari; Serikali ifanye utaratibu wa kuboresha maslahi, mishahara na stahili nyinginezo za Askari. Hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu na hawana muda wa kufanya kazi za ziada za kuongeza kipato na kutunza familia ikiwa ni pamoja na wategemezi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa maji; hali ya upatikanaji wa maji kikosini hauridhishi, hakika maji yaliyopo ya Bwawa hayafai kwa matumizi ya binadamu, maana yanatumiwa na wanyama na muda wote yanatuama kiasi kwamba hata ukioga yanawasha sana. Wizara ifanye hima kuweka miundombinu ya maji kikosini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana wanapotoka mashambani kwa Msanga, Gendagenda na kadhalika, hakika wanahitaji kuoga na usafi mwingine kwa ujumla. Bila ya kufanya hivyo tutaongeza mlipuko wa magonjwa kikosini, mfano, kuhara na magonjwa ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uanzishwaji wa vyuo vya *VETA*; napenda kupendekeza kuwa kuwepo na uanzishwaji wa vyuo vya mafunzo ya ufundi na ujasiriamali. Hakika kuna vijana mara baada ya kumaliza mafunzo hawana sehemu ya kwenda mfano, baadhi watakwenda vyuo, baadhi wataajiriwa na je, hawa wasiokuwa na ujuzi mwingine wanafikiriajwe? Napendekeza kuwa ajira zote zifanyike kupitia vijana walioko Jeshini, kuna wataalam wa fani mbalimbali. Serikali iwatambue na kuwapa ajira hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia vyema utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali ya nchi ya ulinzi wa Taifa. Aidha, nampongeza sana Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Davis Mwamunyange kwa jitihada mbalimbali alizochukua kuhakikisha nchi yetu

ina Jeshi la kisasa, lenye weledi na uwezo mkubwa wa kulinda nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ningependa kutoa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria; je, awamu zilizopangwa kuanza baada ya Julai 2013 haitaathiri nafasi za vijana kujiunga na vyuo vya elimu ya juu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze kwa dhati kabisa uamuzi wa Serikali wa kurudisha tena mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria. Mafunzo haya yanatoa fursa kwa vijana kupata malezi mema ya kuwajengea uwezo na uzalendo. Wakati vijana 4,710 waliomaliza kidato cha sita mwaka 2013 wameanza mafunzo haya, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonesha kuwa vijana wengine waliobaki wataanza mafunzo kwa awamu tatu kuanzia mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipatiwe maelezo juu ya kama utekelezaji wa mpango huu hautaathiri ratiba/nafasi za vijana hawa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu ambapo vyuo vingi huanza muhula mwezi Agosti/Septemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu unyanyasaji wa kijinsia. Je, katika majeshi yetu kuna mikakati gani mahususi ya kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia hasa unyanyasaji dhidi ya wanawake hasa wasichana wanaojiunga na JKT?

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuwa majeshi yetu ni majeshi yenye nidhamu ya hali ya juu na yanayoheshimu haki, utu wa wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hatuwezi kukataa kuwa hakuna vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia. Kumekuwepo na hofu hasa kwa vijana waliojiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria juu ya uwepo wa vitendo hivi vya unyanyasaji dhidi ya wanawake. Mfano, mwezi Februari

mwaka 2013 nilipokuwa mgeni Rasmi wa mahafali ya kidato cha sita ya shule ya sekondari, vijana wa kike waliniomba rasmi nifikishe maombi yao kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika na JKT kuhakikisha hawatakumbana na vitendo vyovyote vya unyanyasaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya kuwatoa wasiwasi vijana wote wa kike/wasichana walioko JKT na wanaotarajia kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria kuwa Jeshi halivumilii vitendo vya aina yoyote vinavyodhalilisha wanawake.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa kuboresha shughuli zake za kazi za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi kuongeza madawa na shughuli nyingine za tiba katika Hospitali zake zote za Jeshi kwani Hospitali hizi zinasaidia sana kutibu Wanajeshi lakini pia raia wengi wanaozizunguka Hospitali hizi hasa wanawake na watoto wanapata huduma na mara nyingi kunakuwepo upungufu wa madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Ulinzi kurudisha utaratibu wa kununua mavazi kwa Wanajeshi waliopo kazini. Kumejitokeza tabia ya wanajeshi kujinunulia nguo wenyewe hasa viatu kutokana na upungufu wa bidhaa hiyo wanapohitaji kutoka sehemu zao za kazi. Inapelekea kuvaa viatu wanavyonunua kwenye mitumba au viatu vya raba vyenye bei rahisi ambavyo havilingani na hadhi ya Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuboresha miundombinu ya kuweka umeme katika Makambi ya Jeshi hasa Bulombola, Kigoma ambayo muda wote wanatumia jenereta linalowashwa kwa baadhi ya muda ukizingatia kambi hii ipo mpakani, ni hatari kwa maisha ya vijana na wanajeshi waliopo kambini hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iharakishe upimaji wa maeneo ya Jeshi hasa Chukwani, Kiembesamaki ambapo Jeshi limechukuwa eneo la wananchi na eneo wanalodai lao bado hawajawalipa wananchi wa eneo hilo ambapo kumesababisha ugomvi mkubwa baina ya raia na wanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bajeti ya Wizara; Jeshi letu limekuwa na uzalendo mkubwa kwa nchi yao. Kwa sababu hiyo, pamoja na uzalendo walio nao kwa nchi yao inabidi Serikali kuangalia upya Bajeti yake ili waweze kukabiliana na changamoto zinazowakabili. Zipo changamoto zinazohitaji utatuzi wa haraka, kama kupunguza idadi ya wanajeshi wanaoishi uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara nyingi imesikika mizozo kati ya wananchi na Wanajeshi, lakini pia kuwepo na baadhi ya Wanajeshi kutumiwa kwa kujihusisha na vitendo vya ujambazi, nashauri Wanajeshi kuishi kambini ili kujiepusha na vitendo kama hivyo nilivyovianisha hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, lakini pia na timu yake yote iliyoshiriki kuandaa kwa umakini mkubwa taarifa hii, lakini pia kwa kazi yao kubwa wanayoifanya kila siku usiku na mchana kuhakikisha wananchi na mali zao wako katika hali ya usalama kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya usalama wa mipaka katika mwaka 2013/2014; kuhusu mpaka wa Magharibi; natoa rai yangu kuwa pamoja na hali kuwa shwari katika mpaka huu wenye urefu wa kilomita 1,220 ambako

Tanzania inapakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ni vizuri Wizara hii wakishirikiana na Wizara dada ya Mambo ya Ndani ya Nchi washirikiane kuwapa vitendea kazi Askari Polisi na wa Uhamiaji walioko katika vituo vya mpakani kama kituo cha Kasanga, Kirando, Kasesya, Mozi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi hivyo ni kama vile, magari, boti kwa ajili ya doria, bunduki na risasi kwa ajili ya ulinzi (*prevention is better than cure*), tuisubiri mpaka mauaji au maafa kwa Watanzania walioko mipakani yatokee ndio tushtuke tukaanza kuwa-*equip* na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkakati wa kupambana na UKIMWI; niipongeze Wizara kwa kuwa na mkakati huu muhimu. Niipongeze Wizara kwa kuendelea kuelimisha juu ya watumishi wake kujikinga na maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI kwa kuendelea kuhimiza upimaji wa hiari kwa maafisa, Askari na watumishi wa umma. Natoa rai yangu kuwa, Askari na familia zao wasipewe dawa tu ila wapewe na chakula-lishe ili wanapojitibu na miili yao iendelee kujengeka kwa lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Armery/Strong Rooms*; Wizara hii na Wizara dada ya Mambo ya Ndani washirikiane kujenga hizo *Strong Rooms/Armery* kwa ajili ya kuhifadhi/kutunza silaha, kwani kutokuwepo kwa *Armery* hizi kumesababisha Askari hao kutopewa silaha kwa sababu silaha haziwezi kuwekwa kiholela tu. Hivyo basi, kwa kuwa ulinzi ni pamoja na silaha, *Armery* zijengwe katika mwaka huu wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi na stahili nyingine; Wanajeshi na Askari ni watumishi wenye kufanya kazi kwa umakini na uadilifu na kwa moyo wa uzalendo, hivyo basi wanayo haki ya msingi ya kupewa makazi/nyumba zenye hadhi, nyumba bora, lakini pia wapewe mishahara mizuri ili wakopesheke na wapewe posho wanazostahili kama watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano ya simu; mawasiliano ya simu ni muhimu, mtandao mpaka wa Magharibi na Kusini yaimarishwe ili ulinzi uimarike ili kusiwe na kushindwa kwa hatua za dharura kuchukuliwa matatizo yanapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu urejeshwaji JKT; napenda kuishukuru Serikali kwa kurejesha tena JKT ili vijana wetu wawe na uzalendo na utiifu. Napenda kushauri kwamba, ni vema muda wa kujifunza JKT ukaongezeka. Pia vijana wanapopitia JKT ni vema wakapata ajira na vile vile wale wanaojitolea ni vema wakatumika katika shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato ikiwa ni pamoja na kupata ajira Jeshini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaohitimu JKT kwa kujitolea ni vema sasa Serikali kupitia Wizara hii ikaangalia upya namna ya kuanzisha Kikosi Maalum kitakachojishughulisha na shughuli za ujenzi, kilimo na ufugaji wa mifugo pamoja na ufundi ili kutoa nafasi za ajira kwa vijana hao badala ya kuwaacha na kurudi uraiani kukaa bure na hivyo kusababisha vijana kujiunga katika shughuli zisizo halali kama uzururaji na ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za ujenzi zinaweza zikawafanya vijana hawa wakaweza kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi na hata pia kushiriki katika ujenzi kama wa nyumba za Walimu na mengineyo, hivyo ni bora kukaanzishwa Kitengo Maalum ndani ya JKT kama ilivyo SUMA JKT. Hivyo basi, vijana hawa wakatumika badala ya kutumia Wakandarasi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii ni vema sasa ikarudia utaratibu wake wa kuwachuja vijana kuwapeleka katika majeshi mengine kama Polisi, Uhamiaji

kwa mafunzo zaidi badala kama ilivyo sasa kwa utaratibu wa Polisi kutangaza nafasi za kujiunga na Jeshi hilo. Yaani waajiriwa wa Majeshi mengine kama Polisi wachukuliwe wale waliopitia JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ikumbuke wajibu wake wa kuwakumbusha mara kwa mara Askari wake kuhusu mambo ya nidhamu, heshima na uzalendo ili kudumisha amani na mahusiano mema na jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za makazi na makazi ya majeshi kambini; ni kipindi kirefu kambi zetu za Jeshi zimekuwa na makazi makongwe au majengo ya mabanda ya kurithi. Hivyo, ili kuweza kuwafanya Wanajeshi wetu wafanye kazi kwa bidii, naomba Wizara itengeneze majengo ya kambi ya Jeshi ya Mwananyanya, Zanzibar, majengo ambayo ni makongwe na hayafanani na Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kambi hiyo kwa kipindi kirefu haina uzio, ambapo ni hatari hasa ikizingatiwa kwamba iko katikati ya wananchi. Pia kambi hiyo imekosa miundombinu ya maji, pamoja ubovu wa barabara. Hivyo, naiomba Wizara kutoa msukumo wa makusudi ili kuinusuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kambi hiyo ya Mwananyanya, kuna *Dispensary* ambayo pia inawahudumia wananchi wa maeneo hayo. Kwa masikitiko kituo hicho, hakina vifaa, hakina dawa, pamoja na upungufu wa Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara kutoa msukumo wa kukipatia vifaa husika kituo hicho, aidha, nauomba uongozi wa Wizara kufanya ziara ya makusudi katika kambi hiyo.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mshikamano kati ya Makamanda na wapiganaji JWTZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Tanzania na Malawi ni hali tete sana. Raia wanakaa kwa wasiwasi wakati wote. Ingawa hatutaki vita itokee, lakini tahadhari ni muhimu sana kwa kupeleka *detachment* za lori mbili kule mpakani mwa Ziwa Nyasa. Aidha, ni vema kuimarisha madaraja ya kijeshi yaliyoko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mishahara ya wanajeshi wote JWTZ, Makamanda na wapiganaji ni kidogo. Nashauri mishahara, marupurupu na posho zao za chakula ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana kwa JWTZ kupata masomo ya uraia ili kujenga uzalendo wa kuilinda nchi yao. Mafunzo hayo kwa sasa hayapo.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi Tanzania limekuwa likifanya kazi nzuri sana ya kulinda usalama nje na ndani ya nchi yetu. Kumekuwa na utataribu mzuri sana wa kuwapatia Wanajeshi wetu fedha kwa ajili ya chakula. Utaratibu huu umekuwa mwiba mkali kwani baadhi ya Wakuu wa Vikosi wamehujumu jambo hili kwa kuwalazimisha wanajeshi hawa kula kwa wazabuni ambao huuza vyakula hivyo kwa bei ya juu sana. Huku ni kuingilia uhuru wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikosi vya *Land Force* na Kibaha KJ 36 majengo yake ni mabovu sana na yanahatarisha hali ya vijana hao. Tunashauri Serikali iyakarabati au kujenga upya majengo hayo ili kunusuru hali yake. Haiwezekani Wanajeshi wanaolinda amani na usalama wetu, waishi maeneo yasiyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kurudisha mafunzo ya JKT nchini. Pamoja na wazo hili zuri inashangaza sana viongozi wakiwa wanatumia wiki tatu



tu kukamilisha mafunzo hayo! Jambo la kujiuliza wiki tatu zinasaidia nini au zinambadilishaje mtu huyu? Lengo la JKT ni nini na iweje aliyefunzwa wiki tatu alingane na wa miezi mitatu na sita au mwaka mmoja kwa kupata cheti kimoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza kuona Wanajeshi wetu wenye utaalum mkubwa wa kihandisi, ujenzi na kadhalika hawapati zabuni na matokeo yake wanapewa watu wasio na utaalum na kwa gharama kubwa. Hivyo, Serikali iandae utaratibu wa kuwapatia zabuni hizo kwani ni wazalendo wa nchi hii.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samani zinazotengezwa na Majeshi, Jeshi la Kujenga Taifa limekuwa likitengeneza samani zenye viwango na imara na zinatengenezwa kwa mbao za hapa nchini na ni za uasilia kuliko zile zinazotoka China, zinazotengenezwa kwa vumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, samani kutoka China kwa mfano hata hapa ndani ya Bunge lako Tukufu viti na meza humu ndani hata miaka kumi bado kuvitumia tayari vimeanza kubomoka na kupasuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, ni vizuri iandaliwe sera ya kuyaagiza Mashirika yote ya umma, ofisi zote za umma kwa kuanzia *order* zote za samani zipelekwe Jeshi la Kujenga Taifa ili wao wazitengeneze na hili litalisaidia Jeshi hili kwa mapato na tutakuwa tunatumia vitu vinavyotengenezwa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji wa mbegu bora; hapa nchini pamekuwepo na tatizo la upatikanaji wa mbegu bora. Wakulima wamekuwa wakipata kununua mbegu nyingi zinazozalishwa nje ya nchi na hapo hupelekea mbegu nyingi kuwa hazikidhi viwango. Lakini SUMA-JKT wanazalisha mbegu, lakini mbegu hizi hazitoshelezi kwa kuwa *project* hii inahitaji mtaji mkubwa. Hili ni suala muhimu sana ukizingatia asilimia themanini ya Watanzania wengi wapo vijijini na wengi wao ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, Kambi Rasmi ilishauri Serikali kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, mfano, ununuzi wa magari ya Kiserikali na badala yake fedha hizi zielekezwe SUMA-JKT na fedha wanazozomba kwa ajili ya maendeleo wapewe zote ili waweze kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Wanajeshi; ni ukweli usiopingika kwa sasa hivi maisha yanapanda sana, gharama za kila kitu ni za juu. Wastaafu hawa walilitumikia Jeshi hili kwa utii na uaminifu mkubwa, hivyo basi, wanastahili kutunzwa na Serikali yao na kulipwa kulingana na gharama halisi za sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mikakati gani ya kuboresha maslahi haya tukumbuke sote hatubaki vijana milele, kuna siku itafikia na sisi sote tutastaafu, hivyo, tuwatendee haki wastaafu hawa.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa hotuba nzuri na zaidi kwa kazi nzuri unayofanya, wewe binafsi na Wizara yako yote. Aidha, nampongeza Mkuu wa Majeshi na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri pamoja na changamoto nyingi. Hata hivyo, ninayo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingine zote masuala yote ya ulinzi na usalama yanajadiliwa kwenye *level* ya Kamati ya Bunge tu na si Bungeni kama hivi kwenye mijadala ya wazi. Mheshimiwa Waziri anaonaje akaleta hoja hiyo kuanzia mwaka ujao wa fedha tuanze utaratibu huo, iishie kwenye *level* ya Kamati. Hapa tunajianika pasipo sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kuanza upya mafunzo ya JKT, suala linalonisumbua ni kwamba, hawa vijana wamalizapo hayo mafunzo wanakwenda wapi? Hilo soko dogo la walinzi haliwezi ku-*accommodate* wote hata makampuni binafsi wakiwachukua bado hawatakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni mikakati gani tuliyonayo kuwapa *skills* mbalimbali na mitaji hata kama ni mikopo kukidhi majukumu au maisha mbele yao? Tusije tukawa tunazalisha majambazi. Naomba majibu hata ikibidi yale mabilioni ya JK yaelekezwe kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Jeshi la Wananchi au Ulinzi unazidi kila siku hapa nchini kwetu. Hali inavyokwenda inabidi mtu mwenye busara aone umuhimu wa kuwepo Jeshi hili. Amani iliyokuwepo inazidi kupungua, hivyo basi, ni muhimu kabisa fedha zinazotakiwa katika maeneo mbalimbali ya Wizara zitolewe tena kwa wakati kama Chuo cha Ulinzi, maslahi ya wanajeshi, vifaa na kadhalika vitolewe. Mheshimiwa Waziri aendelee kuisukuma Serikali kupitia *Cabinet*, nasi tutasukuma zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho suala la Sera ya Ulinzi, kwa sababu imekwamia Zanzibar na Mheshimiwa Waziri kama aliwahi kuwa kiongozi wa juu, tunaomba sasa suala hili alipe kipaumbele lifike mwisho kabla ya Bunge la Katiba, kwani likiachwa litawapa nguvu wasiotaka Serikali mbili na limo chini ya uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera kwa uwasilishaji mzuri wa Makadirio ya Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Upinzani sio *critical*, wamekosa la kusema ndio maana wanatapatapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri naomba asahihishe suala la kilomita 36 ya maji kwenye Ziwa Nyasa (ibara 13), nadhani ni zaidi ya hizo. Naomba masahihisho yafanyike wakati wa majumuisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Hotuba iliyotolewa na Kambi ya Upinzani. Ninaiomba Serikali itafakari Hotuba hiyo na kuifanyia kazi, kwani lengo ni kujenga na si kunyoosheana vidole.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali maboresho yote na mahitaji yaliyoainishwa katika Hotuba ya Wizara hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, yazingatiwe kwa ajili ya ustawi wa Jeshi au Majeshi yetu. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yafanyiwe kazi na si kwa mazoea bali kwa kumaanisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna askari waliostaafu, kuachishwa kazi au kuugua, wanadai mafao yao. Serikali iwaone watu hawa, iwapatie haki zao, kwani madai mengine ni ya muda mrefu na yanalitia doa Jeshi letu mbele ya jamii. Mwanajeshi kukaa analalamika haiteti afya, watu hawa tukumbuke mchango wao, wapewe stahili zao, kama hawastahili basi wajibiwe barua zao za malalamiko zilizoko Wizarani ama maeneo waliyokuwa wakihudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wakati mwingine waache fujo na kutumia ubabe katika jamii maeneo mbalimbali hususan Dar es Salaam, tukio la Kawe hivi karibuni, ni aibu kwa Majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Kwa kuwa ulinzi wa nchi yetu unategemea Jeshi la Kujenga Taifa, Wanajeshi wanastahili kupewa heshima kubwa kwa kazi yao ngumu na ni ya muhimu katika ulinzi wa nchi yetu. Napendekeza kuwa vijana wote wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa baada ya kumaliza Mafunzo yao ya JKT, waweze kuajiriwa katika Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa, PCB, JWT, Bandarini na sehemu zote za ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wapewe Mafunzo ya VETA. Jeshi lipewe *tenderya* kujenga Barabara na Nyumba za Serikali. Wanajeshi walipwe Pensheni yao kwa wakati

siyo kucheleweshwa. Waongezewe Pensheni yao kwa wakati na yongeza zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kuzalisha mali iboreshwe katika Majeshi yetu. Vyuo vya ufundi vijengwe katika Majeshi yetu na wapewe nafasi ya kutoa Shahada ya juu (*Degree* na *Masters*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi – Jenerali Davis Mwamunyange, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye lengo la kuimarisha ulinzi wa nchi pamoja na kuwaandaa vijana kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kuwaandalia Wanajeshi wetu mazingira mazuri ya kazi, bado kuna tatizo kubwa la nyumba za kuishi kwani wengi wao wanaishi nyumba za kukodi uraiani; mfano, Kambi ya Jeshi lhumwa wanaishi Dodoma Mjini au lhumwa huko huko uraiani, jambo ambalo siyo zuri sana kwani ni rahisi kupata vishawishi vya kujihusisha na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni namna gani Serikali imejipanga kuwaondolea adha hii Wanajeshi wetu kwa kuwajengea nyumba za kuishi kwenye Kambi zote za Jeshi ikiwemo Kambi za Dar es Salaam. Nasubiri maelezo ya Serikali kwani zimetajwa idadi tu hatujui mgawo wake kwa kila Kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni muda mrefu sasa tangu Serikali itoe taarifa ya kujenga Kambi za Jeshi Manyoni na Iramba, bali haijulikani kinachoendelea na sijaona fedha zilizotengwa kwa kuanza ujenzi wa Kambi hizi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo Wananchi

wa maeneo hayo wafahamu waweze kutoa ushirikiano pamoja na kuishukuru Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali ya CCM kwa kazi yake nzuri ya kuwapeleka vijana Jeshi la Kujenga Taifa kwani hufundishwa mambo mbalimbali kwa ajili ya kulinda nchi hii. Tatizo ni pale vijana wanapomaliza mafunzo, wachache huajiriwa na wengi hurudi vijijini kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi ni kwamba, kwa vile vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa hutegemea kupata ajira kumbe inakuwa sivyoyote, ni vyema Serikali iangalie uwezekano wa kuajiriwa au kuwaandalia mazingira ya kujiari wanaporudi vijijini kwa kuwapa ufundi na fedha za kununulia vifaa. Kikubwa zaidi, ajira zote Serikalini mfano Mashirika ya Serikali, Taasisi za Serikali au Serikali Kuu, ni vyema wapewe kipaumbele hawa vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, Wanajeshi ni watu *special* kulingana na unyeti wa kazi zao; hivyo, siyo vizuri anapostaafu kucheleweshewa malipo yao ya pensheni, kwa kuwa wamejifunza mengi mazito, wakitugeuka tumeumia. Hivyo, ni vyema mara wanapong'atuka walipwe haki zao ili tusiwape nafasi ya kuingia kwenye vitendo viovu; ni vyema Serikali itoe maelezo kwani hata sasa wapo Wanajeshi bado wanaidai Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la Wanajeshi kuchelewa kupandishwa vyeo wakati sifa wanakuwa nazo. Ninaomba Serikali yangu itende haki kwa Wanajeshi wote. Hii itasaidia Wanajeshi kuwa na moyo wa Uzalendo kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipunguze vigezo vya kujiunga na Jeshi. Vijana wengi wanapenda kujiunga na Mafunzo ya Jeshi, lakini wanapoingia kwenye usaili wanaachwa kwa vile ni wafupi au wana michoro kwenye miili yao, ambayo walijichora wakati wa utoto bila kujua madhara yake. Ninaomba Serikali ichukue maombi yangu

na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, atoe maelezo ya kupunguza masharti ya kujiunga na Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho mbalimbali za Wanajeshi kuna tatizo la wanajeshi kutokulipwa posho zao kwa wakati au kutokulipwa ipasavyo. Ninaiomba Serikali suala hili kulipa kipaumbele ili vijana wasisononeke au kupunguza ari ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa kwenye Kambi za Jeshi na JKT zinatengeneza samani nzuri sana. Ninashangaa Serikali bado inaendelea kuagiza samani za ofisi mbalimbali kutoka nje ya nchi na bei zake ziko juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema hivi sasa samani zote za Serikali zitengenezwe kwenye Kambi zetu za Majeshi ya Wananchi au JKT ili kuinua mafungu ya Kambi zetu na kupunguza matumizi mabovu ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii na kuwatakia utekelezaji wenye tija.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kurudisha JKT kwa vijana. Naiomba Serikali iongeze muda zaidi wa mafunzo hayo kwa miezi sita au mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kwamba, kwa kuwa Mafunzo ya JKT ni muhimu sana kwa Taifa letu kwani yanaleta uzalendo kwa kiasi cha juu sana; hivyo, mafunzo hayo yangepewa kwa makundi mbalimbali. Watumishi wa Umma wangepewa mafunzo maalum kwa wale wote ambao hawakupitia mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la vijana ambao wangepewa mafunzo maalum kwa ajili ya utii, uaminifu na uhodari na pia kwa kuwa vijana wengi hawana ajira, hivyo ni muhimu sana kupewa mafunzo ya ufundi kwenye Sekta mbalimbali ili watoke na ujuzi maalum na kuweza kujijari au

kuajiriwa. Vilevile Makambi yetu yana maeneo makubwa sana kwa ajili ya kilimo, sasa ni wakati mwafaka kuyatumia maeneo hayo kwa ajili ya kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa Serikali ilitenga maeneo makubwa sana kwa ajili ya Jeshi la Wananchi, maeneo haya sehemu kubwa nchini ni mapori makubwa; ni wazo zuri lakini pia lina madhara yake; kwa mfano, katikati ya Morogoro na Chalinze kuna eneo la Jeshi maeneo ya Mwidu, eneo hilo ni hatari sana nyakati za usiku. Huo ndiyo msitu wa majambazi, magari mengi sana yanatekwa maeneo hayo na kupigwa na kuporwa mali zao. Mheshimiwa Waziri cha kusikitisha kuliko yote eneo hili ni la Jeshi; je, majambazi haya yanatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe ni mwathirika, niliwahi kukumbana na majambazi hao, ilikuwa usiku wa saa tisa. Kilichosaidia, tulitekwa magari mengi hivyo tukaweza kujiokoa na askari kila tulivyowapigia hawakufika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba maeneo haya yafanyiwe kazi hasa kwenye barabara kuu kwa ajili ya usalama wa raia na mali zao.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha bajeti nzuri, japo naomba ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Kwanza, niliwahi mara kadhaa hapa Bungeni wakati wa maswali na mijadala ya bajeti, kuitaka Serikali kuondosha JWTZ wanaofanya mazoezi ndani ya Kijiji cha Bunere. Kuna mabaki ya mabomu ambayo yamewahi kuleta madhara kwa Wananchi. Naomba maelezo lini eneo hilo litaachwa kwa ajili ya kijiji hicho?

Pili, bado kuna watu wanaovaa nguo za mitumba zinazofanana na Sare za JWTZ; ni mikakati gani iliyopo kudhibiti hali hii?



Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ndiyo yenye dhamana ya kulinda mipaka ya nchi, ni wazi kwamba, chombo hiki kinahitaji zana za kisasa za kiulinzi ili kuweza kukabiliana na majangili na wahamiaji haramu wanaoingia nchini kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda ieleweke kwamba, idadi kubwa ya wahamiaji haramu wanaoingia nchini huwa wanaingia na silaha kali na za kisasa na miongoni mwao ndiyo wanaosababisha uvamizi wa baadhi ya maeneo, uwaji wa wanyama ambao ni Maliasili ya Taifa na hata kusababisha ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi ni Askari ambao wanapaswa kutunzwa vizuri kwa kuboreshewa mishahara na posho zao ili waweze kujenga weledi katika kufanya kazi zao na kuwaondolea wasiwasi juu ya kuziweka familia zao katika hali ya afya na amani. Ni wazi kwamba, Wanajeshi wetu ni watu wastaarabu, wavumilivu na washiriki wakubwa katika operesheni mbalimbali ndani na nje ya nchi. Wameshiriki katika ukombozi wa nchi mbalimbali za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba, suala la mipaka baina ya Tanzania na Malawi limekuwa na utata hasa baada ya Malawi kukataa kupatikana kwa suluhu ya mipaka baina ya Tanzania na Malawi. Serikali ina wajibu wa kutoa ufafanuzi katika Bunge hili na kwa Watanzania kwa ujumla, juu ya utata huu kwani waathirika wakubwa watakuwa ni ndugu zetu wa Tanzania ambao wako karibu na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haipaswi kuwatumia Wanajeshi kama manokoa wasiokuwa na maana. Naikataa kauli ya Baba wa Taifa aliyoitoa kwa Wanajeshi waliopigana Vita vya Uganda kwa kumng'oa madarakani aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Iddi Amin, alipowaambia Wanajeshi wetu

wamepigana na wameshinda; hata hivyo, hatuna cha kuwalipa isipokuwa malipo yao ni ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ni haki ya kupewa kiumbe chochote, lakini kunahitaji uangalizi wa mazingira gani ya kutolewa ahsante hiyo. Hivyo, kuna haja ya Serikali kuliangalia suala hili kulingana na hali halisi.

Vilevile ni vyema Serikali ikawapatia chochote wale walioathirika na vita vile na kwa wale walio poteza maisha wafidiwe watoto na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, JKT ni chombo ambacho kinaweza kikatoa wataalamu wa aina mbalimbali ambao wanaweza kutoa ajira za aina mbalimbali na kuendesha maisha kwa ufanisi zaidi badala ya vijana walio wengi kukaa vijiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa Wanajeshi wamejitoa katika uwanja wa siasa hivyo wametoa matumaini makubwa kwa Watanzania kwamba wao ni walinzi wa nchi na mipaka ya nchi na vilevile ni walinzi wa amani. Ninatumaini ya kwamba, chombo hiki kina haki na wajibu wa kupewa kila stahiki zao ambazo zitaweza kulinda afya zao, usalama wao na kujenga nchi yao.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi kule Zanzibar ni muhimu sana litafutiwe ufumbuzi ili tuondokane na matatizo baina ya Wananchi na JWTZ katika suala zima la ardhi. Wastaafu waandaliwe vyema haki zao ili wanapostaafu *cheque* zao ziwe tayari, waondoke nazo pamoja na haki zao nyingine zote.

Askari wastaafu wapewe posho au kwa jina lingine *pension* nzuri kidogo ili waweze kujikimu, kwani hali zao siyo nzuri kimaisha, posho ya chakula iongezeke kutoka shilingi 7,500 na kufikia shilingi 10,000 kwani bei ya chakula ni ghali.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mpango wa kuboresha Hospitali ya Jeshi la Lugalo kuwa Hospitali ya Rufaa, lakini katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna mahali popote panapotaja au fedha iliyotengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Je, Serikali inasema nini kuhusu mpango huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo mara chache na matukio ya mahusiano mabaya kati ya Askari na Wananchi na kusababisha mapigano kati ya Wanajeshi na raia. Kwa mfano, Mbalizi ambako yalitokea mapigano na Mwananchi mmoja kuuwawa. Je, Serikali inasema nini juu ya suala hili? Je, kuna haja ya elimu kutolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Wanajeshi ambao wanatoa malalamiko yao kuhusu kuchelewesha mafao yao; je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ambayo imeniwezesha kutoa hayo machache ambayo bila shaka Mheshimiwa Waziri atayafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi linafanya kazi nzuri ya ulinzi wa mipaka yetu, lakini bado yapo matatizo katika Mkoa wa Kigoma. Wavamizi ni wengi kutoka katika nchi jirani za Congo DRC na Burundi, wanasumbua wavuvi, haupiti mwezi bila wavuvi kutekwa na kuibiwa vifaa vyao na mara kadhaa wanauwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama katika mipaka ya Ziwa Tanganyika uimarishwe, Wananchi wajengewe uwezo wa utambuzi kwani bila elimu hiyo wageni wengi wataendelea kuvamia na kuingia ndani ya mipaka yetu. Kutokana na ufinyu wa bajeti, inatokea mara nyingi Halmashauri zinatakiwa kuchangia pesa za mafuta ya mashine za boti kusaidia vyombo vya usalama kulinda mipaka yetu. Mara nyingi uvamizi unapozidi ndipo kero hiyo

ya kuchangia mafuta inapozikumba Halmashauri zetu ingawa hazina bajeti hiyo.

Ufinyu wa bajeti umesababisha maeneo ya Kagunga, Kasulu, Igalula, Sibwesa Biharo na Magamba, hali si shwari, Wanajeshi wamepunguzwa na ipo taarifa kuwa wengi watapelekwa Sibwesa Igalula. Nashauri wasiondolewe katika mipaka hiyo ili ulinzi uzidi kuimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi na ni muhimu; Vikosi vya Usalama (Jeshi) viwezeshe hasa Mikoa ya mipakani, vipewe *spacia*/bajeti ili ulinzi uimarike, hasa Mkoa wa Kigoma. Kwa mfano, pale Kagunga, mtambo wa rada mara nyingi unazimwa kwa kuwa jenereta haliwashwi hawana mafuta, kwani eneo hili halina umeme. Hii ni hatari, Serikali iangalie upya upangaji wa bajeti ili izingatie Mikoa yenye mipaka hasa Kigoma ambayo inapakana na nchi nyingi tena ambazo hazina usalama wa kutosha kama DRC Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; napongeza juhudi za Serikali kuamua Jeshi lizalishe kwa ajili ya Jeshi lenyewe ili kupunguza gharama za kulisha Majeshi yetu.

Nashauri Serikali ihakikishe inatumia bajeti yake binafsi kwani hiyo kazi ya kilimo tukitegemea wawekezaji washirikiane na Jeshi, tutapoteza muda mwingi wa kusubiri wawekezaji na wasipojitokeza mpango wa kilimo utakwama. Hivyo, tutumie pesa zetu za ndani, kwani baada ya Jeshi kuzalisha, wataweza kuzalisha na ziada ili wawauzie Wananchi na wanaweza kusafirisha nchi nzima na nje ya nchi ili wajipatie fedha za Kigeni. Inawezekana kama tutaamua na ninaamini Serikali inaweza kupata fedha za ndani kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya Wanajeshi ni duni hasa Kambi ya Burombola, Rwamkoma na Nachingwea. Pia Makambi yote ya Tanzania hali ya makazi ni duni na Askari Jeshi wengi wanaishi uraiani. Hii siyo hali nzuri. Serikali iongeze juhudi ya kupata fedha za ujenzi wa nyumba bora za Wanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya Wanajeshi ni midogo yaongezwe na yasicheleweshwe, manung'uniko ni mengi mno. Wanaohamishwa na wanaostaafu walipwe stahili zao kwa wakati.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mfumo wa ulinzi kwenye Bahari Kuu ni la kimkakati. Ninashauri suala hili lipewe kipaumbele sana, uwekezaji huu utalifaidisha sana Taifa. Tusione tabu kutumia pesa sana. Sekta ya Mafuta na Gesi tusipokuwa makini tutakuwa Nigeria. *I think we must give top priority to our Navy now now. This is the time to do it.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge tupewe nafasi kujiunga *Defence College*. Mimi binafsi napenda kujiunga mwaka huu ili niweze kuandika kuhusu *International Taxation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza na *NSSF* kuhusu suala la *VETA*, wapo tayari kushirikiana na *SUMA JKT* na *VETA* ili kuanzisha vyuo. Tuanze na *Mgambo* mwaka huu kama *pilot*. Ikiwezekana tufanye kikao cha pamoja kati ya *VETA*, *SUMA JKT*, *NSSF*, Mheshimiwa Waziri na *PAC Chair*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba, Wanajeshi waingizwe kwenye Mfuko mmoja wa Pensheni; kwa mfano, *PSPF* ili tuweke utaratibu wa askari kukopeshwa nyumba kujiandaa na kustaafu. Mfumo wa hivi sasa siyo *sustainable* kwenye Pensheni.

Pili, tuhuishe mfumo wa Pensheni kati ya *Pre 1997* na *Post 1997*. Tulipe sawa Pensheni ya *general* waliostaafu zamani na wanaostaafu sasa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri wanayoifanya Wanajeshi wetu kulinda nchi yetu usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni moja ya nchi zilizosaini na kuridhia kushiriki katika maamuzi yatolewayo na Baraza la Umoja wa Mataifa kuleta Amani na kulinda

Wananchi wasio na hatia popote Duniani tunapopewa jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kwenda DRC tumepewa na Umoja wa Mataifa chini ya Azimio lake Na. 2098 na tunaenda kulitekeleza na maamuzi yalishafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea Kikundi cha M23 kingeshawishi Baraza la Umoja wa Mataifa wakati wa majadiliano kabla ya uamuzi huu wa Azimio Na. 2098 kufikiwa. Hivyo, M 23 watambue Tanzania na nchi washirika wanaenda kutimiza wajibu wa jukumu waliopewa na Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Sasa wasitutishe kwa kuwa sisi ni nchi tunayosumbuka sana na wakimbizi na uvunjwaji wa haki za binadamu wanaofanyiwa na Wananchi wa DRC kwa tamaa ya vikundi vya wachache walioshindwa katika mchakato wa Demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na maliasili gesi na nyingi ipo katika Bahari, sasa tusiruhusu makampuni binafsi kuwa ndiyo yenye dhamana ya kulinda maliasili yetu katika makampuni ya nje yanayofanya tafiti na kutoa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa ya kuwa na gesi si ya kuachia makampuni ya nje yaje kuchuma hapa hata katika ulinzi. Ulinzi ni gharama, ni wajibu wa makampuni ya uchimbaji gesi kugharamia na ni gharama kubwa. Wanalipia hivyo Taasisi yetu ndiyo iwe mlinzi na ipate malipo ya kuendeleza ulinzi wa maliasili yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza bajeti ya Wizara hii nyeti iwe inajadiliwa na Kamati za Ulinzi na Usalama na Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pia Mambo ya Ndani ya Nchi ili iwe siri na si majadiliano ya hadharani na Bunge zima. Mikakati ya ulinzi na usalama ni ya siri ya nchi na ni nyeti, hivyo muhimu

kuhifadhiwa. Usuluhishi wa matatizo ya Jeshi pia utafanyika kimya kimya na Bunge likasimu madaraka kwa Kamati hizo tatu tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu libadilishane tafiti na maendeleo ya ulinzi wa kisasa na Vyuo vyetu Vikuu ili kuongeza ufanisi katika sayansi na teknolojia. Jeshi pia litakuwa chombo cha uzalishaji na matumizi ya kisasa ya vumbuzi mbalimbali Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, JWTZ na JKT wamefanya kazi kubwa ya uhifadhi wa Mlima pale Kigoma na kutunza ardhi na kupunguza mmomonyoko na kujaza mchanga katika Ziwa Tanganyika na hivyo tope kujaa na kina kupungua na meli kupungua kiwango cha mizigo kuja Bandari ya Kigoma. Jeshi lishirikiane na Manispaa ya Kigoma ili mchanga na tope zisiue Bandari na Stesheni ya Kigoma. Nguvu na taaluma ziungane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mto upande wa Kongo Wear ilibomolewa makusudi na Jeshi la DRC na kufanya maji mengi yatoke Ziwa Tanganyika. Jeshi na Wizara isimamie maji kutokana na Wear kukarabatiwa ili Bandari za Tanzania katika Ziwa Tanganyika kina kisiendeleo kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzuia migogoro isiyo ya lazima baina ya Wananchi na Jeshi lao, maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya shughuli za kijeshi yapate fidia ya haraka na yawekewe mipaka haraka. Ugomvi baina ya Jeshi na Raia siyo jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi ya Serikali ya kupatikana fedha ya ujenzi wa nyumba 6,064 za Wanajeshi. Tabia ya Wanajeshi kukaa uraiani inaleta taswira na mahusiano mabaya. Nashauri ujenzi wa nyumba hizo ukamilishwe haraka ili Wanajeshi wote waishi Kambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wanapopangiwa kwenye shughuli za kijeshi nje ya nchi, stahili zao hawapati kwa sababu ni vigumu askari kudai. Stahili nyingi zimepotea, jambo hili litazamwe.

Iwapo tangu Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 fedha za posho hazijaongezeka; Askari walioongezeka wanapataje posho yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, kazi ya kuimarisha mipaka ya nchi ni ya Wizara ya Ardhi na Mambo ya Ndani, lakini kama hatua ya haraka haitachukuliwa hali hii itasababisha vita baina ya nchi na nchi kwa mfano, Mpaka wa Malawi na Tanzania katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili ulinzi wa nchi uwe na dira sahihi kwa kipindi hiki ni muhimu Sera ya Ulinzi wa Tanzania kuhuishwa kwake kukakamilishwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na Jeshi lililokuwa na nidhamu kama sasa, vijana wanaoomba kujiunga na Jeshi wachujwe barabara (*proper vetting*) na wawe waliofaulu skuli.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya masurufu ya wastaafu (Jeshi la Akiba) pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waraka wa Serikali Nambari 234 wa tarehe 7 Julai, 1967, Sheria ya Jeshi la Ulinzi 1966, Kanuni chini ya Fungu 66, unafafanua jinsi maslahi ya masurufu ya askari wastaafu yanavyotakiwa kuboreshwa kwa muktadha ufuatao:-

- (i) Masurufu ya pensheni;
- (ii) Pensheni ya kutojiweza; na
- (iii) Pensheni ya vifo na bahshishi kwa makundi mbalimbali katika utumishi wa wajane.



Hali ilivyo sasa kwa wastaafu wa jeshi imeweka njia panda ya sintofahamu ni nani anastahili maboresho ya pensheni kati ya askari wastaafu wa miaka 1964 – 2007 na askari wa miaka ya 2008 na kuendelea, kwa vyeo vya aina moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu upi wa Serikali uliotumika kuwaweka wastaafu katika mafungu mawili ya maslahi ya masurufu duni na wapiganaji, askari wastaafu maslahi ya masurufu bora. Kwa vyeo linganifu kwa wastaafu (Jeshi la Akiba)?

Ni utaratibu upi wa Serikali uliotumika kwa Maafisa Wakuu Wanadhimu (*Generals*) Wastaafu kuhamishiwa katika Wizara ya Utumishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kawe, ambalo lina wastaafu wengi sana wa Jeshi, kumekuwa na sintofahamu nyingi sana juu ya uwepo wa Jeshi la Akiba. Naomba Serikali itoe ufafanuzi, kwani wengi wamekuwa wakihoji nafasi yao ikoje; je, kuna maslahi yoyote ambayo wanastahili kupata hawayapati?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dhana yake ya kuwalea vijana na kuwapa mafunzo, JKT imekuwa na utaratibu wa kuwachukua vijana wa kujitolea kutoka katika maeneo mbalimbali ya nchi. Vijana ambao hupewa mafunzo ya kutumia silaha za moto, mbinu za kivita, medani za kivita na kadhalika. Mafunzo ambayo huchukua takribani miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, jukumu la msingi la JKT ni kutoa mafunzo tu na si kutoa ajira, lakini ni ukweli vilevile kwamba, Serikali ina wajibu wa kujitazama upya na kuangalia ni kwa namna gani vijana hawa wanaopewa mafunzo ya hali ya juu na kuachwa wanazagaa mitaani mara baada ya kumaliza mafunzo. Hakuna ubishi kuwa Wizara, Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali ambazo zimekuwa zikiajiri watu wanaotakiwa na Taaluma ya Kijeshi pasipo kuishirikisha JKT ambayo tayari ina vijana ambao wana ujuzi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe kauli ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba vijana hawa, ambao wamekaa Kambini kwa gharama za Serikali wanatumika ipasavyo kwa masilahi ya Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ubishi kwamba, Jeshi letu ndiyo mhimili mkuu wa ulinzi wa ndani na mipaka ya nchi yetu. Pia hakuna ubishi kwamba, Kambi zetu za Jeshi hazina budi kuwa salama ili kuepusha majasusi kupata taarifa za ndani za kiusalama za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa masikitiko makubwa, katika Kambi ya Jeshi ya Ruvu, kuna Wachina ambao idadi yao haifahamiki, wamekuwa wakiishi ndani ya Kambi kwa kisingizio kwamba eti Serikali ya China ina ubia katika kiwanda cha kushona nguo au sare za jeshi!

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari sana kwa usalama wa nchi yetu. Naomba kupata kauli ya Waziri juu ya uhalali wa raia wa kigeni kuishi ndani ya Kambi zetu za Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mambo machache tu ambayo nimeyaona katika Wizara hii, pamoja na changamoto ambazo zimekuwa zikikwamisha ufanisi wa Wizara hii. Pamoja na kuwa mimi ni Mjumbe mtiifu wa Kamati inayohusu Wizara hii, lakini kuna mambo ambayo pengine nimeyapata baada ya Vikao vya Kamati na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la upandishaji vyeo kwa Maafisa ambao wameongeza elimu yao kitaaluma. Sielewi ni vigezo gani vinafuatwa kumpandisha cheo Afisa wa Jeshi maana kwenye kada zingine, Afisa akiongeza elimu yake lazima apande cheo na mshahara upandishwe, lakini kwa Jeshi la Ulinzi hiki kitu hakipo na hakifanyiki, hivyo, kuwakatisha tamaa maafisa ambao wangependu kuongeza elimu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie suala hili kwa umakini ili mwenye haki ya kupandishwa cheo apandishwe na kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wastaafu kuendelea kutumikia Jeshi kwa mkataba ni tatizo kubwa, kwani nimepata malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wanajeshi ambao utaalumu waliionao ni sawa na hao wastaafu, lakini hawapewi nafasi hizo. Wakati huo huo Serikali inapoteza pesa nyingi kuwalipa maafisa ambao wamestaafu lakini wanaendelea kufanya kazi kwa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria ambayo inamtaka Askari katika Jeshi la Wananchi anapomaliza miaka sita ya utumishi wake ndani ya Jeshi kuruhusiwa kuoza au kuwa na familia (yaani kutoka katika ukapera). Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki hii kwa Askari hawa, kwani Wakuu wa Vikosi wamewafanya Askari hao makapera kuwa ni miradi yao ya kujipatia vipato, licha ya ukweli kuwa kwa mujibu wa taratibu za Jeshi wanapaswa kuruhusiwa kuoza au kuolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu katika hili suala kwani huu ni ukiukwaji wa haki ya msingi na pengine inaweza ikawasababishia hata maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU). Wahanga hawa ni Askari wa *intake* ya 17 na 18, hawajaruhusiwa kupata haki yao hiyo, huku watoto wa Maafisa wakubwa au wametoka wote, wamewaacha watoto wa maskini wakilia na kusaga meno. Askari hao ambao wana miaka minane bado mpaka sasa wameshikiliwa ndani tu huku Wakuu wa Vikosi wakidai hawawezi kuwatoa eti kwa sababu vikosi vyao havijapata Askari wapya huku jukumu hilo ni la mwajiri na siyo la Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wamechoka sana huko makambini, naomba Serikali iangalie jinsi gani itaweza kuwasaidia hao Askari ili waweze kupata haki yao hiyo ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeweka utaratibu wa vijana wanaomaliza Kidato cha Sita kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa Sheria; na kwa kuwa wapo vijana wanaojiunga na JKT kwa kujitolea hivyo kufanya Makambi ya JKT kuwa na vijana wengi kwa ajili ya mafunzo mbalimbali; lakini yapo matatizo mbalimbali katika Makambi hayo na kama hayatapatiwa ufumbuzi yanaweza kuleta madhara makubwa kiafya.

Kwa mfano, Kambi ya 835 Kj (Mgambo JKT), yapo matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama, gari kwa ajili ya shughuli mbalimbali za hapo kambini, gari la wagonjwa, pamoja na gari la Mkuu wa Kambi, matrekta kwa ajili ya kilimo na nishati mbadala kwa ajili ya kupikia. Nataka kufahamu mikakati au mipango ya Serikali kuondoa matatizo hayo kwenye Makambi yetu ya Jeshi hususan 835 Kj (Mgambo JKT).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ajira kwa Askari wa JWTZ, naomba Serikali itoe kipaumbele au liwe ni sharti kwa yule raia anayetaka kuajiriwa na JWTZ awe amepita JKT. Hii itasaidia sana kuondoa dhana ya upendeleo, kwani wapo vijana waliojiunga na JKT kwa kujitolea na kupata mafunzo kwa zaidi ya miezi sita lakini wanapoomba ajira JWTZ, hawapati na hivyo kuwafanya kukosa ajira na kurudi majumbani kwao mikono mitupu. Hii ni hatari kwa mtu aliyepata Mafunzo ya Kijeshi kuachwa mtaani bila ajira yoyote, anaweza kushawishika na kujiingiza katika makundi ya kihalifu kama ujambazi, ujangili na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naiomba Serikali badala ya kuajiri Askari wa JWTZ kutoka mtaani, sasa iajiri kwa kuwachukua vijana waliopo au waliopitia JKT. Suala hili lisiwe kwa JWTZ pekee, bali hata Polisi, *TANAPA*, Bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Kwanza, naunga mkono hoja.

Pili, Wananchi wa Kongwa bado wanaendelea kuliomba Jeshi la Wananchi wa Tanzania kufikiria kurudisha Kambi ya Kongwa.

Kupitia kwangu kama Mbunge wao, naomba kuwasilisha ombi la Wananchi wa Kongwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii katika eneo moja tu nalo ni migogoro ya ardhi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWT), ambao umekithiri na kuwaacha Wananchi wakikaa bila kufanya shughuli za maendeleo kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka ni mara kadhaa nimeshafuatilia na kuhoji juu ya JWT kuvamia maeneo ya raia, ambapo awali walipewa makazi ya muda tu baada ya Mto Mori kufurika na kukosa miundombinu ya daraja, ambapo kikosi chao kilikuwa Nyandoto, lakini walivamia na kujimilikisha maeneo ndani ya Makazi ya Raia (*Ronsolti & Msati*) Wilayani Tarime kinyume cha Sheria ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni kinyume na haki za binadamu, kumsimamisha Mwananchi kutofanya shughuli yoyote ile ya uzalishaji kama kulima, kujenga wala kutembea usiku au jioni ilihali hawa JWTZ wamevamia eneo lile tangu 2007 na kuwaambia Wananchi kutokufanya shughuli yoyote ile na hadi sasa hamna fidia yoyote ile iliyofanywa. Badala yake mazao ya Wananchi wale yaliharibika, hata miti yao ya kudumu kama Mikaratusi walikatazwa kukata na nyumba na vyoo vikibomoka hawaruhusiwi kukarabati. Hii siyo haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilishahoji juu ya mmoja wa Wanajeshi hao kumbaka mtoto wa shule ya msingi na kesi ipo Mahakamani. Hii ni athari mojawapo ya hawa Wanajeshi kuishi ndani ya makazi ya raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inipe majibu ni lini watalipa fidia ya wale Wananchi wa Ronsolti/

Msati; na je, hiyo fidia itazingatia hasara ya kutozalisha (kufanya shughuli za kiuchumi tangu 2007? Kama imeshindwa bora iwaruhusu Wananchi wafanye shughuli zao kama kawaida na wale Wanajeshi warudi Ngandoto kwani miundombinu ya Daraja la Mto Mori imeimarishwa na pale ndiyo mbali na makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nawapongeza Wanajeshi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ulinzi wa Taifa letu mpaka sasa hatuna vita nchini. Hii inaonesha ni jinsi gani Mkuu wa Majeshi yetu alivyo imara katika uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iziangalie nyumba zilizopo za Wanajeshi wetu kwani zinatia aibu. Nyumba ni chakavu na ni ndogo sana kuweza kumudu familia moja ya Mwanajeshi mwenye mke na watoto. Mfano, *barracks* za Lugalo ndani, nyumba hizi ni ndogo kwani zina chumba kimoja tu cha kulala na sebule. Ikumbukwe Askari hawa wana watoto. Kwa namna hii maadili ya watoto wetu yatatoka wapi? Kuna *barracks* zingine za Dar es Salaam, Area D, H, na E. Hizi nazo zina vyumba viwili tu vya kulala na wanaishi Askari wenye watoto. Licha ya kuwa ni chakavu, tukiacha za Area E ambazo zilikarabatiwa, ni ndogo mno kuweza kuleta staha ya familia za Wanajeshi wetu. Naitaka Serikali sasa ilione hili na ilichukulie uzito ili kuleta heshima ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa JWTZ na Serikali kuangalia Wanajeshi wake wakitangatanga mitaani na kujichanganya na raia. Askari ni mtu ambaye amebeba siri nyingi sana kifua ni mwake na kama binadamu ana madhaifu yake. Sasa anapokaa uraiani atawezaje kuhimili utunzaji huu wa siri endapo atakuwa kwenye maeneo ya starehe na watu wengine?

Licha ya kutunza siri, tumeshuhudia ugomvi na mauaji ya mara kwa mara, aidha, kwa raia au Askari wakiwa katika maisha yao uraiani. Hili tungeweza kuliepuka endapo Serikali ingekuwa makini na kuona umuhimu wa makusudi wa kuwajengea Askari wake nyumba za kuishi Kambini. Athari ni kubwa sana na ndiyo maana nidhamu ya Jeshi inashuka na hata heshima ya Jeshi inakuwa haipo kutokana na tabia za wachache. Serikali ikae chini na kutafakari ni kwa namna gani inaweza kuondoa fedheha hii ya Wanajeshi kutangatanga na kuishi uraiani ambako inawavunjia heshima na kupunguza heshima ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tofauti kubwa sana kati ya Askari waliostaafu kuanzia mwaka 2006 kurudi nyuma na wale waliostaafu 2007 na kuendelea. Hawa waliostaafu zamani wanapata pensheni ndogo sana isiyokidhi mahitaji yao pamoja na kulitumikia JESHI kwa zaidi ya miaka 30 tena kwa uadilifu mkubwa. Ikumbukwe kwamba, Wanajeshi hawana utaratibu wa kuchangia kwenye Mifuko ya *Pension* na Hifadhi ya Jamii na hivyo hulipwa mafao yao kulingana na *rank* zao. Kwa nini *pension* inapopanda kwa hawa wanaostaafu sasa hivi hata kama wana cheo sawa na waliostaafu miaka ya nyuma na ya hao wastaafu wa zamani isipande?

Wanajeshi wastaafu wanaishi maisha ya aibu sana huko mitaani. Hii yote ni fedheha kwa Serikali. Naishauri Serikali iangalie upya mafao ya wastaafu yaendane sawa na ya wengine. Mfano mzuri ni wa *CDF* waliostaafu zamani, wana maisha magumu sana ukilinganisha na hawa waliostaafu hivi karibuni wakati wote ni Majenerali. Serikali iondoe aibu hii kwa Askari wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mara yangu ya tatu kulalamikia unyonyaji unaofanywa na Maduka ya Jeshi yanayoendeshwa na Waasia. Haya ni maduka ambayo yameondolewa kodi (*Duty Free*) ili yaweze kuwahudumia Wanajeshi na familia zao. Nia ya kuondoa kodi ni kuwafanya Wanajeshi waweze kumudu kununua bidhaa kwa bei ndogo kama motisha kwa kazi kubwa na ya hatari wanayoifanya.

Sasa ni kwa nini wamiliki wa maduka haya wanauza bidhaa kwa bei sawa na zile za mitaani? Kwa nini Serikali pamoja na Jeshi wamekaa kimya na wasiyafungie maduka haya na kuwachukulia hatua za kisheria za kukiuka mikataba waliyosaini? Je, siyo kweli kwamba kuna mkono wa wakubwa katika maduka haya na hivyo kuwalinda wawekezaji hawa wa kigeni? Naitaka Serikali itoe tamko ama wamiliki walipe kodi sawa na wengine au wayafunge maduka haya ya kinyonyaji. *TRA* nayo itoe tamko ni kwa nini haifuatilli maduka haya na kuona kama hayakiuki mkataba?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuwalipa askari *allowance* ya kulipa bili zao za umeme na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo mkubwa wa kulipa bili hizi ambazo zilikuwa zimezidi uwezo wake kwa matumizi mabaya. Pamoja na hilo, ningeshauri Serikali ianze sasa kuwapa askari *allowance* ya kulipia ankara zao za maji ili kupunguza udaiwa sugu wa Wizara kwa mamlaka za maji nchini. Tumekuwa tukipitisha fedha za kulipa bili za maji kila mwaka, lakini malalamiko toka Mamlaka za Maji nchini ni makubwa na Jeshi ni wadaiwa sugu. Serikali iondoe aibu hii kwa kuwapa askari *allowance* ili wao wenyewe walipie kama wanavyolipia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wamekuwa wakijitolea kufanya mafunzo JKT kwa miaka miwili na wanafundishwa mbinu za kivita, ni vizuri Wizara ikaona umuhimu wa kuwaajiri vijana hawa kuliko kuendelea kukaa mitaani ambako wanaweza kushawishika na kuwa majambazi, maana tayari wameshakuwa na ujuzi wa kutumia silaha na wana mbinu za kujihami walizofundishwa JKT. Pia kuna malalamiko mengi kwamba, ajira zinatolewa kwa upendeleo kwa kuwabeba watoto wa wakubwa wasio na sifa. Kama hili lipo, Wizara ijsahihishe maana watoto wasio na sifa ndiyo hao wanaoliaibisha Jeshi na husababisha utovu wa nidhamu Jeshini. Ajira zitolewe kwa wanaostahili na wenye sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.



**NAIBU SPIKA:** Sasa naomba nimwite Waziri wa Mambo ya Nje - Mheshimiwa Benard Membe.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nitajikita kwenye masuala mawili ambayo yameelezwa na Kambi ya Upinzani, nayo ni Malawi na M23.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo, napenda kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri na pia niipongeze leo *exceptionally* Kambi ya Upinzani, wamezungumza wakiweka utafa mbele, uzalendo na Ndugu yangu Mheshimiwa Lissu amezungumza kwa staili ambayo kama akiendelea na hali hiyo, atakuwa mwanasiasa mzuri sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sana! *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Malawi. Kwenye Kambi ya Upinzani wametoa hoja moja nzuri lakini ni mbili. Moja ni swali kwamba: Je, hali ya mpakani inakuwaje baada ya Malawi kutishia kuondoka? La pili: Je, kule *DRC* ambapo vijana wanakwenda na Malawi inakwenda huko, hali ya usalama wa vijana wetu itakuwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mpaka wa Malawi na Tanzania ni nzuri na Malawi imerudi tena kwenye mazungumzo. Mazungumzo yataanza rasmi kwa maana ya sisi kuitwa kuhojiwa akiwamo Mwanasheria Mkuu mwishoni mwa mwezi huu, Mjini Maputo. Tutakuwa tunahojiwa na mazungumzo yatakuwa yanaendelea.

Ni imani yetu Watanzania kuwa jopo la Marais wastaafu linaloongozwa na Mheshimiwa Joachim Chisano, litafikia uamuzi. Lakini tumesema wakitushauri kwamba, ili tupate uamuzi wa kudumu inabidi tusonge mbele kwenye *ICJ*, Tanzania hatutasita kufanya hivyo na tuna kila aina ya ushahidi wa kuhakikisha tunashinda kesi ile. *(Makofi)*

Kuhusu vijana wanaokwenda *DRC* pamoja na kikosi cha Malawi, naomba niseme pia kwamba ni kweli katika nchi zilizochangia kupeleka Askari wake *DRC* Malawi ipo. Pia ni kweli kwamba vikosi vile vitakuwa vinaongozwa na Kamanda Mtanzania.

Taarifa tulizonazo hadi sasa ambazo nitazisema juu juu kidogo kwa makusudi ya kuhifadhi usalama wa vijana wetu ni kwamba, maeneo watakayokuwepo Wamalawi na Watanzania ni umbali wa karibu kilomita 100 *apart*. Yaani watakuwa tofauti kilomita 100.

Kwa hiyo, hakuna atakayemtisha mwenzake na wote watakuwa wanafanya majukumu yaliyoorodheshwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa *Resolution Na. 2098*. Kwa hiyo, hakuna matatizo ya vijana wetu pale.

Kuhusu *M23*, *M23* wameleta barua Bungeni na imezungumzwa vizuri na Kambi Rasmi ya Upinzani na Ndugu yangu Mheshimiwa Zitto, vizuri sana.

Kule Wizarani pia nimepokea barua, imeandikwa, wenyewe wamesema imeandikwa na Mungu, *signature*, ya Mungu; na imekuwa *addressed* kwangu na Mungu. Lakini lugha yenyewe ni hii hii. Nadhani na wenyewe walikuwa wanataka kutumia jina la Mwenyezi Mungu na wenyewe kuishinikiza Serikali ili tutishike na tusifanye majukumu ya kitaifa.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwaasa na kuwashauri Watanzania wenzangu, nakubaliana kabisa na kauli ya Kambi Rasmi ya Upinzani na Ndugu yangu Mheshimiwa Zitto, *M23* wanatutisha kama alivyotutisha Kanali Bakari wakati tunakwenda Anjuan Commoro, kwamba vijana wetu wakienda watakuwa chakula cha mamba. Vijana wakaenda, badala ya kuliwa na mamba, wao ndiyo walikula samaki na siku ya tatu Kanali Bakari akaondoka na buibui kukimbilia Mayote Island. *The rest is history!*

**MBUNGE FULANI:** Ni baibui!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Baibui! (*Kicheko*)

*The rest is history.* Kwa hiyo, ni vitisho vinavyokuja na mtu aliyekata tamaa. M23 wanaua, wamebaka, wamedhalilisha wazee na akina mama, wameleta wimbi la wakimbizi 220,000 na hasa 30,000 kuingia Tanzania. M23 hawawezi kum-*quote* Mwalimu Nyerere anayesema binadamu wote ni sawa, huko ni kukufuru. Kama wangekuwa wanathamini kauli ya Mwalimu kwamba, binadamu wote ni sawa, wasingaliau, wasingalibaka na wasingalidhalilisha wazee wenzao. (*Makofi*)

Wamefanya hivyo hadi kusababisha Kiongozi wao, John Bosco Ntaganda kujisalimisha mwenyewe na hivi ninavyozungumza, yuko kwenye Mahakama ICC, *the Hague* kujibu mashtaka ya uhaini na makosa ya jinai aliyoyafanya na wenzake hawa hawa M23. Kwa hiyo, hawawezi kutufundisha ubinadamu na amani na wala hawawezi kutumia jina la Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Baba yetu wa Taifa, kutuambia wema ni kitu gani. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, M23 chimbuko lake ni nini hasa? Mwaka 2008 Tanzania ilipokuwa Mwenyekiti wa AU, CNDP iliyokuwa inaongozwa na Laurent Nkunda wakati huo, ndiyo ilishika eneo lote la Kivu na wakawa wanapiga, wanadhalilisha na kubaka. Umoja wa Mataifa ukaingilia kati, ukamteua Olusegun Obasanjo na AU ikamteua Mzee Benjamin Mkapa kuwa wasuluhishi wa tatizo la vita ya wenyewe kwa wenyewe DRC, wakaenda.

Tarehe 23 mwezi Machi, 2009 ndipo mkataba huu au makubaliano haya yalipofikiwa ya kuwaomba Askari 3,600 wa CNDP wajiunge na Jeshi la Taifa la Kongo – DRC ili kuwe na amani pale. Askari 3,000 wakakubali, 600 wakakataa. Ni hawa Askari 600 ndio waliounda kikosi kinachoitwa leo M23, yaani March 23<sup>rd</sup> *Agreement* iliyofanywa na Mzee Benjamin Mkapa pamoja na Olusegun Obasanjo. Askari hao 600! Wakaanza vita Aprili, 2012, wakaua, wakabaka, wakafanya vitendo vyote hadi kufikia Novemba wakashika Mji wa Goma.

Mheshimiwa Naibu Spika, walipofikia hapo, *AU* ikakutana na ikatoa suluhisho kwamba ni vizuri Rais Kagame pamoja na Rais Museveni wasaidie kutatua tatizo hili. Kwanini walifanya hivyo? Walifanya hivyo kwa sababu Rais Kagame alikuwa anatumia wa Umoja wa Mataifa kutokana na timu iliyopelekwa *DRC* kufanya uchunguzi wake, wakagundua kwamba, kule kwenye M23 kulikuwa na majeshi na silaha za Rwanda.

Kwa hiyo, Rwanda ikaanza kusakamwa. *AU*, *SADC* na nchi za Maziwa Makuu zikawataka Rais Kagame na Rais Kabila chini ya uongozi wa Rais Museveni wakae wayamalize. Hatukufanikiwa. Lakini baadaye *SADC* ikaukumbusha Umoja wa Mataifa kwamba, kwa kuwa mna majeshi yenu 17,000 *DRC* na mnatumia dola bilioni 1.5 kwa mwaka, fanyeni kitu, kwa sababu wakati wa mashambulizi ya Goma, Majeshi ya Umoja wa Mataifa ndiyo yaliyosimama na kushangilia waasi hawa mpaka wakaingia jiji la Goma na kuleta maafa yote yaliyotokea Goma. *SADC* pamoja na Nchi za Maziwa Makuu tulikasirishwa mno kuona kwamba kuna majeshi ya Umoja wa Mataifa yanayoitwa *MONUSCO* yako pale kwa muda wa miaka 15 na Rais Museveni anayaita Majeshi ya Utalii wa Kijeshi, yako pale hayafanyi kitu chochote. (*Kicheko*)

Sasa nchi za Maziwa Makuu pamoja na *SADC* zikaazimia kutengeneza Jeshi linaloitwa *Intervention Brigade* ili liende kule likaifanye kazi waliyoshindwa wenzetu wa majeshi ya *UN*. Lakini ili kwenda kule, tulihitaji *resolution* maalum ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Siku ya tarehe 28 Machi, mwaka tumelipata lile azimio linaloruhusu sasa nchi kutoka *SADC* na *ICGR* ikiongozwa na Tanzania ziende kule. Nchi nyingine ziko pale; Malawi imehajitolea kama mlivyosema, Mozambique imejitolea, Angola sasa imejitolea inaingia mle ndani, *South Africa* imo mle ndani; nia yetu ni kupata Askari 4,000 waende wakafanye kazi tatu. Hatuendi vitani! Kazi tatu. Kazi ya kwanza ni kuhakikisha kwamba, M23 haijipanui. Wako Askari 600 na wengine wameishaanza kujindoa. Kwa hiyo, ni kuhakikisha haijipanui na kuleta madhara *DRC*.

Kazi ya pili, lazima tuidhoofishe hii M23 kwa kuondoa silaha zao kutoka mikononi na kule walikozificha ili *DRC* ibaki nchi ya amani. Kazi ya tatu ni *re-integration*. Ni vizuri wale Askari ambao tutaona wako bora, waingie kwenye Jeshi la Taifa la *DRC* ili kuleta amani pale, na tutalinda amani pale. Wakituchokoza, tutajibu mapigo. Lakini lengo la safari ile, siyo kwenda kupigana vita. Nasi tunakwenda na *mandate* ya Umoja wa Mataifa ya *Chapter Seven*.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linapopeleka vikosi maalum kama cha kwetu, *International Brigade*, hakiendi kule kwa ajili ya vita. Tunakwenda kulinda amani, na pale inapokosekana, kuitengeneza (*peace enforcement*). Ndiyo matetemeko hayo mnayoyasikia kutoka M23, "mkija tutawaua kwa halaiki!" Hawawezi kufanya hivyo! Mbona Pakistan wako pale hawawau? Mbona India wako pale hawawau? Mbona *South Africa* imetangulia na hawawau? Kwanini wawaue Watanzania tu? Au wanaogopa vijana wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni moja tu kwamba, vijana wetu na Jeshi letu ni imara sana, lenyewe halishindwi! Lipo Lebanon linafanya kazi nzuri na ya kustahili kusifiwa; lipo Darfur linafanya kazi nzuri na linastahili kusifiwa na Watanzania wajue tena nasisitiza aliyoyasema Waziri kwamba, kiongozi wa *UNAMID (United Nations Mission in Darfur)* sasa inaongozwa na Jenerali Mtanzania kuanzia mwezi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na rekodi nzuri ya Jeshi letu la Tanzania ndiyo maana hawa waasi wanaobaka na kua, wakisikia tu Tanzania inakwenda, wanamsingizia Mungu kwamba anawaunga mkono, wanamsingizia Mwalimu kwamba anawaunga mkono, wanaliomba hili Bunge liseme kwamba Serikali isiende.

Mimi nasema nalipongeza sana Bunge kwa uelewa mpana, na kuungana kuwa kitu kimoja tunapokabiliwa na vitisho vya aina hii. Tanzania tunatisha, tuna nguvu na tuna historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, M23 wakitaka sisi tusiende kule, wafanye mambo matatu tu. Moja, wafanye kama walivyofanya jana, waanze kujitoa kwenye Jeshi lile na kujisalimisha, kwa sababu tutakwenda. Pili, yako mazungumzo yanayofanywa na Rais Yoweri Museveni, Kampala ya kuitaka M23 pamoja na Serikali ya *DRC* kukaa na kumaliza tofauti zao. Wamalize tofauti zao na watupigie simu, kwamba tumeishamaliza matatizo yote.

Tatu, waache kubaka, kua, kuwatawanyisha watu kutoka kwenye nyumba zao na kwenda porini na kuwafanya wakimbizi ndani ya nchi yao. Waache kufanya vile, ili siku moja hata ninyi Wabunge hasa wale 25 waliokwenda Jeshini, mwende Goma mkakae wiki moja, mrudi mje mtwambie. Akina Membe na Nahodha wala hamna haja ya kwenda Goma, hali ni nzuri na shwari. Ingawa wakati wa kwenda huko inabidi mwanze kusali kwanza kwa sababu hatujui kinachotokea kule. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, *mission* tuliyopewa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, *AU* na *SADC*, na sisi ndiyo Mwenyekiti wa troika ya *SADC*, *mission* tuliyopewa na nchi za Maziwa Makuu, ikatutaka twende tukawasaidie jirani wanapoungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nalijibu swali la Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba, sasa tuna faida gani za kiuchumi tunapokwenda kule? Tokea enzi za Baba wa Taifa, kote tulikokwenda kukomboa wenzetu, kipaumbele chetu cha kwanza kilikuwa ni usalama wa kudumu katika nchi ile. Tumekomboa nchi nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuendi kama hawa aliowaita ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, *the lords of wars*, wale wanaotengeneza vita au kujiingiza katika vita kwa ajili ya manufaa yao ya kiuchumi. Tanzania tunakwenda kama *peace advocates*. Tunakwenda kuleta amani kwenye nyumba jirani. Baada ya amani kupatikana, ndiyo tunaziomba sasa *NGOs*, Mashirika na watu wengine, hata binafsi wanaoweza kuchangamkia fursa za

kwenda kule tulikowekeza damu yetu, kwenda kuwekeza. Kama sasa hivi Watanzania wanavyoanza kwenda kule Comoro, na kama Watanzania wanavyojipanua kule Sudan. Waende kule baada ya amani kupatikana, Watanzania binafsi, mashirika na makampuni mnaruhusiwa kabisa kwenda kuwekeza kule, *ofcourse* ni pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Naibu pika, kipaumbele chetu tunapokwenda kwenye ukombozi, shughuli za uhuru, ni amani na usalama kwa sababu hiyo ndiyo nguvu aliyotuletea Baba wa Taifa na ndiyo heshima ya Tanzania duniani. Kuzima moto kwenye nyumba ya jirani kwanza kabla ya mambo mengine. Baada ya hapo tutazungumza masuala ya mipango mipya ya uchumi, kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya namna gani mnaweza mka-*take* kutokana na uchumi uliopo pale ili muweze kuendelea, nchi yenu pamoja na nchi jirani.

Kwa hiyo, mwishoni naomba nimalizie tu kwa kusema kwamba, chimbuko la tatizo la M23 lilianza kwao wenyewe kwa vita vya ndani kwa ndani, tukapata vibali vyote vya Baraza la Usalama, *AU*, nchi za Maziwa Makuu pamoja na nchi za *SADC*, kukubaliana kwamba muda umefika, na nakubaliana na Mheshimiwa Zitto kwamba tulichelewa. Muda umefika wa kwenda kuwasaidia ndugu zetu ili Kongo kwa mara ya kwanza iishi kwa amani, ili tuwe na uhusiano kama majirani zetu. Tukifanya hivyo tutakuwa tumetimiza wajibu wetu.

Kwa hiyo, M23 wasitutishe, wala hakuna cha mtu wa kututisha, kuzuia majeshi yetu kwenda kulinda amani na ku-*reinforce* amani ile. Nawahakikishia kwamba tumezungumza na Kamati zote mbili; Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa undani zaidi ili kuomba baraka zao, na wametoa baraka kwa niaba yenu wote na muikubalie Serikali kwenda kutimiza wajibu ambao nchi hii inaendelea kupata heshima yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bernard Membe - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ambaye ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili aweze kupitia hoja za wachangiaji wote.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kutoa michango yao kwa maandishi na kwa kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka nimehemewa kwa jinsi Waheshimiwa Wabunge hasa waliopata nafasi ya kuchangia, kwanza nikianza na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, wametoa michango mizuri sana. Kwa kiwango cha michango waliyoitoa, ninajihisi kwamba nina deni kubwa kwao. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuyafanyia kazi maoni na ushauri waliutoa kwa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Wabunge 65 waliochangia, Wabunge tisa wamechangia kwa kuongea, na Wabunge 56 wametoa michango yao kwa njia ya maandishi. Kutokana na ufinyu wa muda, sitaweza kuzijibu hoja zote kwa ukamilifu. Hata hivyo, hoja zote zitajibiwa kikamilifu kwa maandishi na majibu yake kuwasilishwa hapa Bungeni ili kila Mbunge apate nafasi ya kupata majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba yangu kwa kuanzia na hoja ya Mheshimiwa Omari Nundu, aliyesoma hotuba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omari Nundu, ametoa uchambuzi mzuri sana kuhusiana na suala la ufinyu wa bajeti unaoikabiri Wizara yangu hasa kwenye eneo la fedha zinazotolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.



Ameiomba Serikali basi, ichukue hatua na kuhakikisha kwamba kabla ya kufika mwezi Juni, mwaka huu wa 2013, fedha ambazo hazijatolewa, zitolewe ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake.

Namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutoa maelezo hayo. Bila shaka kama nilivyoeleza kwenye bajeti, eneo hili limeathiri sana utekelezaji wa bajeti. Sasa sisi Serikali tumelisikia jambo hilo, Wizara yangu imelisikia ombi hilo na tutakaa na Wizara ya Fedha ili tuone ni kwa kiasi gani wanaweza kulitekeleza jambo hili. Kwa sababu tulipokutana wakati wa kuwasilisha mapitio ya bajeti katika Kamati ya Ulinzi na Usalama, Watendaji wa Wizara ya Fedha walitoa ahadi kwamba wanao uwezo huo wa kuhakikisha kwamba watatoa fedha kabla ya kufika tarehe 30 Juni, mwaka huu. Ahadi ni deni, na muungwana akiahidi, basi lazima atekeleze. Nina hakika kwamba, watatekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu kudhibiti wahamiaji haramu na wafugaji kutoka nje ya Tanzania; ni kweli kwa muda mrefu tumekuwa tukikabiliwa na wimbi kubwa la wahamiaji haramu wanaoingia nchini kwetu kupitia mipaka ya nchi jirani, lakini pia tumekuwa na tatizo kubwa la wafugaji kutoka nchi jirani nchi ambao wanakwenda nchini kwetu kwa ajili ya kutafuta malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu tayari imeshaandaa mapendekezo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu namna bora ya kuweza kutekeleza jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge jambo lenyewe siyo rahisi sana kwa sababu maeneo haya ambayo wahamiaji haramu wanapita kama mnavojua mipaka ya nchi yetu ina maeneo makubwa sana, lakini Wizara yangu itashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mikoa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na sisi wenyewe ili tuweze kushirikiana namna ya kuweza kutafuta njia rahisi zaidi ya kuweza kufanikisha ulinzi katika eneo hili ili hatimaye wahamiaji haramu waweze kudhibitiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na tatizo la kung'olewa alama za mipakani pamoja na ujenzi wa barabara za mipakani, tayari sisi tumeshawasilisha mapendekezo Serikalini ya namna ya kulitatua jambo hili. Lakini Serikali wakati ilipokuwa inalitafakari jambo hili, ikabaini jambo moja kwamba alama ambazo zimeng'olewa kwenye maeneo ya mipakani ni nyingi sana na kuweza Serikali kupata fedha kwa ajili ya kuzigharamia. Pengine zoezi hilo linaweza kuwa na gharama kubwa sana pamoja na kutengeneza barabara za usalama kwenye mipaka.

Sasa tulichokipendekeza ni kwamba tuanze kwenye baadhi ya maeneo. Kwa mfano, tumependekeza kwenye yale maeneo ambayo tatizo linaonekana kubwa, mpaka wetu kati ya Tanzania na Kenya na mpaka wetu kati ya Tanzania na Uganda na kati yetu na Zambia inaonekana hali siyo nzuri sana. Kwa hiyo, tumependekeza Serikali iweze kuyafanyia kazi maeneo hayo ili tuipe muda wa kuweza kutafuta uwezo zaidi na kushughulikia maeneo mengine katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu lililoelezwa na Kamati ni kuhusiana na ujenzi wa nyumba za Wanajeshi 6,064. Tumetakiwa kuliwekea utaratibu jambo hili ili kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo hayakupata kujengewa nyumba katika awamu ya kwanza yaweze kunufaika katika awamu ya pili. Lakini labda tu niseme, katika ile awamu ya kwanza tumeyaainisha maeneo na hasa vikosi vilivyopo katika Mikoa ile tuliyoitaja, ni Mikoa ambayo Wanajeshi wengi wanaishi katika maeneo ya uraiani, tukaona basi tuanze na Mikoa hiyo ambayo vijana wengi au Wanajeshi wengi wapo uraiani ili sasa tupate nafasi baada ya nyumba hizi kujengwa, Wanajeshi hao wapate nafasi kurudi katika Makambi.

Kwa mnasaba huo, utafanya hivyo hivyo katika awamu ya pili. Katika hizi ambazo takriban 4,000 tutazijenga katika yale maeneo ambayo hali ya majengo wanayoishi Askari hali ni mbaya sana, lakini pia katika maeneo ambayo Wanajeshi wengi wapo uraiani. Pengine hatutaweza

kumaliza tatizo lote kwa ujumla wake. Lakini nina uhakika tukifanya hivyo tutaweza kupunguza tatizo kubwa sana la upungufu wa nyumba kwa wanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la posho za wanajeshi, ambazo kwa muda mrefu kwa takriban kwa kipindi cha miaka mitatu zimekuwa haziongezeki, tatizo hili ni kweli; tukiangalia kwenye vifungu vya Wizara vinavyoeleza katika vitabu vya bajeti, tutaona dhahiri kwamba kuanzia mwaka 2010/2011, mishahara ilikuwa Shilingi bilioni 311, mwaka uliofuata mishahara ulikuwa Shilingi bilioni 354 na mwaka huu Shilingi bilioni 460. Lakini ukiangalia posho ya Askari mwaka huo 2010/2011 ni Shilingi bilioni 121.6, mwaka uliofuata Shilingi bilioni 121.6 na hatimaye mwaka huu ni kiwango hicho hicho.

Kwa bahati mbaya au nzuri, Wizara kwa kipindi chote hicho cha miaka mitatu tumekuwa tukiajiri Askari wapya. Ni dhahiri kwamba kutokana na kuongezeka kwa idadi hii ya Askari ambao tunawaajiri kila mwaka, bila shaka kiwango hiki cha posho kitakuwa hakiwezi kukidhi haja ya wanajeshi. Tayari tumezungumza na Wizara ya Fedha, najua tuna tatizo la upungufu wa fedha, lakini hoja tuliojenga Wizara ya Fedha imeisikia na Serikali hoja ambayo tumeijenga imeisikia. Kwa hiyo, tutaipa nafasi Serikali iweze kutafuta njia na namna ya kullitua jambo hili katika kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viongozi wa Vyama vya Siasa na Mashirika na Taasisi za Serikali kupelekwa kwenye Makambi ya JKT ili kupata mafunzo ya uzalendo na umoja. Sisi Wizara ya Ulinzi tunalikaribisha sana wazo hili na tunaupongeza sana ushauri huu, lakini sina hakika kwamba kwa mujibu wa Sheria tuliyonayo sasa kama tunayo mamlaka ya kuweza kuwalazimisha Viongozi wa Siasa, Mashirika ya Umma na Taasisi kujiunga na Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyofanya kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Mashirika ya Umma na Taasisi zake na hasa wale

wanaojali maslahi ya Taifa letu, mimi nina hakika na ninaomba sana wajitokeze kwa hiari yao, kama walivyofanya Waheshimiwa Wabunge kwa hiari yao.

Nampongeza sana Mheshimiwa Zitto Kabwe pale aliposema kitendo cha Waheshimiwa Wabunge 24 walioamua kwa hiari yao kuhudhuria Mafunzo Maalum ya Jeshi la Kujenga Taifa, wametoa funzo kwa Watanzania kwamba bila ya kujali nafasi uliyonayo katika jamii, viongozi ni lazima waweke mbele maslahi ya Taifa lao na wawe mfano kwa watu ambao wanawaongoza. Kwa maana hiyo, kama alivyosema, hapana shaka yoyote vijana ambao wanapaswa kwenda katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria kwa uamuzi huu uliofanywa na Waheshimiwa Wabunge 24, mimi nina hakika hakuna ambaye atasita kuchukua uamuzi huo, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge tayari wameishaonyesha njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wabunge ni wanasiasa, sisi wanasiasa kwa upande wa Chama kinachotawala na Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa upande wa Chama cha *CHADEMA*, nadhani tuendelee tu kuwashawishi viongozi wetu wa kisiasa, hasa viongozi maana viongozi wanayo dhamana kubwa ya kuwaongoza watu na kulinda maslahi ya Taifa letu. Sasa tuendelee tu kuwahimiza na kuwaeleza juu ya umuhimu wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga la Taifa. Mimi nina hakika watafika mahali wao wenyewe kwa hiari yao wataorodhesha majina yao na wakifanya hivyo jambo hili sisi kama Wizara ya Ulinzi tunalikaribisha sana kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijibu hoja za Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Mheshimiwa Mchungaji Natse. Mchungaji amesema maslahi ya Taifa lazima yazingatiwe kwa kupeleka wanajeshi katika *operation* za kulinda amani hasa katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, na ameuliza hapa maswali ya msingi sana. Masuala mawili, kwanza: Je, wanajeshi watakuwa salama hasa tukizingatia kwamba watu ambao

tuna mgogoro nao, Malawi na wao wanashiriki kwenye *operation* hii ya kulinda amani *DRC*?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, Tanzania itanufaika vipi kiuchumi kwa kushiriki katika *operation* hiyo. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa maelezo yake mazuri sana. Lakini na mimi nitatoa maelezo ya ziada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli upo mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi hasa katika eneo la Ziwa Nyasa, lakini kuwepo kwa mgogoro huu hakuna maana kwamba Tanzania na Malawi haziwezi kukaa meza moja na kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwape taarifa kwamba hivi karibuni wenzetu, ndugu zetu wa Malawi wanao mpango maalum wa kuanzisha *operation* ya kijeshi maalum katika nchi yao, na kwa bahati nzuri Tanzania imealikwa katika zoezi hilo la pamoja, pamoja na nchi nyingine jirani ikiwemo Zambia pamoja na Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lazima niseme kwamba *operation* hizi za Umoja wa Mataifa zinaratibiwa kwa utaratibu maalum, hata kama kuna uhamasa kati ya nchi moja na nchi nyingine, inakuwa vigumu sana hilo kuweza kuwafanyia hujuma Askari wanaotokana na nchi ambayo mna mgogoro. Nadhani kwa mazingira yalivyo, siyo rahisi sana jambo hilo kuweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, Tanzania itaweza kunufaika vipi kwa uamuzi huu wa kupeleka majeshi katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Watu wa Kongo? Napenda niseme mambo mawili. La kwanza, Tanzania inapeleka Majeshi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo kwa ajili ya kulinda amani chini ya Umoja wa Mataifa, uamuzi ambao uliridhiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kupitia Azimio lake 2098 la tarehe 28 Machi, 2013. Hii siyo mara yetu ya kwanza kufanya hivyo. Kwa muda mrefu Tanzania

tumekuwa tukifanya hivyo na kwa maana hiyo basi, tunadhani tunao wajibu huo wa kuendelea kufanya hivyo.

Pili, Umoja wa Mataifa utagharamia gharama zote za kuwahudumia wanajeshi pamoja na vifaa watakavyovitumia wakati watakapokuwa wanashiriki katika zoezi hili la *operation* ya kulinda amani. Kwa mnasaba huo basi, kwa ujumla nchi yetu itapeleka Majeshi ya kulinda amani Kongo ili kutekeleza wajibu wake huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la mwisho ambalo ni la msingi sana, sina hakika kama jambo hili linasaidia moja kwa moja katika maslahi ya uchumi, lakini nina hakika kwamba linasaidia sana katika maslahi ya usalama wa nchi yetu. Kama Wasemaji waliotangulia walivyosema, tukumbuke kwa muda mrefu hasa pale yanapotokea mapigano na migogoro ya kisiasa katika nchi jirani, mlengwa wa kwanza na mwathirika wa kwanza imekuwa ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka kilichotokea Burundi, tunakumbuka kilichotokea Rwanda, wakimbizi zaidi ya milioni mbili wakimbilia na kupewa hifadhi katika Mkoa wa Kigoma. Leo ukiwauliza watu wa Kigoma kwa kiasi gani wameathirika, bila shaka mimi sidhani kama watu wa Kigoma tena wapo tayari kurudia historia ile.

Kwa kadri hali inavyoendelea ya mapigano pale Kongo, Tanzania na Mataifa tunayozunguka Kongo kama hatukuchukua hatua hiyo ya kuwasaidia wenzetu, bila shaka tutakuwa tunaelekea huko tena. Ndiyo maana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikaona ishirikiane na Mataifa mengine chini ya Umoja wa Mataifa iweze kuchukua hatua hiyo na sisi sote tunakubali hapa kwamba upo uhusiano wa karibu sana kati ya Ulinzi na Usalama na maendeleo ya kiuchumi. Bila ya ulinzi na usalama, hakuna maendeleo ya kiuchumi. Kwa maana hiyo, tunaweza kusema hali hii inaweza kutusaidia sana na kutoa mchango kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Msemaji wa Kambi ya Upinzani amelizungumzia ni suala la maslahi na stahili za Wanajeshi lazima ziboreshwe na zitolewa kwa wakati.

Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ushauri wake Wizara imeusikia, Serikali imeusikia na tutaendelea kulifanyia kazi kwa kadri hali ya fedha inavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Natse amelizungumzia, ameuliza: Je, kuna migogoro ipi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wananchi? Ametaka niitaje migogoro hiyo ya ardhi ili Waheshimiwa Wabunge na wananchi waweze kuelewa. Nitachukua nafasi hii kueleza migogoro hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaeleza migogoro hiyo baadaye. Kwanza, tu niendeele na posho ya chakula kwamba haiongezeki. Suala hili tayari nimeshalieleza pale juu kwamba ni kweli Shilingi bilioni 121 zinazotolewa kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu, haionyeshi kuongezeka na bila shaka Serikali itaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililoulizwa lilihusu bajeti ya Wizara kwamba lazima iongezwe na Serikali inatakiwa ionyeshe dhamira ya dhati ya kulifanyia kazi jambo hili. Serikali bila shaka inayo dhamira ya dhati.

Naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hivi sasa inatekeleza mpango wa miaka 15 wa kuliimarisha Jeshi la Ulinzi la wananchi wa Tanzania. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akitoa mchango wa hali na mali katika kuhakikisha kwamba Wizara ya Ulinzi inatekeleza adhima hiyo.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na upungufu wa fedha unaotukabili, Serikali ina ya dhamira dhati kutekeleza jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lilihusu utunzaji wa silaha za milipuko, Serikali itoe fedha za ujenzi wa maghala kabla ya mwezi Juni, 30. Tayari nimeshalitolea ufafanuzi hapo juu kwamba Serikali imesikia jambo hili na Wizara ya Fedha tayari imeshatoa ahadi ya kutekeleza jambo hilo kabla ya tarehe hiyo. Nina hakika wataitekeleza ahadi hiyo kama walivyoeleza wenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Kamandi ya Wanamaji hawatumiki vizuri na kwa hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itoe zabuni za ukarabati wa vivuko na ujenzi wa madaraja.

Naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwa hoja hii ni ya msingi. Ni kweli wakati umefika sasa kwa Serikali kufanya juhudi za makusudi hasa zinapotoka zabuni zinazohusu vivuko, basi Kamandi yetu ya Wanamaji na Kamandi ya Wanamaji ni kweli inao Wahandisi wenye uwezo wa kuvikarabati vivuko hivyo katika kiwango kinachotakiwa, lakini hata kuhusiana na suala la ujenzi wa madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati niliwahi kuitembelea nchi moja lakini sitaitaja jina kwa sababu za kidiplomasia, nikawauliza kwa nini barabara zenu ni pana sana na madaraja yenu ni mapana kupita kiasi? Akaniambia wamefanya makusudi na Jeshi limeshirikishwa kikamilifu katika ujenzi wa barabara na katika ujenzi wa madaraja. Akasema wakati wa hali hatari itakapotokea, basi barabara hizi ambazo tunazona zipo zinatumika kama ni viwanja vya ndege kwa ajili ya ndege za kijeshi.

Sasa mimi nadhani hili ni jambo la msingi sana, sisi kama Taifa tunapaswa kulizingatia sana na Serikali kwa mnasaba huo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesikia na sisi Serikali tumesikia. Ipo haja ya kulitekeleza jambo hili kwa vitendo kwa maslahi ya Taifa letu.



Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa waweze kupewa kipaumbele kwa kupatiwa ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la msingi kwa sababu ni ukweli ulio dhahiri kwamba, vijana hawa si tu wanafunzwa masuala ya ufundi katika Jeshi la Kujenga Taifa, lakini pia wanapewa mafunzo maalum ya kutumia silaha. Tusipokuwa makini na jambo hili kuna siku vijana hawa wanaweza kuleta maafa kwa sababu vijana hawa wanafundishwa silaha. Kwa hiyo, tusipokuwa na mikakati maalum ya kuwaandalia mazingira ya kujajiri au kuajiriwa siku moja tunaweza kutengeneza majambazi watarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania tayari limeshachukua hatua. Tunao utaratibu maalum wa kuchukua vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na kuajiri katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Zamani tulikuwa na utaratibu wa kuajiri nje ya Makambi, lakini sasa hivi tumeanzisha utaratibu huo. Jeshi la Polisi linatumia utaratibu huo, Magereza linatakiwa nalo kutumia utaratibu huo na Uhamiaji wanatakiwa pia kufuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu letu kufanya hivyo. Namwomba na kumshauri Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kwa sababu yeye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha kwamba, vyombo vyote vya ulinzi na usalama vinatekeleza agizo hili, lazima vihakikishe kwamba vijana wa JKT wanapewa kipaumbele katika ajira katika vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni maeneo ya uzalishaji mali katika Jeshi la Kujenga Taifa lazima yaimarishwe na yaainishwe kwa sababu jambo hili litaweza kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi katika Taifa letu. Jambo hili ni jambo la msingi, nakubaliana naye na kama nilivyoeleza katika hotuba yetu ya bajeti, Jeshi la Kujenga Taifa limeshapewa agizo maalum la kuhakikisha kwamba

wanazalisha mbegu za kutosha kwa ajili ya kuendeleza kilimo, lakini pia kuzalisha chakula cha kutosha ili kuweza kutosheleza mahitaji ya Jeshi pamoja na kuuza ikiwezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalotukabili sasa hivi ni upungufu wa bajeti. Lakini nina hakika Serikali itafanya kila linaloweza kutafuta fedha ili tuweze kuwekeza katika jambo hilo muhimu na hasa nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge pale waliposema Serikali inapaswa kuweka uzito katika masuala yenye maslahi makubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama pendekezo nillilopendekeza kwenye bajeti lina ubaya wowote. Kwenye bajeti nilisema hivi, kwa kuwa Serikali haiwezi kukidhi mahitaji ya mtaji unaohitajika katika kuliimarisha Jeshi la Kujenga Taifa, hakuna ubaya wowote, basi kuyakaribisha Makampuni na Mashirika ya Watu Binafsi, wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi wale ambao wana nia njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani si vizuri fursa hii tukaanza kuifungia milango. Nadhani kuna haja kuwakaribisha watu hawa, lakini jambo la msingi Wizara yetu na watendaji tuwe makini katika kuwateua na kuwachagua wawekezaji ambao wanaweza kwenda sambamba ba mpango wa kuliimarisha Jeshi hasa katika dhamira hii ya kulifanya Jeshi la Kujenga Taifa liwe ni kitovu cha uzalishaji mali pamoja na eneo la kibiashara. Tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kulifanya jambo hilo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naikubali pia *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba pamoja na kuyafanya yote hayo umefika wakati basi Jeshi la Wananchi wa Tanzania liwe kielelezo cha usafi na uadilifu. Sina wasiwasi na viongozi wa Jeshi tuliokuwa nao, ni watu safi sana, ni watu weledi sana na ni watu wema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Waziri jukumu langu ni kuhakikisha kwamba, tunatekeleza dhamira hiyo.

Mimi kama Waziri, kama wenzangu hawa walivyo, taswira yao ni watu wazuri, ni watu wema, nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuhakikisha kwamba masuala ya uufisadi, rushwa, tunayapa kisogo na kama kuwaharibu basi pengine labda mimi Waziri ndiye ambaye naweza kuwaharibu. Lakini naomba niwahakikishie kwamba Jeshi letu linaongozwa na watu wasafi sana na watu makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la msingi ambalo Mheshimiwa Natse ameleleza kwenye hotuba yake, Jeshi la Kujenga Taifa lihusike kikamilifu katika kuandaa operesheni ya upandaji miti nchi nzima kwa kuwatumia vijana wa JKT. Jambo hili ni jambo la msingi sana na hatuna sababu ya kupuuza ushauri mzuri kama huu, ushauri ambao una maslahi makubwa kwa Taifa letu hasa katika kudumisha mazingira kwa ujumla wake, kwa hiyo, ni jambo ambalo tunapaswa kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na ushauri mwingine ambao tayari ameshautoa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wakuu wa Kamandi mbalimbali pamoja na vyombo vya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tutaufanyia kazi ushauri huu, kwa sababu ushauri huu ni ushauri mwema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto ameeleza mambo matatu ya msingi sana. La kwanza, ametuomba tusirudie tena makosa tuliyoyafanya mwaka 1994 pale tulipositisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Naomba tumhakikishie tu, kuwa tutazingatia ushauri wake. Waswahili wanasema: "Kujikwaa si kuanguka." Tumeteleza, tumenyanyuka, mimi nadhani kwa hapa tulipofika hatutaweza kurudia tena makosa ambayo tuliyoyafanya huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejifunza jambo moja. Sote hapa tunakubaliana kwamba, kuna mmomonyoko mkubwa sana wa maadili miongoni mwa vijana wa Tanzania. Ukiwasikiliza wazee, wazazi na viongozi mbalimbali wa kisiasa wanasema tatizo letu kubwa tuliacha mafunzo ya Jeshi la

Kujenga Taifa. Kutokana na Jeshi la Kujenga Taifa katika malezi, katika uzalendo bila shaka tunapaswa kulipa uzito unaostahili jambo hili lenye maslahi makubwa na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kila Kambi iwe ni kituo cha ufundi na akasema pengine tungeanzia na Kambi ya Mgambo ambayo yeye amepata mafunzo yake ya wiki tatu ya Jeshi la Kujenga Taifa. Sina tatizo na jambo hilo, jambo hili ni zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhakikisha kwamba mbali na mafunzo ya kijeshi ambayo vijana wetu wanapatiwa, tunahitaji pia kuwapatia mafunzo ya stadi za maisha na ufundi kwa ujumla wake. Kwa muda mrefu Makambi yetu yamekuwa yakifanya kazi hiyo, lakini nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kiwango cha weledi hasa katika masuala ya ufundi kiko chini sana kutokana na uhaba wa vifaa na wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tumeliona tatizo hilo. Tutafanya kila lililo katika uwezo wetu kuhakikisha kwamba tunapata vifaa vinavyokidhi mazingira ya ufundi katika karne hii ya 21 na kupata wataalamu wenye uwezo unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaeleze hatua ambazo tumeanza kuzichukua katika hatua ya awali. Hivi sasa nimewapa agizo Watendaji na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa kuandaa Waraka Maalum kwa ajili ya kuanzisha *Centre of Excellence* kwa ajili ya mafunzo ya ufundi. Kituo hicho kina uwezo wa kuchukua kati ya vijana 4,000 mpaka 6,000. Kazi hiyo inaendelea vizuri na tutakapokuwa tayari basi Serikali itatakiwa kutafuta fedha ili kutekeleza jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Serikali itaweza kukidhi mahitaji, tutafanya hivyo, lakini pia najua wako wafadhili hasa nchi marafiki ambazo zinatutakia mema pia zinaweza kutusaidia katika jambo hili, hatutasita kuchukua hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, tusiruhusu Wanajeshi kulalamika kuhusu maslahi yao. Sioni kama kuna neno naweza kuzidisha katika kauli hii ya msingi. Haki ni lazima ionekane, si kuwepo tu, lakini pia ionekane inatendeka. Kama mimi ninavyohitaji kulipwa maslahi yangu, nadhani na mtu mwingine hivyo hivyo anastahiki kulipwa haki na ujira anaostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haina pingamizi ya aina yoyote kuhakikisha kwamba Wanajeshi, si kwa sababu tu ya jukumu zito wanalolitekeleza katika Taifa letu, lakini kwa sababu tu haki za ubinadamu wanastahiki kulipwa malipo na ujira unaostahiki. Nchi yetu pamoja na umaskini wake, nchi yetu pamoja na tatizo tulilionalo la uhaba wa fedha, tutajitahidi kulipa uzito unaostahiki jambo hili, ili tuhakikishe kwamba Wanajeshi wanalipwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lazima walipwe maslahi yao kwa wakati ili tuweze kupunguza manung'uniko miongoni mwao. Tukifanya hivyo ni kwa maslahi ya Serikali kwani wakilipwa vizuri vijana hao wataweza kutekeleza wajibu wao na kwa maana hiyo manung'uniko haya yataondoka na kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa amezungumza mambo manne na nitayazungumza kwa ufupi sana. Ameniomba tuandae mazungumzo kati yangu mimi kama Waziri wa Ulinzi na wananchi wa Cheju ili kutafuta suluhu ya mgogoro ambao umedumu kwa muda mrefu katika eneo hilo. Nakubali rai ya Mheshimiwa Mbunge tutajitahidi kadri ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada tu ya kumalizika bajeti hii, namwomba Mheshimiwa Mbunge tukumbushane ili tuweze kutekeleza dhamira hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, matengenezo ya zana amesema ni muhimu. Wakati wa kuwasilisha bajeti yangu, nilisema wazi kwamba, suala la kupata zana na vifaa vya kijeshi ni jambo moja, lakini suala la matunzo ni jambo

lingine. Nilitoa rai kwamba, Jeshi la Wananchi wa Tanzania linapaswa kukarabati zana hizi kwa wakati ili tuweze kupunguza gharama za uendeshaji wa zana hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, askari wanaohamishwa hawapewi haki zao ipasavyo. Tatalifuatilia jambo hili na kulifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili tujue kweli askari hawalipwi maslahi yao, tutafanya hivyo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, katika baadhi ya Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa hakuna umeme, huduma za maji safi na hakuna vyoo vya uhakika. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge tualifanyia kazi jambo hili ili tuhakikishe kwamba, Makambi yanakuwa na vyoo vinavyostahiki, vyoo vya heshima. Pia Makambi hayo yaweze kupata huduma mbalimbali za umeme kwa sababu Kambi ya Ulinzi, haiwezi kukamilika kama haina huduma za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa sana niliposikia kauli ya Mheshimiwa Mariam Kasembe wakati alipokuwa akitoa mchango wake kwamba, kuna askari wa Jeshi la Kujenga Taifa hasa katika Kmbi ya Bulombora wanachangishwa fedha kwa ajili ya kununua mafuta ya jenereta ili waweze kupata huduma za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri jambo hili linanisikitisha sana, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote hawa wawili kwamba jambo hili tualifanyia kazi na kuchukua hatua ipasavyo na tutajitahidi ili tutakapokuja hapa katika bajeti ya mwaka unaokuja angalau tuwe na majibu ama tuwe tumelitatia kabisa jambo hili, ama tuje na majibu yanayoridhisha juu ya hatua mbalimbali ambazo tunazichukua katika kurekebisha matatizo hayo ya vyoo, maji safi na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mariam Msabaha amesema Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa wapate mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa sababu wakifanya hivyo watakuwa wazalendo na wakakamavu.

Tumeona Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi hiyo ya kuhudhuria mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa jinsi walivyokuwa wakakamavu. Kwa hiyo, bila shaka ushauri wako tumeusikia na Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wa kisiasa ambao hapa hawapo wataufanyia kazi ushauri huo wa busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mariam Kasembe, hali ya Bulombora ni mbaya sana na amependekeza niende wakati wa kufunga mafunzo hayo ili niweze kujionea mwenyewe juu ya hali inavyoendelea huko. Pia amesema nyumba haziko katika hali nzuri. Nimekubali ombi hili nitafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la hali mbaya ya nyumba, naomba nimhakikishie kwamba, katika nyumba 6,064 ambazo tumekusudia kuzijenga kuanzia mwaka huu wa fedha, JKT itapata mgao maalum kwa ajili ya Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Naomba nimhakikishie kwamba tutaanza na yale Makambi ambayo hali ya nyumba ni mbaya zaidi kuliko maeneo mengine wakati tukijipa muda kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ameeleza mambo manne ya msingi sana. Kwanza amesema nchi jirani tunazona zinajimarisha kiasi cha kutosha, zinanunua silaha nzito nzito na bahati nzuri sisi tunazona kwa sababu zinapita kwetu. Sasa ametuomba kwamba na sisi tujiandae.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wataalam wa mahusiano ya kijeshi wanasema ukimwona adui yako anakusanya silaha basi inawezekana kwamba anajiandaa kwa mapambano siku zinazokuja. Sasa hiyo, mimi kama Waziri wa Ulinzi ujumbe nimeupata, lakini nadhani na Serikali pia ujumbe imeupata kwamba na sisi tujiandae kwa hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Idara za Utafiti Jeshini ziendelezwe ili ziweze kujitegemea. Waasisi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania hii ndio iliyokuwa dhamira yao hasa

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tokea siku za mwanzo za uhuru. Ndiyo maana Serikali iliunda Mashirika kama Mzinga, Nyumbu na Suma JKT. Mashirika haya yaliundwa kwa dhamira hiyo ya kuweza kuwawezesha Wanajeshi kufanya utafiti katika teknolojia si kwa masuala ya kiulnzi tu na kijeshi, lakini mpaka kwenye masuala ya kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalotukabili ni upungufu wa fedha. Nimezungumza na Mameneja Wakuu wa Shirika la Mzinga, Nyumbu na Suma JKT, wameonesha wanayo nia na dhamira ya dhati ya kutekeleza azma hii ya kujitegemea, lakini jambo linalowakwamisha ni fedha. Sisi wenyewe ni mashahidi tukiangalia kwenye bajeti hii tutaona dhahiri kwamba utoaji wa fedha kwa Mashirika hayo umekuwa hauridhishi sana. Serikali tumelisikia, tunalichukua, tutalifanyia kazi ili tuweze kufikia dhamira hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Jeshi la Kujenga Taifa wapewe fedha za kutosha ili waweze kuongeza uzalishaji mali wa mazao ya kilimo na biashara. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwenye bajeti yangu nimelieleza jambo hilo kwa urefu. Jambo lililobaki tu hapa ni utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sote tunakubaliana kwamba, tunayo dhamira ya dhati na nia ya kuendeleza Suma JKT kuwa kitovu cha biashara na mazao ya kilimo, lakini jambo linalotukabili ni upungufu wa bajeti. Sasa tushauriane na kuelekezana jinsi gani tunaweza kupata mtaji huo wa shilingi bilioni 13 kama nilivyoeleza kwenye bajeti yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, ametuambia kwamba, viongozi wa kisiasa tujizuie na kauli zetu, kauli zetu zinaweza kuhatarisha amani na kuwapa vishawishi watu wengine wasioitakia Tanzania mema kuweza kupata nafasi ya kuchukua rasilimali zetu wakati sisi wenyewe tukiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati niliwahi kusema hivi, kadri Tanzania inavyoendelea kuvumbua rasilimali za kimaumbile ikiwemo gesi na mafuta, ndivyo itakavyoweza kutengeneza maadui ama wa dhahiri ama wa siri na kwa



maana hiyo nakubaliana na kauli ya Mheshimiwa Mbunge kuwa tujizuie kutoa kauli zinazoweza kuhatarisha amani, lakini si amani hatimaye kuhatarisha maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Deo Sanga ameniomba niende Makambako kuzungumza na wanakijiji pamoja na wananchi kuhusiana na tatizo la mgogoro wa mipaka uliopo kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wananchi. Nimeukubali ushauri wake, nitafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yatangazwe kwenye vijiji, lakini pia ajira zinazotolewa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Polisi, Uhamiaji na Magereza pia zitangazwe vijijini. Naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, nakubaliana nae kwamba iko haja ya mafunzo haya ya JKT kutangazwa ili wananchi wapate fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana kwa upande wa ajira zinazotolewa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza hatuwezi kuzitangaza kwa utaratibu huo. Kwa nini? Kwa sababu kuanzia mwaka juzi tumekubaliana sasa hivi wakati umefika na hata Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia bajeti hii wamelizungumza jambo hilo, kwamba wakati umefika vyombo vya ulinzi vianze kuajiri vijana wa JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mahali pekee ambapo tunaweza tukaajiri ni kwenye makambi ya JKT. Sasa wazo la kwamba tutoke sasa tukaajiri mitaani, nadhani hawa vijana ambao tayari wameshapata mafunzo ya JKT kwenye makambi, tutakuwa hatuwatendei haki. Kwa hiyo, nadhani ushauri huu una walakini kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Amina Clement, amesema Kijiji cha Unguja Ukuu na Kikungwe kimezungukwa tayari eneo hili ambalo lilikuwa linatumwa na jeshi kwa kulenga shabaha limezungukwa na wanakijiji wa eneo hilo. Sasa nasema Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itafute eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo zito kidogo kwa sababu mimi mwenyewe ni mwenyeji wa visiwa vya Zanzibar najua hali ya Zanzibar ilivyo. Zanzibar ni nchi ndogo sana, kuna uhaba mkubwa sana wa ardhi kama mnavyojua eneo hili la Unguja Ukuu lina historia ndefu sana. Tangu mwaka 1964 Serikali ya Mapinduzi iliwapa Jeshi la Wananchi wa Tanzania eneo hili kwa ajili ya kupigia shabaha na hakuna lengo lingine isipokuwa kuweka tayari wanajeshi wetu kwa ajili ya mapambano. Kwa sababu jeshi haliwezi kukaa tu hivi bila kufanya mazoezi kila mara. Mazoezi ya weledi lakini mazoezi pia ya kutumia vifaa vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa bahati mbaya wananchi ambao hawajui umuhimu wa kuwepo Jeshi la Ulinzi wamekuwa wakivamia eneo hilo pamoja na kwamba wamekuwa wakielezwa hivyo, tumeweka mabango, lakini bado wanalitumia eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anaposema tukatafute eneo lingine wasiwasi wangu ni kwamba, tutakapoamua kutafuta eneo lingine kuna matatizo mawili. Kwanza eneo hilo kwa udogo wa Zanzibar tutakwenda kulipata wapi wakati huu maana maeneo yote yameshavamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata kama tukilipata eneo hilo Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaweza kunihakikishiaje hata hilo tutakalolipata halitatoka kama lilivyotokea kwenye hili. Sasa nadhani wakati mwingine Waheshimiwa viongozi tuamue na wakati mwingine tunaambizana hapa katika Bunge kwamba, tufanye maamuzi magumu. Sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi nao wafanye maamuzi magumu. Tunahitaji Jeshi kwa ajili ya ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo maeneo yao yaendeleo kuheshimiwa. Sisi tutaheshimu maeneo ya wananchi. Narudia, Jeshi la Wananchi wa Tanzania litaheshimu maeneo ya wananchi na kama tutalazimika kuchukua eneo lolote la mwananchi kwa ajili ya shughuli za

ulinzi wa Taifa letu, tutamfidia mwananchi huyo haki yake kama inavyopaswa. Lakini na wananchi nao wajenge utamaduni na ustarabu wa kuheshimu maeneo ya Jeshi kwa sababu Jeshi hili lipo kwa ajili yetu. Labda kama Mheshimiwa Mbunge anasema kazi ya Jeshi sasa imekwisha tuko salama, hatuhitaji tena Jeshi? Nadhani si jambo jepesi kama anavyodhani yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari anielekeze tu wapi tunaweza kupata eneo hilo la kutosha kwa ajili ya kazi hiyo na akiniambia leo, basi tuko tayari kesho kuliacha eneo hilo. Kuna mtu mmoja wa Zanzibar aliwahi kunishauri jambo moja akaniambia kwa nini Waziri hamtafuti eneo kwenye Mikoa ya bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia Wazanzibar wakati mwingine ni watu wa ajabu sana. Sisi ndiyo wakati mwingine tunaosema Muungano unaongeza mambo, halafu wakati mwingine pia tunasema, mazoezi ya kijeshi kufanyika, tukatafute maeneo Tanzania bara. Sasa unaweza kuona namna gani wanasiasa mawazo yao yasivyokuwa na mtiririko mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameeleza suala la nyumba za Ubago ziko katika hali mbaya sana. Ni kweli najua jambo hilo. Lakini kama nilivyoeleza kwenye bajeti kwamba, tunayodhamira ya kuwajengea wanajeshi nyumba za kisasa. Tutaanza awamu ya kwanza nyumba 6,064 na awamu ya pili tutajenga nyumba zipatazo kama 4,000 hivi. Yote haya ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanajeshi wanaishi katika nyumba zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu askari wanaokwenda kozi moja, lakini malipo yao ya ujuzi yanatofautiana sana kati ya Koplo na Luteni. Labda nimfahamisha tu kwamba utaratibu wa Jeshi ni tofauti sana na wa raia. Haiwezekani askari mwenye cheo cha Koplo au Sajini aweze kuwa na mafunzo na Luteni. Luteni ni Afisa wa

Kijeshi, kwa hiyo mafunzo yake ni mafunzo maalum ya ukamanda. Kwa hiyo, sikuona uhusiano wa moja kwa moja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja litolewa iamuliwe)*

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

### **Fungu 38 – Ngome**

Kif. 1001 – *Defence Forces*

*Headquarters' Command...* Sh. 631,535,920,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa ajili ya kasma 221700, *food supply and services* ambayo inahusu pamoja na mambo mengine posho ya chakula kwa ajili ya wanajeshi kwa maana ya *ration*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limehojiwa na Kamati na Kambi ya Upinzani na katika mchango wangu wa maandishi na Wabunge mbalimbali. Katika majumuisho Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, tatizo hili limefahamika na litapatiwa ufumbuzi kwamba, kiwango cha *ration allowance* ni kile kile kwa miaka mitatu mfululizo wakati ambapo idadi ya wanajeshi imeongezeka. Sasa pamoja na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri ambayo yanaashiria kama vile jambo hili linaanza kutafakariwa kwenye mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ili lipatiwe ufafanuzi wa ziada; jambo hili lilihojiwa sana vile vile mwaka wa fedha uliopita. Wakati ule sababu ya kulihoji ilikuwa ni kwamba fungu la mishahara liliongezeka kwa shilingi bilioni 45, lakini fungu la posho likabaki pale pale. Safari hii fungu la mishahara limeongezeka kwa zaidi ya bilioni 100, fungu la posho limebaki pale pale. Kwa maneno mengine wanajeshi wanaongezeka, lakini posho ya chakula kiwango kiko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa jambo hili lilishafahamika tangu mwaka wa fedha uliopita, ni kwa nini tusipewe ufafanuzi wa ziada na Mheshimiwa Waziri wa Fedha sasa kwa kuwa jambo hili lilishafahamika; ni kwa vipi tutaweza kuwa na askari wengi namna hii ambao tumeshawaongeza kwa shilingi bilioni 143 *in total* na tukaendelea kuwapa *rationing allowance* kwa kiwango hiki hiki bila ongezeko kubwa sana la madeni ya askari yanayotokana na *rationing allowance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi na iwapo ufafanuzi hautaridhisha Mheshimiwa Waziri ni afadhali tui poteze ile shilingi moja tu, zibaki bilioni 126.6/- tuweze kutoa ufafanuzi wa hakika wa upembuzi wa jambo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyika, eneo hilo bado si la kutoa shilingi. Mheshimiwa Waziri afafanuzi!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mnyika kwamba, jambo hili la posho za askari lilizungumzwa mwaka 2012/2013 na ukiangalia bajeti za nyuma 2010/2011, mpaka mwaka huu ukiangalia mishahara imekuwa ikizidi, lakini posho za askari zimekuwa kwenye kiwango hicho hicho. Tunapokutana na watalaam wa Wizara ya Fedha hoja yao kubwa ambayo wamekuwa wakieleza ni kwa kiasi gani tumeweza kuathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna jambo ambalo tumekuwa tukijadiliana nao kwamba, kasma hii tunayoitumia kwa ajili ya kulipa askari posho, pia inatumika kwa ajili ya *TPDF Stock* yaani akiba ya vyakula ambavyo ni vikavu kwa ajili ya shughuli za *operation* na za kivita pale inapotokea. Sasa ikifika wakati ambapo tunaajiri vijana wavya haijaingiziwa fedha, kwa hiyo, fedha za kifungu hiki kinatumika kuwalipa vijana hawa ili kuhakikisha kwamba kila askari analipwa posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni vizuri nikaeleza kwamba, posho hii tunayozungumza hapa imekuwa ikileta utatanishi kidogo. Wengine wanadhani fedha hizi ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya askari. Fedha hizi ni kwa ajili ya chakula cha askari anapokuwa katika maeneo ya kazi. Si kwa ajili ya kuhudumia familia yake, hizi ni kwa ajili ya shughuli maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya utafiti huko nyuma tukagundua kwamba askari wengi wanaanza kuzitumia hizi fedha kwa ajili ya shughuli za kifamilia na matokeo yake wanaacha shughuli za ulinzi wanaanza sasa kwenda kutafuta vyakula visivyokuwa na usalama sana. Tukasema huu si utaratibu mzuri, sasa tukaandaa utaratibu maalum ili vijana hawa waweze kupewa fedha hizi kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nisisitize fedha hizi si kwa ajili ya kuendeleza familia. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuhakikisha askari anapata chakula cha kutosha kwa sababu kazi za Jeshi ni kazi ambazo zinahitaji sulubu sana na kwa maana hiyo wanahitaji kula vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niwahakikishie kwamba kwa muda mrefu huo tunaendelea kujenga hoja Wizara ya Fedha na nina hakika kwa sababu viongozi wa Wizara ya Fedha wako hapa, nadhani hoja hii wameiona na bila shaka wataweza kuitafutia ufumbuzi unaostahiki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Hapa Mheshimiwa John Mnyika aliendelea kusimama ili aweze kuchagua)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Mnyika mshahara wa Waziri uko mbele kule. Hapa tunauliza mara moja tu. Tunaendelea, Katibu!

Kif. 1007 - *Land Force Command* ... .. Sh. 8,066,929,000/=

**MWENYEKITI:** Kuna Wabunge watatu, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Lugola. Tuanze na Mheshimiwa Suzan Lyimo!

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naomba ufafanuzi kwa ujumla, naona kwamba bajeti katika kifungu hiki, ukiangalia bajeti ya mwaka huu na mwaka jana vifungu vyote, isipokuwa 220500 na kifungu 230200 *actually* fedha zake zinalingana kabisa. Naomba kujua ni kwa sababu imekuwa namna hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kama umempata Mheshimiwa Mbunge!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, mwaka uliopita zinaonekana hizo shilingi bilioni 10 na hapa zinaonekana hizo hizo. Sasa hili ni ukomo wa bajeti kama inavyoonekana, kwa hiyo, "tunakata pua tunaunga wajiji."

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 220600 *clothing, bedding, footwear and services*. Nataka tu maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kama unavyoona hapo, fedha zinazotengwa ni ndogo mno, nadhani imewekwa kama *figure* tu kwa sababu kimsingi haiwezi kutosha mahitaji ya nguo na viatu kwa wanajeshi wetu na kuna tatizo kubwa sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna madai, lakini mengine hatuwezi kuyasema kwa sababu *M23* watatusikia. Lakini kuna madai ya Wanajeshi kukatwa fedha kwenye pensheni zao kwa gharama ambazo ni za nguo wanazonunuliwa na Jeshi. Kwa hiyo kwanza tuna tatatizo nguo hazinunuliwi, wanajeshi hawana nguo hasa wanajeshi wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, zile chache zinazonunuliwa ambazo labda atapata sare moja kwa miaka mine, wanakatwa kwenye pensheni zao. Sasa naomba maelezo ya Waziri na ukiangalia hiyo bajeti hapo ni ndogo sana. Hata ukienda kwenye *Navy, Air force* na *Land force command*, hili ni tatizo kubwa sana ambalo tumeliona Jeshini.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge hapa, fedha zilizotengwa shilingi milioni tano kwa ajili ya sare, fedha ambazo hazitoshi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi fedha zilizowekwa hapa kwa ajili ya sare. Hizi ni sare maalum za sherehe, lakini sare za kawaida aangalie kwenye fungu kuu la Ngome, ziko fedha kwa ajili ya kununulia sare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na askari ambao wamekuwa wakikatwa fedha binafsi kwa ajili ya kununuliwa sare. Jambo hili sijalisikia, lakini kwa kuwa nimelisikia sasa, naomba nikuhakikishie na ukubali kwamba nitalifanyia kazi ili kujua ukweli wake na kuchukua hatua zinazostahili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* 1007, kifungu 220300, kinachohusiana na mafuta, *oil*, pamoja na vilainishi. Inakuwaje bajeti ya mwaka jana ifanane kabisa na Bajeti ya mwaka huu ili hali masuala ya magari kwa matumizi ya mafuta lazima tu kwa shughuli za mwaka jana zisiwe sawa na za mwaka huu. Sasa nataka ufafanuzi hizi *figures* sijui wamezifikiaje. Nataka ufafanuzi.



**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lugola, lilishaulizwa na Mheshimiwa Susan Lyimo na limeshajibiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 - *Air Defence Command* ... .. Sh. 6,207,507,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1009 - *Navy Command* ... .. Sh. 2,709,790,000/=

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa Zitto peke yake.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma ndogo ya 410400, nataka nipate maelezo ya Waziri, mwaka jana iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilitoa mapendekezo hapa kuhusiana na Jeshi letu kuimarisha *Navy*, kwa ajili ya kusimamia ulinzi kwenye Bahari kuu, kipindi hiki ambapo kuna shughuli nyingi sana za utafutaji wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makampuni ya Mafuta yanatumia fedha nyingi sana kulipa makampuni binafsi ya ulinzi ambayo yanaingia na silaha kali ambazo zinaweza kuhatarisha amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifahamu kwamba, pale *acquisition of specialized equipment* ndiyo tumeanza hiyo kazi? Kama siyo, kifungu kiko wapi kwa sababu tunapaswa kufanya jambo hilo sasa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana hiki kifungu ambacho Mheshimiwa Mbunge amekisema 410400, *acquisition of specialized equipment* hapana, hivi ni vifaa vya zimamoto na kamera kwa ajili ya kupigia picha na utambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na suala lake kuwa, tumejiandaa vipi kwa sababu ni kweli kwamba, hivi sasa makampuni ambayo yanatafuta mafuta na gesi yanatumia kampuni binafsi za ulinzi na jambo hili limetokea kwa sababu hatuna meli za kutosha kwa ajili ya kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kuwa, hivi sasa tumepata msaada wa meli mbili ambazo tunaendelea kuzifanyia ukarabati na kuziweka katika hali nzuri. Nina hakika baada ya kufika mwishoni mwa mwaka huu, suala hilo la ulinzi ambao linafanywa na makampuni binafsi tayari Jeshi la Wananchi wa Tanzania litachukua nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi katika kipindi cha mpito nimezungumza na Waziri wa Nishati maana suala hili liko kwake, lakini kuzungumza na Viongozi wa Jeshi kuhakikisha kuwa makampuni binafsi ambayo yanaendelea na ulinzi ni lazima kwao kuhakikisha kuwa wanashirikiana na Jeshi la Ulinzi ili liweze kudhibiti aina ya silaha ambazo zinatumika katika zoezi hilo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 1010 – Military Hospitals... ..Sh. 2,495,227,000/=*

**MWENYEKITI:** Nimeona Wabunge watatu Mheshimiwa Christowaja, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Sabreena.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kwenye kifungu 220400, kuhusu *Medical Supply and services* inaonesha kuwa fedha zilizotengwa mwaka 2012/2013, ni sawa na zilizotengwa kwa bajeti ya mwaka huu 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivi kwa sababu hospitali nyingi za Jeshi zimekuwa na matatizo makubwa sana

ya madawa, hata Wanajeshi wenyewe wanakuwa hawapati *service* nzuri za dawa na mara nyingi wamekuwa wakijinunulia dawa hizo. Pia izingatiwe kuwa hospitali hizi za Jeshi hazina migomo kwa hiyo, ikitokea hospitali za Serikali za uraiani zimegoma wagonjwa wengi hukimbilia hospitali za Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama inafikia mahali Wanajeshi wananunua dawa wakati ni haki yao ya msingi kupewa dawa, ni kwa nini fedha hizi hazijaongezeka mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christowaja *uli-declare interest?* Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa tunajua sana umuhimu wa hospitali hii ya Kijeshi kuwahudumia raia, Wanajeshi Wastaafu na Wanajeshi ambao wako katika Utumishi, tunajua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Waziri hatuna hiana yoyote ya kuwanyima askari wetu hawa huduma za matibabu, lakini hii ndiyo hali halisi ya bajeti tuliyokuwa nayo. Kwa hiyo, tumepanga hapa na pale kwa mujibu wa kiwango ambacho tayari tumetengewa. Nina hakika tukipata fedha nyingi zaidi mwakani na *Inshallah* tutaongeza fedha nyingi zaidi kuliko hizi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali ambalo Mheshimiwa Christowaja ameliuliza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sungura!

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika tayari swali limeshapatiwa majibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *The National Service...* ... ..Sh. 187,301,634,000/=

**MWENYEKITI:** JKT nimewaona watatu; Mheshimiwa Lugola, Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Suzan Lyimo. Mheshimiwa Lugola!

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo *subvote* 1002, Kifungu 220900, Mafunzo Nje ya Nchi, naona hii milioni tano mafunzo nje ya nchi si inashia nauli tu hii? Naomba kujua kama kweli kuna dhamira hapo ya kupata mafunzo nje ya nchi, hizi milini tano zitatoshwa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tunarudi pale pale, hali halisi ndiyo hiyo, kiwango cha fedha tulichonacho ndiyo hicho. Kama nilivyosema, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tukipata fedha nyingi tutatenga nyingi zaidi kuliko hizo. Kwa hiyo, hiki ndicho kiwango tulichotenga kulingana na ukomo wa bajeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo!

**MHE. SUZAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kasma ndogo 220400, *Medical Supplies and Services*. Wakati Waheshimiwa Wabunge wanachangia wameelezea masikitiko yao kuwa, Wanajeshi wetu au wale wanaokuwa katika Mafunzo ya Kijeshi wamekuwa wakipata shida kubwa sana ya madawa, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie na atuahidi kuwa pamoja na kwamba fedha hizi zimeongezeka hadi bilioni moja. Je, anatumhakikishia kuwa madawa haya yatakuwa yanafika kwenye kambi hizi kwa wakati ili wale wanaokuwa katika mafunzo waweze kupata huduma hii adimu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutajitahidi fedha hizi ziweze kufika kunakostahili. Kama nilivyoahidi wakati nilipokuwa nikihitimisha majumuisho ya hotuba yangu hapa nilisema, mimi na wenzangu tutajitahidi kuwa waadilifu ili kuhakikisha kuwa tunatekeleza wajibu wetu ipasavyo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie na atuamini kwamba tutalifanyia kazi jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, program hii ina shilingi bilioni 187 pale kwenye *total sub-vote* chini kabisa. Pale Mgambo JKT kuna tatizo kubwa sana la gari la wagonjwa, inabidi watu wakiumwa kama ni askari au wagonjwa pale gari ya Mkuu wa Kikosi ndiyo ibebe wagonjwa kuwapeleka Muheza au kuwapeleka Tanga Mjini kama wanatakiwa kwenda Tanga Mjini na kuna gari moja tu na tumeomba gari la wagonjwa kwa muda mrefu sana pale, naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie katika hizi fedha *ambulance* ya *Dispensary* ya Mgambo JKT iko humu kwenye hizi pesa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, safari ijayo Wabunge wote waende kwenye kambi moja hutapata tabu sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amezungumza kwa ujumla fungu lote na anauliza katika fungu hili lote, kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya gari la wagonjwa katika kambi ya Mgambo. Nasema hapana, lakini *concern* yake tumeisikia na uongozi maana yake ni kutafuta suluhu ya matatizo yanayozikabili Taasisi zetu. Kwa hiyo, tutafanya hivyo na kuliangalia ili tuone namna gani tunaweza kulitua jambo hili pamoja na kuwa fedha hapa hazipo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

*Kif. 1001 – Administration and Human*

*Resources Management... ... Sh. 16,678,374,000/=*

**MWENYEKITI:** Sasa hapa ndiyo nakwenda na ile orodha yangu kwa ule utaratibu wetu wa Kikanuni, nitaanza na Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Hamad Rashid ajiandae. Tuendeleo Mheshimiwa Diana na wengine nitawataja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopita tuliambiwa hapa jinsi Sera ya CCM inavyotekelezwa na Serikali yake kwa kuongeza kujenga vituo vya JKT vipya na vingi nchini kikiwepo kituo cha Sandawanda, Manyoni na kituo cha Ndago, Iramba, lakini katika bajeti hii sijaona mkakati wowote au hela yoyote iliyotengwa kwa ajili ya mpango huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi kuhusu Makambi mapya ya JKT!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kasma hii hakuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa Makambi mapya, fedha hizo zitaonekana wakati tutakapojadili fungu linalohusika, kasma ya maendeleo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika kujenga uhusiano baina ya raia na kambi zilizoko kwenye maeneo pale Wawi, Mheshimiwa Waziri alifanya ziara, lakini bahati mbaya Wizara yake akaikatisha hakuweza kuonana na viongozi ambao tuliwachagua kukutana nao, akiwemo Mzee Hamis Juma Mkadala katika matatizo ambayo yametokea. Je, ziara ile ataikamilisha lini ili tuweze kumaliza lile tatizo ambalo lipo baina ya askari wetu na wananchi pale? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mimi na Mheshimiwa

Mbunge Mheshimiwa Hamad Rashid tulikubaliana twende kwenye Jimbo lake ili tuweze kuzungumza matatizo mbalimbali yanayowakabili Wanajeshi na wananchi wanaozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya siku ambayo nilipanga kwenda kwenye eneo hilo yeye mwenyewe hakubahatika kuwapo na yule mzee nilipokwenda niliambiwa kuwa alikwenda kwenye shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa niko tayari sasa, nafikiri yeye apange katika kipindi hiki ambacho tuko hapa Bungeni kama anadhani kuwa kuna siku tunaweza tukafanya hivyo, pengine tufanye hivyo, niko tayari kwa jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge yote inalenga kuwa ajira za Zimamoto, Magereza, Polisi, Uhamiaji, Jeshi la Wananchi pamoja na Walinzi wa Wanyamapori na pia wenye Makampuni ya watu binafsi ya Ulinzi, vijana wote waajiriwe kutoka JKT. Sasa Serikali inaona kigugumizi gani kutamka hapa bayana kuwa kuanzia sasa ni marufuku kuajiri mtu yeyote asiyepitia JKT? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy nilifikiri utasema kuanzia sasa na Wabunge nao lazima iwe JKT ni lazima.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge wazee tulishapitia mgambo, mimi binafsi nishapitia Mgambo miezi sita, kwa hiyo, JKT kwangu ni kama cha mtoto. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiona hoja ya Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Keissy, unajua jambo hili linagusa Taasisi

na Wizara nyingi ambazo zingine sina mamlaka nazo za moja kwa moja, lakini niliyokuwa na mamlaka nayo ni mawili; JKT na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni lazima wahakikishe na wenyewe wananisikia, kuwa, wanaajiri moja kwa moja kwa kupitia vijana wa JKT. Lakini kwa vyombo ambavyo viko Wizara ya Mambo ya Ndani, mimi ni Mwenyekiti wa Komandi ndogo ya Ulinzi na Usalama ya Baraza la Mawaziri na Mheshimiwa Waziri Nchimbi ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ananisikia kuwa, kuanzia sasa Jeshi la Polisi, Magereza na Zimamoto wahakikishe nao vile vile kama Jeshi lazima waajiri moja kwa moja kama tulivyokubaliana kupitia Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Wanyamapori, Taasisi ambayo iko kwenye Maliasili na Utalii nafikiri Waziri na Serikali inasikia, nina hakika kuwa, tumelisikia na Serikali itaufanyia kazi ushauri huu na nadhani ushauri huu una maslahi kwa Taifa letu na kwa hiyo ni lazima tuutekeleze.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu imezungumzwa sana, lakini bado ningetaka kupata hali halisi ya mkakati wa Serikali na Wizara husika, suala la mgogoro wa ardhi limezungumzwa sana kwenye hotuba yake mwenyewe Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba ya Kamati na kwenye hotuba ya Upinzani. Lakini ukiangalia hii migogoro kati ya Wanajeshi na wananchi haileti afya kwa sababu inazuia maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini migogoro hii nataka kuizungumzia katika nyanja mbili; kwanza, kwenye mipaka yetu, kuna maeneo mengine yako kwenye maziwa, kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika, barabara nzuri hakuna na vyombo vya kwenye maji havipo, lakini unakuta watu kutoka nchi jirani wanaingia na kuleta mgogoro na walinzi wetu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tatizo la mipaka baina ya Kambi za Jeshi na wananchi waliokuwa maeneo



jirani, kambi zilijengwa mbali sana na wananchi, lakini kutokana na idadi ya watu kuongezeka na kufuata mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine liko ndani ya wanaostaafu kujenga pembeni mwa zile kambi kwa kuwa hakuna alama zozote zinazoonesha mipaka halisi. Sasa hii haileti hali nzuri katika nchi na tumeona matatizo mengi Nachingwea kule kwenye Kambi ya Majimaji, ukienda pale Dar es Salaam, Gongu la Mboto na Mbagala na tumeona madhara ambayo wananchi wamekutana nayo kutokana na kambi kuwa jirani na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kuna matatizo mengine ya mipaka ambayo siyo ya kwenye kambi yenyewe, kuna tatizo la mpaka wa Kigamboni kwenye Mikadi *Beach*, Jeshi liliomba lile eneo, lakini hadi leo eneo lile halijarudishwa kwa mwenyewe na bado limekuwa na migogoro. Je, Serikali inasema nini katika hili?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii kujibu la Mheshimiwa Vullu kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama nilivyosema kwenye hotuba ya bajeti, iko migogoro mingi sana kwenye maeneo mengi zaidi ya 80 hivi kati ya Jeshi na wananchi na sababu iko dhahiri sana kwamba thamani ya ardhi hivi sasa imeongezeka sana kwa ajili ya shughuli za kilimo na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kadri ardhi inavyoendelea kuongezeka thamani ndivyo tunavyoweza kushuhudia mambo haya. Kwa maana hiyo basi Wizara yangu tumesema kuwa tutalipatia ufumbuzi na njia moja ni kuhakikisha tunayapima maeneo haya ili tuweze kujua mipaka yetu na mipaka ya wananchi tunayopakana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala ambalo Jeshi wameliomba, lakini kwa muda mrefu hawajapatiwa eneo hilo tutalifuatilia jambo hilo ili tuweze kujua ukweli wake haraka iwezekanavyo.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Moja ya majukumu ya majeshi yetu ni kulinda mipaka yetu, lakini kuhakikisha pia afya za askari wetu zinaimarika na zinakuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango mingi ambayo imetolewa hapa Bungeni pamoja na wa kwangu, katika Makambi haya ya JKT ambayo sasa kwa mujibu wa Sheria vijana wetu wanaomaliza kidato cha sita wanajiunga kwa maelfu, yako matatizo ambayo yamejitokeza yapo makambi mengi ambayo huduma hazijaimarishwa zikiwemo huduma za afya, huduma ya maji pamoja na usafiri wa lazima kama *ambulance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lipo kwa kiwango kikubwa sana katika Kambi ambayo nilikuwepo 835 KJ. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi au muda mrefu kuhakikisha kwamba matatizo haya yanatatuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusu barua ya waasi wa Congo (*M23*) kwa nchi yetu na bahati mbaya sana barua hii imepitia hapa Bungeni. Lakini niseme siku zote Askari hatishiwi nyau. Je, Waziri atakuwa tayari kumwomba Amiri Jeshi Mkuu pale waasi hawa watakapoleta matatizo zaidi, *platoon* ambayo ipo hapa Bungeni ambayo na mimi ni *Platoon Sergeant* niwe mstari wa mbele kwenda kupambana na waasi hao? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Iddi Azzan, Mpiganaji wa Jeshi la Akiba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika baadhi ya makambi yapo matatizo ya vituo vya afya, uhaba wa maji safi, umeme na usafiri. Mpango wa muda mfupi kwa kupitia bajeti ya mwaka huu tutahakikisha kwamba, tuweze

kupunguza ukubwa wa matatizo haya yaliyoelezwa. Nina hakika kwamba kwa kiwango cha fedha kilichotengwa hatutaweza kuyamaliza yote kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kipindi cha mpito tutaangalia, ikiwezekana tuweze kutafuta sasa suluhisho la kudumu. Kwa mfano, tutafanyia tathmini ya umeme ili tuweze kujua maana miradi hii ya umeme gharama zake ni kubwa sana, tujue itagharimu kiasi gani, ili tuweze kuchungulia huko Serikalini tuone wanaweza kutusaidia namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la *M23* kwamba *Platoon* iliyopo kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lipewe ruhusa kwenda kupambana na waasi hawa wa *M23*. Hili ni Jeshi la akiba, kwa hiyo, naomba wasubiri kwanza, tutalitafakari na wakati ukifika tunaweza tukafanya hivyo. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Na ni lazima waombe ruhusa kwa Spika kwanza.

**MHE. KABWE Z. ZITO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana la wastaafu wa zamani wa Jeshi kabla ya mwaka 1997. Hii imeathiri Askari wa chini mpaka wa juu. Kwa mfano, leo Jenerali au Meja Jenerali au Brigedia Jenerali au Kanali anayestaafu, malipo yake ya pensheni ni bora zaidi kuliko waliostaafu kabla ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa sana kiasi kwamba, hata baadhi ya wazee wetu ambao wametumika katika Jeshi, utumishi uliotukuka kama akina Jenerali Sarakikya wanahangaika sana na pensheni ndogo. Wastaafu wengi sana wa Kijeshi wa ngazi za chini ndiyo wanahangaika vibaya mno, wanalipwa elfu ishirini, elfu hamsini *maximum* tofauti na wanaostaafu sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiuliza unaambiwa kwamba sheria ni tofauti, kwa hiyo, sheria ilivyotungwa haiwezi ikaanza nyuma. Lakini Sheria hii ya Jeshi ndiyo

ambayo haianzi nyuma, Sheria ya Viongozi wa Kisiasa ilianza nyuma. Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999, *Public Leaders Benefit Act*, ilienda ikawachukua akina Mwalimu, akina Kawawa na wa nyuma wote, lakini hii ya Wanajeshi inaanzia 1997 kuja mbele, nadhani hii siyo haki kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba, Wanajeshi wengi ambayo wanahangaika ni wale ambao walipigana vita ya Uganda na kuiletea heshima nchi yetu. Je, Waziri haoni sasa umefikia wakati kuwianisha mafao ya Wanajeshi wa zamani na Wanajeshi wa sasa, wote wawe *treated* sawa sawa ili kutoa heshima kwa wanajeshi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata majibu ya kuridhisha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, nitachomoa shilingi yake. Kwa hiyo, naomba nipate majibu ambayo yataridhisha, tuweze kuwatetea wastaafu wetu katika Jeshi ili watu wengine wajitoe zaidi katika kufanya kazi za Jeshi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba, wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania hasa hawa Majenerali ambao wamestaafu kabla ya mwaka 1997, mafao yao ni madogo sana. Kwa hiyo, anasema anapouliza anasema anapouliza anaambiwa kwamba sheria haiwezi kutumika nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tatizo siyo hilo, tatizo lililopo dhahiri ni kwamba, nafikiri taratibu na viwango vya mishahara kwa sababu mishahara ambao Jenerali analipwa leo siyo sawa na ule ambao Jenerali alilipwa mwaka 1990, sasa utakapotumia hesabu yoyote watu hawa hawawezi kulipwa katika kiwango kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa sababu ya ubinadamu na hawa watu wametumikia Jeshi letu kwa heshima kubwa na utifu wa hali ya juu sana. Serikali imesikia,

tutatazama sheria kama inaweza kuturuhusu mahali Fulani, lakini tatizo langu nadhani siyo sheria, tatizo langu ni viwango vya mishahara, labda tuweze tu kutafuta namna ya kuwasaidia wazee wetu hawa ambao wametumikia nchi hii kwa heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo sina tatizo nalo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa askari wa chini inawezekana tatizo likawa ni viwango vya mishahara, lakini kwa askari kwa maana ya majenerali pensheni zao zinaendana na mishahara ya waliopo hivi sasa. Kwa mfano, Mkuu wa Majeshi Mstaafu atalipwa pensheni yake kwa mwezi asilimia 80 ya mishahara anaoupata Mkuu wa Majeshi wa sasa hivi. Kwa hiyo, ningetarajia kwamba Wakuu wa Majeshi kabla ya mwaka 1997 pensheni zao za mwezi zingekuwa ni bora zaidi kama ambavyo wanaostaafu sasa hivi. Hilo ni kwa ngazi ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ngazi ya chini nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba, inabidi liende likaangaliwe ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kuwasaidia hawa askari wetu. Lakini pia tufikirie, tatizo kubwa ninaloliona kwenye mfumo wa pensheni kwenye majeshi yetu ni kwamba, wanajeshi siyo wanachama wa mfuko wowote ule wa pensheni. Wanajeshi wanalipwa pensheni kutoka kwenye bajeti, kwa hiyo, hakuna fedha ambayo imetengwa maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kila mwaka tunakaa kwenye bajeti, tunatenga, ndiyo maana tunakuwa na woga wa namna gani ambavyo tutawalipa pensheni. Nadhani kuna haja ya kuangalia hata kama *contribution* yao itakuwa ni kidogo, isiwe *ten percent* kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine au *five percent* kama ilivyo kwa wafanyakazi wa *PSPF*, tunaweza tukaweka *one percent or two percent*. Lakini kuwe na *contributory scheme* ambayo itamfanya mwanajeshi atakapomaliza apate pensheni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kupitia hiyo Mifuko ni rahisi kuwaandalia maisha ya ustaafu, kwa maana ya Mifuko inaweza ikawajengea nyumba kutokana na pensheni zao. Kwa hiyo, naomba tuliangalie hili tuone namna gani ya kuboresha mfumo wa pensheni kwa wanajeshi wetu ili wasihangaike wanapokuwa wamestaafu.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo hujatoa shilingi sasa?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nashukuru, amekupa ushauri Mheshimiwa Waziri unasemaje kuhusu ushauri huo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mbunge mawazo yake ni mazuri sana. Busara na hekima ya namna hii ni mwendawazimu tu ambaye anaweza akaipuuza. Sisi Serikali tumeisikia. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - Finance and Accounts...	Sh. 247,166,000/=
Kif. 1003 - Policy and Planning...	Sh. 492,366,000/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit...	Sh. 148,432,000/=
Kif. 1005 - Procurement Management Unit...	Sh. 113,943,000/=
Kif. 1006 - Legal Services Unit...	Sh. 46,532,000/=
Kif. 1007 - Government Communication Unit...	Sh. 108,848,000/=
Kif. 1008 - Military Tender Board Unit...	Sh. 0
Kif. 1009 - Independent Telecommunication Network...	Sh. 85,118,000/=
Kif. 2001 - Industry, Construction and Agriculture...	Sh. 635,018,000/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Military Research and Development...* ... .. Sh. 301,599,000/=

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Nipo kwenye fungu la *Military Research and Development*. Kama tunavyojua kabisa kwamba, tunataka kujenga Jeshi la kisasa, ukienda kwenye kasma ndogo ya *training foreign* ya 220900, tunaona hapa kuna upungufu wa fedha kutoka milioni 21 kwa mwaka wa fedha uliopita kwenda mpaka milioni saba. Tunaposema tunataka kujenga Jeshi la kisasa ni kwamba, lazima wanajeshi wetu wafanye *research* katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa mfano mzuri, tumeona hata wakati wa watu North Korea wakifanya mazoezi, hata ukiangalia mwendo wao wa haraka ni *quite different* na wa kwetu. Kwa hiyo, tunahitaji kuwaongezea fedha. Nataka tu busara za Waziri, je, kwa sababu bajeti ya Kamati bado ipo kwenye *process*, haoni kwamba kuna umuhimu wa kuongeza fedha kwenye kifungu hiki? Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dhana ambayo nadhani si sahihi hasa tunapotaka kujenga Taifa linalojitegemea. Yapo mawazo kwamba mawazo mazuri na fikra mbalimbali za kisayansi ni lazima zifanyike nje ya nchi, siamini hivyo. Ukiangalia hapa kwenye fungu la ndani la mafunzo kunaonekana kwamba kuna fedha ambazo si haba, kwa hiyo, mafunzo mengi yataelekezwa ndani zaidi kuliko nje ya nchi. Pale haja itakapotokea tunaweza tukafanya hivyo kwa kiwango kidogo sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - *Building Construction Unit...* ... .. Sh. 66,649,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2004 - *Estate MGT and Development*

*Unit... ..Sh. 176,450,000/=*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wawili, tuanze na Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, niko kwenye kasma ya 220100, *Office and general supplies and services* ambayo imepanda kutoka mwaka jana shilingi milioni 5.6 mpaka mwaka huu shilingi milioni 28.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maoni yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ambayo ilikuwa na Wabunge wa pande zote, ukurasa wa saba Kamati ilionesha kwamba haijaridhishwa au haijapata maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Serikali juu ya ongezeko hili la pesa. Kwa kuwa, Kamati haikupata maelezo ya kuridhisha ikapendekeza kwamba, pesa zibaki zile zile za mwaka jana milioni 5.6 na Kamati ikapendekeza milioni 22.8 zilizoongezeka, zihamishwe na zipelekwe kwenye kasma nyingine hapo chini, kasma 227500, *Other supplies and services* ili kuongeza pesa ya kiwango cha upimaji wa ramani kwenye maeneo yenye migogoro kati ya Jeshi na wananchi ili kupunguza migogoro kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majumuisho ya Waziri, jambo hili hakulizungumzia na jambo hili limesemwa vile vile na Kambi Rasmi ya Upinzani ukurasa wa tano ikipendekeza pesa za ugharamiaji wa upimaji wa ardhi ziweze kuongezwa kupunguza migogoro. Kwa hiyo, ningepomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwa nini hakukubaliana na ushauri huo wa Kamati na ushauri wa Kambi ya Upinzani na kuhamisha hizo pesa kuelekea kifungu kinachohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo ufafanuzi huu hautaridhisha nitaomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ambayo inaruhusu Mbunge kutoa hoja ya kuhamisha



4 APRILI, 2013

kiwango cha pesa kwenye kifungu kimoja kupeleka kwenye kifungu kingine ili kuweza kutekeleza huu ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na ushauri wa Mheshimiwa Mnyika kwamba fedha hizi zihamishwe kupelekwa katika kifungu kingine, lakini tatizo langu ni kwamba, kitengo hiki cha *Estate Management and Development Unit*, ni kipya na kama kitengo ni kipya kinahitaji vifaa vya kufanyia kazi na hicho ndicho ambacho tumekifanya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kama Mbunge na Kamati walikuwa wanapendekeza pengine kitengo hiki kisingekuwepo, pengine hoja hiyo ingekuwa na maana na shughuli zake zikapelekwa kitengo kingine. Lakini kuondosha tu fedha wakati kitengo kipo na shughuli zake zipo, halafu fedha upunguze, nadhani hili wafanyakazi watakuwepo pale tu, lakini hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ndiyo hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kutokana na dakika tulizobakiza kwa sababu tunapaswa kumaliza saa nane kamili, kufuatana na kanuni zetu sasa ni wakati *guillotine*. Kwa hiyo, namwomba Katibu asome sasa fungu la mwisho kwa ujumla wake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 38 – Ngome

Kif. 1001 - *Defence Force Headquarters' Command...* ... Sh. 10,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa

Kif. 1001 – *The National Service Force...* ... Sh. 6,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Kif. 1003 - *Policy and Planning...* ... Sh. 100,000,000/=

Kif. 1009 - *Independent Telecommunication Network...* ... Sh. 5,221,914,000/=

Kif. 2001 - *Industries, Construction and Agriculture...* ... Sh. 33,577,920,000/=

Kif. 2002 - *Military Research and Development...* ... Sh. 186,232,193,000/=

Kif. 2004 - *Estate MGT & Development Unit...* ... Sh. 4,450,000,000/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yeyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## TAARIFA

### WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati imepitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Fungu 38, Jeshi la Wananchi

wa Tanzania; Fungu 39, Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa  
kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu na kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya kwa siku ya leo Jumamosi. Tumewezesha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuweza kupata bajeti yao kwa mwaka wa fedha ujao. Nawatakia kila la kheri Mkuu wa Majeshi na watumishi wengine wote wa Jeshi hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu matangazo, nimepata karatasi nyingi za Wabunge wakiuliza masuala yanayohusu utaratibu. Ni kwamba, utaratibu umekaa vizuri, kwa hiyo, wale ambao wanataka kupitia pitia kule *NMB*, basi mambo yamekaa sawa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia natangaza kuwa kesho kuna semina ya Wabunge wote, saa nne, Ukumbi wa Msekwa ambayo itasimamiswa na ndugu zetu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo inahusisha suala la mfumo mpya wa ufuatiliaji wa tathmini ya utekelezaji wa miradi na *program* za maendeleo, ambayo imeandaliwa na wenzetu wa Tume ya Mipango. Tume ya Mipango wanatuomba sana, semina hii ni muhimu sana, kesho saa nne kamili semina hii itaanza ukumbi wa Msekwa, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo langu la mwisho linatoka Kanisa la Anglikana la Tanzania likiwatangazia Ibada maalum ya kumsimika Askofu Mkuu wa Tanzania mpya ambayo itafanyika hapa katika Kanisa Kuu la Anglikana Dodoma ambapo Mheshimiwa Mhashamu Dkt. Jacobo Chimeledya.

Ibada hiyo itahudhuriwa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana duniani Justin Welby na mgeni rasmi atakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 18 Mei, 2013. Tunaombwa sote kuhudhuria na Wabunge ambao wana *interest* mnaweza mkajandikisha kupitia Mheshimiwa Margareth Mkanga kwa ajili ya zoezi hilo.

Waheshimiwa Wabunge, huyu Dkt. Jacobo Chimeledya, Askofu mpya wa Anglikana Tanzania atakayeapishwa siku hiyo ni mzaliwa na mpiga kura wa Kongwa. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zote zimekwisha hapa mezani, naomba sasa kuahirisha shughuli za Bunge mpaka keshokutwa Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 8.00 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 6 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*